

**HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA
UWEKEZAJI
MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE (MB.),
AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA
MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018**

1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuanzia tarehe 29 hadi 30 Machi, 2017, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mwaka 2017/2018.
2. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya, upendo, baraka, ulinzi na usalama unaotuwezesha kumudu majukumu, dhamana na wajibu wetu kwa Taifa na jamii nzima ya Watanzania. Naomba kazi njema za mikono yetu ziendelee kumpendeza na hivyo kupata kibali chake daima.
3. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi thabiti na maamuzi makini yanayotia chachu, ari na kasi ya utekelezaji wa mipango yenye tija na manufaa mapana kwa Taifa. Hatua hizo zimetoa msukumo wa kipekee katika kuimarisha uwajibikaji wa umma wa Watanzania katika kuchochaea maendeleo na vita dhidi ya umaskini.
4. ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuwa nguzo imara ya kuelekeza na kusimamia masuala yanayoimarisha ushirikiano wa masuala ya kisekta kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT)

5. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuongoza vyema shughuli za Serikali Bungeni na kusimamia vyema shughuli za Serikali bungeni. Pia, ninampongeza kwa hotuba yake yenye kutoa dira makini ya malengo, mipango na mwelekeo wa utendaji wa Serikali hususan katika kutekeleza mipango na programu za Serikali ya Awamu ya Tano kwa mwaka 2017/2018. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wamewasilisha Hotuba za Bajeti za mwaka 2017/2018 na kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

6. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuliongoza vema Bunge la Kumi na Moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano ya Uongozi wa nchi yetu. Tunashukuru kwa ushirikiano ambao Wizara na wadau wake wameendelea kuupata kutoka kwa wenyeviti wa kamati za kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kushika dhamana ya kusimamia na kuendeleza sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji nchini. Nami napenda kumhakikishia kuwa nitaendelea kujibidiisha kutekeleza jukumu hilo ili kukidhi matarajio ya Watanzania walio wengi kwa kuifanya Tanzania ya kesho kuwa ya matumaini makubwa zaidi kupitia maendeleo ya viwanda.

8. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, chini ya

Mwenyekiti wake Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki (CCM) na waheshimiwa wajumbe wote kwa namna ambavyo wameipokea, kuichambua na kushauri juu ya mambo ya msingi ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018, katika kuendeleza sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji. Napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Spika, ushauri na maelekezo ya Kamati, tunayathamini na tumeyazingatia katika kuandaa na kuboresha Hotuba ninayoiwasilisha.

9. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Alhaji Abdallah Majura Bulembo (Mb.), Mheshimiwa Anne Killango Malecela (Mb.); Mheshimiwa Juma Ali Juma (Mb.); Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.); Mheshimiwa Salma Rashidi Kikwete (Mb.); na Mheshimiwa Mch. Dkt. Gertrude Pangalile Rwakatare (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wabunge. Vilevile, nawapongeza wabunge wateule wa Bunge la Afrika Mashariki kwa ushindi wao. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Tunawakaribisha kuungana nasi katika shughuli hii muhimu ya kujenga Tanzania ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

10. *Mheshimiwa Spika*, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wapiga kura wangu wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kama mwakilishi wao katika Bunge hili tukufu. Aidha, naishukuru sana familia yangu hususan mke wangu, watoto, ndugu na jamaa kwa sala zao na kwa ushirikiano wao mzuri unaonipa nguvu na hamasa katika kuwatumikia Watanzania wenzangu.

11. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa uchumi wa nchi yetu na hususan maendeleo ya sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo, biashara ndogo na uwekezaji unategemea sana ushirikiano wa wananchi na wadau wote ndani na nje ya nchi. Hivyo, napenda kutambua na kushukuru taasisi za sekta binafsi za ndani na nje ya nchi, waandishi na wamiliki wa vyombo vya habari, Washirika wa

Maendeleo na Watanzania wote kwa ujumla. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

12. *Mheshimiwa Spika*, hotuba hii ya bajeti ninayoiwasilisha ni matokeo ya kazi nzuri na makini ya ushirikiano wa Menejimenti ya Wizara na taasisi zake. Hivyo, niruhusu niwapongeze Dkt. Adelhelm J. Meru, Katibu Mkuu – Viwanda; Prof. Adolf F. Mkenda, Katibu Mkuu-Biashara na Uwekezaji; Mhandisi Joseph K. Malongo, Naibu Katibu Mkuu; wenyeviti wa bodi, wakuu wa idara na vitengo; taasisi na watumishi wote wa Wizara. Nina imani kubwa kuwa ari hiyo itaendelea kuimarishwa kwa kutumia ipasavyo fursa, utaalam na ujuzi walionao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kisekta (*Jedwali Na. 1*).

13. *Mheshimiwa Spika*, naomba kuwapa pole ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mhe. Hafidh Ally Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Dimani (CCM) na Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Aidha, nawapa pole ndugu, jamaa marafiki na wananchi wote waliokumbwa na kadhia ya tetemeko la ardh, maafa ya mvua, ukame na ajali zilizotokea ambazo zimesababisha majeruhi, ulemavu, vifo na uharibifu mkubwa wa mali. Tunaomba Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa faraja timilifu.

14. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze majukumu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

2.0 MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

15. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ambayo imeundwa kwa Tamko la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili, 2016 ina majukumu yafuatayo:-

- (a) Kuandaa, kuratibu na kupitia Sera na mikakati ya sekta ya Viwanda, Biashara, Uwekezaji, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo;

- (b) Kufuatilia na Kuperemba (M&E) utendaji katika viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na taasisi zinazowezesha maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji;
- (c) Kubuni na kuandaa programu za kuendeleza sekta za viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na taasisi zinazowezesha maendeleo ya viwanda, biashara na uwekezaji;
- (d) Kukusanya, kuchambua, kusambaza na kutathmini taarifa za sekta za viwanda, biashara, uwekezaji, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo;
- (e) Kukuza na kuhamasisha biashara ya ndani na nje na kuboresha upatikanaji wa huduma za kuendeleza biashara;
- (f) Kuimarisha ufanisi wa utendaji wa wafanyakazi wa Wizara na taasisi zake;
- (g) Kusimamia utekelezaji wa sheria zinazosimamia viwanda, biashara na uwekezaji;
- (h) Kuimarisha utafiti wa maendeleo ya Sekta ya Viwanda;
- (i) Kusimamia utendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara;
- (j) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa sekta binafsi;
- (k) Kutafuta fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania; na
- (l) Kuratibu na kutoa mwongozo juu ya maendeleo ya uwekezaji na uboreshaji wa mazingira ya biashara.

16. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nieleze Mchangano na Mwelekeo wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika mwaka 2016/2017.

3.1 MCHANGO NA MWELEKEO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI KATIKA KULETA MAGEUZI YA UCHUMI

3.2 DHIMA YA MAGEUZI YA UCHUMI WA VIWANDA

17. *Mheshimiwa Spika*, Serikali ya Awamu ya Tano inaingia katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2016/2017 – 2020/2021 unaojikita katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Lengo kuu la Mpango huo ni kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati inayoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Ni dhahiri, Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani inahitaji uchumi wa viwanda ili kuleta mageuzi ya haraka na kujenga msingi imara wa uchumi. Uamuzi wa Serikali wa kujenga uchumi wa viwanda unalenga kuleta maendeleo jumuishi na endelevu kwa kutumia ipasavyo rasilimali zilizopo na hivyo kuchangia katika kukuza Pato la Taifa, kutoa nafasi nyingi na endelevu za ajira, kuzalisha na kukuza teknolojia zinazohitajika na kuwa chachu ya maendeleo ya sekta zinazohusiana na kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya masoko ya ndani na nje ya nchi.

18. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji umadhubuti na nguvu za ziada katika kusimamia na kutekeleza kwa vitendo uvutiaji wa wawekezaji, ujenzi wa viwanda, kulea na kulinda viwanda vya ndani na pia kupambana na nguvu za ushindani usio haki katika soko. Mfumo wa mahusiano ya kiuchumi kati ya mataifa makubwa na madogo duniani hauna urafiki wa kuachia nchi maskini zijitawale kiuchumi. Kwa hiyo, Wizara inaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kila Mtanzania kwa nafasi yake awe na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya soko, kufichua na kudhibiti mbinu chafu za soko, kuwa tayari kuwekeza na pia kutoa kipaumbele katika kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini.

3.3 SEKTA BINAFSI KATIKA UJENZI WA UCHUMI WA VIWANDA

19. *Mheshimiwa Spika*, kimsingi, sekta binafsi inajumuisha shughuli zote za uzalishaji kiuchumi zinazoendeshwa na watu binafsi, makampuni, taasisi pamoja na shughuli zinazohusisha ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Joint Ventures*). Kwa maana nyingine, sekta binafsi inajumuisha jasiriamali ndogo sana, ndogo na za kati (*Micro, Small and Medium Enterprises - MSMEs*) ambazo uzoefu duniani unaonesha ndizo zenye mchango mkubwa kwa maendeleo ya jamii. Katika ujenzi wa uchumi wa viwanda, sekta binafsi inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kutumia fursa zilizopo na zinazojitokeza katika uwekezaji, biashara na masoko. Pia, ina jukumu la kutoa ushirikiano unaohitajika (*Public-Private Dialogue*) katika jitihada zinazofanywa na Serikali za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, kupambana na mbinu chafu na zisizo haki katika soko zinazopunguza ushindani na kuboresha mbinu za uzalishaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kukidhi matakwa ya kuchochea maendeleo kwa wote. Hivyo, Serikali inategemea ushirikiano wa dhati kwa sekta binafsi kuunga mkono ipasavyo sera, programu, mikakati, sheria na kanuni zinazopigania, kutetea na kulinda maslahi ya Taifa.

20. *Mheshimiwa Spika*, maendeleo ya sekta binafsi na uwekezaji ndio msingi wa mipango mikuu ya maendeleo ya nchi yetu. Sera, mipango na mikakati mbalimbali ambayo Serikali imekuwa inaandaa, kuboresha na kutekeleza siku zote ina lengo la kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi iendelee kuwa mhimili wa uchumi na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya viwanda. Lengo ni kufikia Dira ya Maendeleo (2025) kwa kuweka misingi ya uchumi wa soko huria ili kuwa na uchumi wenye ushindani (*competitive economy*). Jukumu kubwa la Serikali katika mipango hiyo ni kuweka mazingira wezeshi ili sekta binafsi itimize wajibu wake wa kuwekeza na kuzalisha bidhaa na kutoa huduma.

21. *Mheshimiwa Spika*, Serikali inathamini jitihada za sekta binafsi zinavyoshiriki katika maeneo mbalimbali ya uwekezaji,

kushirikiana na sekta za umma na kuendesha shughuli za uzalishaji. Katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Serikali kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania ilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 242 ya sekta mbalimbali ambayo ilikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,079; na inayotarajiwa kutoa ajira mpya zipatazo 17,385. Kati ya miradi hiyo, miradi ya viwanda ni 170 ambapo miradi 54 ipo katika hatua ya ujenzi na miradi 17 imeanza uzalishaji. Kwa upande wa viwanda vidogo, SIDO imeweza kusajili viwanda vidogo 1,843 katika mikoa mbalimbali nchini. Serikali itaendelea kushirikiana kikamilifu na sekta binafsi katika maandalizi na maboresho ya sera, mikakati na sheria mbalimbali kwa kuhusisha wadau wa kisekta wakiwemo TPSF, TCCIA, CTI na TAFOPA kwa kutaja baadhi.

3.4 MCHANGO WA SEKTA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

3.3.1 Sekta ya Viwanda

22. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2016, shughuli za uzalishaji viwandani zilikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 6.5 mwaka 2015. Ukuaji huo ulitokana na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za vyakula, vinywaji na bidhaa za tumbaku. Ukuaji wa Sekta ya Viwanda wa asilimia 7.8 ni juu ya wastani wa ukuaji wa Pato la Taifa wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016. Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 5.1 ukilinganishwa na asilimia 5.2 katika mwaka 2015. Kwa mwaka 2016, Sekta ya Viwanda imetoa ajira 146,892 ikilinganishwa na ajira 139,895 zilizotolewa mwaka 2015. Ongezeko hilo la asilimia 7.1 kwa mwaka lilitokana na ajira mpya viwandani kufuatia uwekezaji katika upanuzi na uanzishaji wa viwanda vipyta nchini (*Jedwali Na.2a, 2b, 2c, 2d, 2e, 2f na 2g*).

3.3.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

23. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo nchini ni sekta muhimu katika kutengeneza ajira, kukuza kipato na kuondoa umasikini. Sekta hiyo ina jumla ya jasiriamali milioni 3.1 ambazo zimeajiri asilimia 23.4 ya nguvu kazi ya Taifa na imechangia asilimia 27 katika Pato la Taifa. Aidha, kulingana na takwimu za Sensa ya Viwanda ya mwaka 2013 iliyozinduliwa mwaka 2016, Tanzania ina jumla ya viwanda 49,243 ambapo asilimia 85.13 ni viwanda vidogo sana, asilimia 14.02 ni viwanda vidogo, asilimia 0.35 ni viwanda vya kati na asilimia 0.5 ni viwanda vikubwa. Takwimu hizo zinadhahirisha kuwa asilimia 99.5 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati (*Jedwali Na.3a*).

24. *Mheshimiwa Spika*, taswira ya takwimu hizo inaonesha wazi kuwa maendeleo ya viwanda Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingine yatatokana na kuweka nguvu katika sekta za viwanda vidogo, viwanda vidogo sana na vya kati. Hali hiyo siyo ya kushangaza kwa kuwa taswira kama hiyo inajitokeza pia katika nchi karibu zote duniani. Kwa mfano, Japan, viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati vinachukua takribani asilimia 99 ya Sekta ya Viwanda; Kenya asilimia 98; Malaysia asilimia 97.3; Indonesia asilimia 99.9; Canada asilimia 98 na Ujerumani asilimia 99. Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuviwezesha viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati kukua na kufanya kazi kwa tija zaidi.

25. *Mheshimiwa Spika*, faida ya Sekta ya Viwanda Vidogo ni kuwa uanzishwaji wake hauhitaji elimu kubwa na mtaji mkubwa na hivyo vinaweza kuanzishwa katika eneo lolote la nchi yetu. Sekta hiyo inatoa mwanya mkubwa kwa vijana na wanawake kuanzisha viwanda na kujajiri ambapo wasingepata fursa katika sekta nyingine zinazotoa ajira. Viwanda vidogo huongeza thamani ya mazao, hali ambayo humpatia kipato zaidi mzalishaji na kupunguza hasara baada ya mavuno. Sekta ya Viwanda Vidogo ni msingi muhimu wa kuwandaa Watanzania kuwa wamiliki wa viwanda vya kati na viwanda vikubwa hapo baadaye. Viwanda vidogo ni darasa kwani wale wanaoanza na viwanda vidogo sana huhitimu na kujenga viwanda vidogo, vya kati

na hatimaye viwanda vikubwa. Sekta ya Viwanda Vidogo husaidia kusambaa kwa viwanda nchi nzima hali ambayo pamoja na faida nyiningine, hupunguza wimbi la wananchi kutoka vijijini kuhamia mijini. Aidha, ujenzi wa viwanda kwa kutumia mfumo huo ndio hujenga Sekta ya Viwanda endelevu.

3.3.3 Sekta ya Biashara na Masoko

26. *Mheshimiwa Spika*, shughuli za biashara za jumla na rejareja, ukarabati wa magari na pikipiki na vifaa vingine vya nyumbani kwa mwaka 2016 zilikua kwa kasi ya asilimia 6.7 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.8 mwaka 2015. Kasi ya ukuaji wa shughuli hizo ulipungua kwa asilimia 1.1 kutokana na kushuka kwa mauzo ya bidhaa zilizoingizwa nchini katika mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. (*Jedwali Na. 3b*).

3.3.4 Sekta ya Uwekezaji

27. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea na jitihada za kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kuchangia ipasavyo katika uwekezaji nchini. Kutokana na jitihada hizo, Sekta ya Uwekezaji imeendelea kukua ikilinganishwa na nchi nydingi za Afrika Mashariki. Ripoti mbalimbali za uwekezaji duniani zinaonesha Tanzania imeongoza kwa kuvutia uwekezaji kwa mwaka 2016 katika Afrika Mashariki. Kwa mfano, Ripoti ya Uwekezaji ya Dunia (World Investment Report) ya mwaka 2016 inayotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) inaonesha kuwa Tanzania imevutia uwekezaji wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1,532 mwaka 2015, ikifuatiwa na Kenya Dola za Kimarekani 1,437 na Uganda Dola za Kimarekani 1,057. Vile vile, ripoti ya Shirika la *Quantum Global* inayotafiti hali ya uwekezaji katika nchi 54 za Afrika imeiweka Tanzania katika namba nane kutoka nafasi ya 19 mwaka 2015, ikiwa ni nchi pekee katika Afrika Mashariki kuwa katika nafasi kumi za juu. Ripoti hiyo inaangalia vigezo sita vikiwemo ukuaji wa uchumi, mzunguko wa fedha, ubadilishaji wa fedha, mazingira ya biashara, wingi wa watu na matumizi ya teknolojia na ubunifu.

28. *Mheshimiwa Spika*, takwimu hizo za nafasi nzuri ya nchi yetu kwenye uwekezaji zinaonekana pia katika viwango vyta uwekezaji nchini. Kwa mfano, takwimu za Benki ya Dunia zinaonesha uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa umekua kutoka asilimia 14.8 mwaka 1997 mpaka asilimia 31.3 mwaka 2015. Hivyo ni viwango vikubwa ikilinganishwa na wastani wa nchi za Afrika wa asilimia 21 – 22 na nchi zilizoendelea wa asilimia 23 - 25. Kwa kuwa uchumi wetu umekuwa ukikua, hiyo inaonesha bado kuna uwezekano mkubwa wa kuongeza kiwango cha uwekezaji nchini.

29. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo naomba sasa nitoe taarifa ya Utekelezaji wa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2016/2017.

4.0 UTEKELEZAJI WA MIPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/2017

30. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara imetekeleza mipango iliyooanishwa katika Ilani ya CCM ya 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017 – 2020/2021, ambayo imefafanuliwa kisekta katika Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano na Mpango Kazi wa 2016/2017. Aidha, Wizara imezingatia ahadi na maagizo ya viongozi wakuu wa Serikali, sera na mikakati mbalimbali ya kisekta, kitaifa na kimataifa. Mipango hiyo inatoa mwelekeo wa kisekta na kuwa mwongozo wa utekelezaji wa sekta za viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo na uwekezaji.

4.1 MALENGO YA MWAKA 2016/2017

31. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika kipindi cha mwaka 2016/2017, iliweka msukumo mkubwa katika kuimarisha uzalishaji na tija katika viwanda vilivyopo; kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipyta na kuhamasisha mauzo ndani na nje ya nchi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa

Tanzania. Pia, kushirikiana na sekta binafsi katika uanzishaji na kuendeleza viwanda vya msingi na vya kimkakati kupitia taasisi zake za NDC na EPZA na kuendeleza na kuimarisha taasisi za utafiti na maendeleo ya viwanda. Vilevile, kuboresha mazingira ya kufanya biashara, uwekezaji na uzalishaji; na kuendeleza taaluma na weledi wa watumishi wake ili kutoa huduma bora zaidi kwa wadau. Madhumuni ya hatua zote hizo ilikuwa ni kuchangia katika uboreshaji wa uchumi ili kujenga Taifa linalojitegemea na litakaloongozwa na uchumi wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

4.1.1 Maduhuli ya Serikali

32. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi **20,000,000,000** kutokana na ada za leseni, uuzaaji wa nyaraka za zabuni, faini kwa kukiuka Sheria ya Leseni pamoja na makusanyo mengine. Hadi kufikia Aprili, 2017, jumla ya Shilingi **11,298,764,130.71** zilikuwa zimekusanywa ikilinganishwa na Shilingi **8,910,207,736.69** zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2015/2016, sawa na ongezeko la Shilingi **2,388,556,394.02**. Ongezeko hilo linatokana na matokeo chanya ya uboreshaji wa mazingira ya biashara.

4.1.2 Matumizi

33. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilitengewa Shilingi **81,871,992,000** za matumizi. Kati ya hizo, Shilingi **41,871,992,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **40,000,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, Shilingi **5,304,997,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **36,566,995,000** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, katika Shilingi **5,304,997,000** zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **4,652,877,000** zilikuwa kwa ajili ya Wizara na Shilingi **625,120,000** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara.

34. *Mheshimiwa Spika*, bajeti yote ya maendeleo ya Shilingi **40,000,000,000** ilikuwa ni ya fedha za ndani. Katika matumizi ya

fedha za maendeleo, vipaumbele vilivyozingatiwa kwa fedha za ndani ni pamoja na kuendeleza Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga shilingi **10,000,000,000 (25%)**, Kuwezesha taasisi chini ya Wizara kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama ile inayosimamiwa na NDC- *Industrial Park* (TAMCO, Kibaha) shilingi **9,000,000,000 (23%)**; Mashirika ya tafiti za viwanda ya TIRDO, TEMDO na CAMARTEC Shilingi **1,500,000,000 (4%)**; Kuchangia (*counter part funds*) katika utekelezaji wa miradi ya MUVE, *Gender Mainstreaming, Support for Trade Mainstreaming*, ASDP, UNIDO, WRRB, NEDF, BEST na KAIZEN Shilingi **11,300,000,000 (28%)**; *Lake Natron/ Engaruka Soda Ash Project*, Kiwanda cha Matairi Arusha Shilingi **1,850,000,000 (5%)**; na kuendeleza biashara katika maeneo ya CBE, COSOTA, TANTRADE na SIDO Shilingi **6,350,000,000 (16%)**.

4.1.3 Fedha Zilizopokelewa kutoka Hazina

35. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017, Wizara ilikuwa imepokea Shilingi **39,393,067,796.49** sawa na asilimia **48** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka 2016/2017. Kati ya fedha hizo, Shilingi **31,630,307,171.49** ni za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **7,762,760,625.00** ni za Matumizi ya Maendeleo (fedha za ndani). Aidha, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi **31,630,307,171.49** zilizopokelewa kutoka Hazina, Shilingi **26,429,483,302.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na Shilingi **5,200,823,869.49** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Kwa upande wa fedha za maendeleo, Shilingi **7,566,620,625.00** sawa na asilimia **18.92** ya fedha za ndani na Shilingi **196,140,000** ni fedha za nje zilipokelewa kutoka Hazina. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa kutoka Hazina ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.4.**

4.2 UTEKELEZAJI WA MALENGO

4.2.1 Sekta ya Viwanda

a) Kuhamasisha Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda

(i) Ushirikiano wa Wizara na OR-TAMISEMI

36. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa, Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendesha kampeni za kuhamasisha Watanzania na taasisi mbalimbali kuchangamkia ujenzi wa uchumi wa viwanda. Zoezi hilo limehusisha kutenga maeneo ya kujenga viwanda na kufanya biashara, kuwahimiza na kuelimisha wananchi juu ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, kuvutia wawekezaji na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

(ii) Ushiriki wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

37. *Mheshimiwa Spika*, katika kuongeza kasi ya uwekezaji wa ndani, Shirikisho la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Tanzania Social Security Association - TSSA*) pamoja na Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF, PPF, LAPF, GEPF, PSPF na NHIF imehamasika kuwekeza katika ujenzi wa uchumi wa viwanda ambapo hadi Aprili, 2017 miradi 25 ya kuwekeza imebainishwa. Baadhi ya miradi hiyo ni mradi utakaoteklezwa kwa ushirikiano kati ya mifuko ya PPF na NSSF ya kuendeleza eneo la Mkulazi kwa ajili ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari; PPF imeingia mkataba na Gereza la Karanga kwa ajili ya kutengeneza viatu; LAPF inafanya majadiliano ili kuwekeza kwenye Kiwanda cha Chai Mponde; GEPF imesaini makubaliano ya kuwekeza katika Kiwanda cha Mvinyo Dodoma pamoja na kuwekeza katika ujenzi wa kinu cha kuyeyusha chuma katika Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Corporation (KMTC)*, Moshi. Vilevile, TSSA imeanza majadiliano na Kiwanda cha Urafiki kwa ajili ya kuzalisha mavazi. **(Jedwali Na.5)**

(iii) Ushirikiano na Sekta Binafsi

38. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda nchini. Kupitia Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), Wizara ilishiriki katika utoaji wa Tuzo za Mzalishaji Bora wa mwaka (*11th Presidential Manufacturers of the Year Awards*) ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Wizara iliandaa kampeni ya kuhamasisha ununuzi wa bidhaa za ndani ijulikanayo kama *Top 50 Tanzania Brands*. Mpango huo ulibuniwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) pamoja na TPSF ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazozalishwa nchini zinafikia viwango vya kitaifa na vile vya kimataifa na hivyo kuongeza ushindani kwenye soko.

39. Mheshimiwa Spika, baadhi ya washindi wa tuzo hizo ni *Kilimanjaro Lager, Konyagi, Superdoll, Twiga Cement, Azam Embe, Azania Wheat Flower, Sundrop Cooking Oil, Whitedent* na *Grand Malt*. Baadhi ya washindi kwenye kundi la wajasiriamali wadogo na wa kati ni *Alaska Rice, Asali ya Bibi, Chocolate Mama, Nelwa's Delight Ice Cream* na *Nuya's Essence*. Aidha, Mkurugenzi wa *Nuya's essence*, Bi. Hellen Dausen alitambuliwa na jarida maarufu la *Africa's Most Promising Entrepreneurs* (Forbes Africa's Under 30 for 2016). Washindi wa tuzo hizo mbili za CTI na TPSF wameoneshwa kwenye *Jedwali Na.6a* na *6b*.

(iv) Kutenga Maeneo ya Viwanda katika Mikoa

40. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kuelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia mikoa na wilaya kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda. Lengo la mpango huo ni kuwa na maeneo ya kutosha kujenga viwanda sasa na baadae. Hadi Aprili, 2017 mikoa 13 imetoa taarifa ya utengaji wa maeneo hayo na kuwasilisha taarifa zao ambapo mkoa wa Kigoma umetenga ekari 451.46; Kilimanjaro ekari 53,033.16; Simiyu ekari 807.06; Shinyanga ekari 33,637.63;

Tanga ekari 33,788.62; Mbeya ekari 6,618.83; Pwani ekari 63,065.2; Dodoma ekari 54,614.16; Singida ekari 15,442; Mwanza ekari 11,204.3; Njombe ekari 15,662.29; Lindi ekari 8,790.52; na Geita ekari 472 na viwanja 144.

41. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa na Serikali chini ya mpango wa SEZ katika maeneo ya Kigoma (KISEZ) hekta 3,000; Bunda (Bunda SEZ) hekta 1,360; Ruvuma-SEZ hekta 2,033; Manyoni-SEZ hekta 1,909, kwa mwaka 2016/2017, eneo lenye ukubwa wa hekta 63,000 lililopo Mkulazi-Morogoro limekabidhiwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PPF kwa ajili ya kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari chini ya *Mkulazi Holdings Co. Ltd* iliyoundwa kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza mradi huo. Upatikanaji wa maeneo hayo unatoa nafasi kwa Serikali na sekta binafsi kuyaendeleza kwa kuyawekea miundombinu ya msingi ili kuvutia wawekezaji na kuongeza idadi ya viwanda nchini. Serikali itaendelea kukamilisha malipo ya fidia kwa maeneo yaliyobaki na kuyawekea miundombinu wezeshi.

b) Sensa ya Viwanda

42. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na UNIDO, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilikamilisha Ripoti ya Sensa ya Viwanda ya mwaka 2013 na kuzinduliwa rasmi mwezi Oktoba 2016. Ripoti hiyo inaonesha kuwa, Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 49,243 (*Jedwali Na.7a*), ambapo asilimia 85.13 ni viwanda vidogo sana, asilimia 14.02 ni viwanda vidogo, asilimia 0.35 ni viwanda vyatka kati na asilimia 0.5 ni viwanda vikubwa. Takwimu hizo zinadhahirisha kuwa, asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo sana na viwanda vidogo. Aidha, juhudhi za Serikali za kuhamasisha uwekezaji katika kukuza uchumi kupitia viwanda umewezesha kuongeza uwekezaji katika viwanda.

c) Miradi ya Viwanda

43. *Mheshimiwa Spika*, tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani hadi kufikia mwezi Machi, 2017, miradi ya viwanda

vikubwa 393 yenye jumla ya mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 2,362.59 (Shilingi trilioni 5.198) inayotarajiwa kutoa ajira 38,862 imesajiliwa. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na mingine katika hatua za mwisho za kuanza uzalishaji. Kati ya miradi hiyo, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 224 (**Jedwali Na.7b**); Mamlaka ya EPZ imesajili miradi 41 (**Jedwali Na.7c**) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesajili miradi 128 (**Jedwali Na.7d**). Aidha, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limeratibu uanzishwaji wa viwanda vidogo 1,843.

d) Viwanda Vilivyoanzishwa

44. *Mheshimiwa Spika*, kwa muhtasari naomba niwapitishe katika baadhi ya viwanda ambavyo vimeanzishwa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017.

(i) *Viwanda vya Kuzalisha Chuma na Bidhaa za Chuma*

45. *Mheshimiwa Spika*, kwa sasa Tanzania kuna jumla ya viwanda 22 vya chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo vimeendelea kuongeza uzalishaji mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2015, viwanda hivyo vilizalisha tani 62,612 na mwaka 2016 tani 65,686 (**Jedwali Na.3a**). Uwekezaji katika uzalishaji wa chuma na bidhaa za chuma umeendelea kuongezeka ambapo viwanda vitatu tayari vimefanya uwekezaji katika Mkoa wa Pwani. Kiwanda cha *Kiluwa Steel* kilichopo Mlandizi mkoani Pwani kimewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 41 sawa na Shilingi bilioni 90.2 na kina uwezo wa kuzalisha tani 500,000 kwa mwaka na kutoa ajira 800. Kiwanda hicho kimeanza uzalishaji. Kiwanda cha *Lodhia Steel Industry* kilichopo Mkuranga kimewekeza mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 9.35 sawa na Shilingi bilioni 20.57 na kinatarajia kutoa ajira 300. Aidha, kiwanda cha tatu ni *Lake Steel and Allied Products Ltd* kinachojengwa Kibaha, Pwani. Kiwanda hicho kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 13 sawa na Shilingi bilioni 28.6 na kitazalisha tani 168,000 za chuma kwa mwaka na kitaajiri wafanyakazi 120. Ujenzi wake upo katika hatua ya msingi.

(ii) *Viwanda vya Saruji*

46. *Mheshimiwa Spika*, nchi yetu kwa sasa ina viwanda 11 vya kuzalisha saruji vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani milioni 10.8 kwa mwaka ilihali mahitaji ya soko la ndani ni tani milioni 4.8. Kiasi cha juu cha uzalishaji kilichowahi kufikiwa na viwanda vyetu ni tani milioni 7.1 kwa mwaka. Ongezeko la uwezo wa uzalishaji na kiasi kilichozaishwa kwa mwaka 2016/2017 limechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukamilika kwa ujenzi wa Kiwanda cha *Dangote* chenyе uwezo wa kuzalisha tani milioni 3 kwa mwaka kilichowekeza Dola za Kimarekani milioni 568.1 sawa na Shilingi trilioni 1.25 na kutoa ajira 1,150; upanuzi wa *Tanga Cement Co. Ltd* kwa tani 500,000 kutoka tani tani 750,000 hadi tani 1,250,000 kwa mwaka uliogharimu Dola za Kimarekani milioni 152 sawa na Shilingi bilioni 334.4 na upanuzi wa *Mbeya Cement Co. Ltd* kwa tani 710,000 kutoka tani 400,000 hadi tani 1,100,000 uliogharimu Euro milioni 50 sawa na Shilingi bilioni milioni 154. Ongezeko hilo la uzalishaji limeongeza ajira 1,185 za moja kwa moja na 3,167 zisizo za moja kwa moja. Aidha, Sekta ya Saruji kwa kiasi kikubwa imechangamsha sekta nyingine za uchumi ikiwa ni pamoja na ujenzi, usafirishaji, uchimbaji wa madini na nishati kwa kutaja baadhi.

47. *Mheshimiwa Spika*, juhudu zimefanyika na kuweza kupata wawekezaji zaidi katika Sekta ya Saruji. Kampuni ya *Motisun* itawekeza kiwanda cha saruji Chapa Mamba chenyе uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka na kitajengwa mkoani Pwani. Kampuni ya *Hengya Cement Co. Ltd* imekamilisha taratibu zote za uwekezaji katika uzalishaji wa saruji mkoani Tanga. Kiwanda hicho ambacho kitazalisha saruji kwa kulenga soko la ndani na kimataifa uwekezaji wake ni Dola za Kimarekani bilioni 2.35 sawa na Shilingi trilioni 5.17 na utafanyika kwa awamu mbili hadi kufikia uwezo wa kuzalisha jumla ya tani milioni 7 za saruji kwa mwaka. Mradi huo mkubwa utakapokamilika unategemewa kutoa ajira za moja kwa moja 8,000 (**Jedwali Na.8**). Mafanikio katika uwekezaji wa Sekta ya Saruji ndio umesababisha kushuka kwa bei ya saruji nchini.

(iii) *Viwanda vya Vigae(tiles)*

48. *Mheshimiwa Spika*, kwa miaka mingi, nchi yetu haikuwa na viwanda vya vigae. Kutokuwepo kwa viwanda hivyo kulisababisha nchi kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, mwaka 2015 nchi ilitumia Dola za Kimarekani milioni 90.61. Juhudi za kuhamasisha uwekezaji nchini zimezaa matunda na kuwezesha viwanda viwili vikubwa vya kuzalisha bidhaa hizo kuanzishwa. Viwanda hivyo ni Kiwanda cha Vigae cha *Goodwill Ceramic Ltd* kilichopo Kijiji cha Mkiu Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani. Uwekezaji katika kiwanda hicho umegharimu Dola za Kimarekani milioni 50 sawa na Shilingi bilioni 110. Kiwanda hicho kilichowekwa jiwe la msingi na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania tarehe 2 Machi, 2017 kimeanza uzalishaji. Kiwanda hicho kitazalisha vigae mita za mraba milioni 20 kwa mwaka na kitatoa ajira 4,500.

49. *Mheshimiwa Spika* kiwanda cha pili ni *Twyford* kilichopo Chalinze kilichowekwa jiwe la msingi na Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji tarehe 22 Januari, 2017, kinategemewa kukamilika na kuanza uzalishaji mwezi, Agosti 2017. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha vigae mita za mraba milioni 12.5 kwa mwaka na kutoa ajira 6,000 kati ya hizo 2,000 za moja kwa moja na 4,000 zisizo za moja kwa moja. Viwanda vyote viwili vinategemea malighafi za ndani kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 95. Sekta zitakazofaidika ni pamoja na madini ujenzi, usafirishaji, makaa ya mawe na gesi asilia.

(iv) *Viwanda vya Nguo na Mavazi*

50. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendeleza Sekta ya Nguo nchini, Wizara kupitia Mradi wa *Supporting Indian Trade and Investment for Africa (SITA)* iliandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi (*Cotton to Clothing Strategy-C2C*), 2016-2020, uliozinduliwa Mei 2016. Mkakati huo unatoa mwongozo wa kuendeleza mnyororo wa uongezaji thamani kuanzia pamba hadi mavazi kwa kubainisha hatua za kuchukuliwa kutatua changamoto zinazokwamisha uwekezaji na uendelezaji viwanda. Wizara imekuwa ikikutana na wazalishaji

na kujadiliana jinsi ya kutatua kero zinazowakabili. Mawasiliano yamefanyika na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kushughulikia kero ya *under invoicing and under-declaration* hususan kwa bidhaa kutoka nje; Shirika la Viwango Tanzania limeelekezwa kudhibiti bidhaa zisizo na ubora zisiingie sokoni na Tume ya Ushindani Tanzania imeelekezwa kudhibiti bidhaa bandia.

51. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia NDC imefanya majadiliano na *Gatsby Africa* kwa kushirikisha Kitengo cha Nguo na Mavazi (Textile Development Unit -TDU) ili kuandaa Mpango Kabambe (*Master Plan*) kwenye eneo la ekari 95 maalum kwa viwanda nya nguo TAMCO Kibaha. Wizara imefanya majadiliano na kuzishawishi taasisi za Serikali hususan majeshi na hospitali ili wanunue nguo na mavazi yanayozalishwa na viwanda nya ndani. Aidha, mafunzo ya useketaji nguo (weaving) kwa kutumia mashine za mikono (*Handlooms*) yalitolewa kwa waseketaji 89 katika Chuo cha VETA Tabora. Wahitimu hao wameweza kujiajiri na wanaendesha shughuli zao katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Morogoro. Pamoja na kufanya shughuli zao, wahitimu hao wanatoa mafunzo kwa waseketaji wengine.

52. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na wataalam chini ya Mradi wa SITA ilitoa mafunzo kwa wazalishaji (artisans) 30 kuhusu usanifu wa mavazi, mbinu za useketaji bora kwa kutumia mashine za mikono na uwekaji rangi (tie & dye). Pia, taasisi za VETA na Kampuni za: *Shime Sanaa Machinga Complex Tie & Dye* na *Hand Made in Tanzania* kila moja ilitoa mwakilishi mmoja ambao waliwezeshwu kupata mafunzo ya utumiaji rangi za asili (natural die) huko Hyderabad, India. Vilevile, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia msaada wa *Gatsby Africa*, kimeendelea kutoa mafunzo ya Shahada ya Teknolojia ya Nguo (*Textile Degree*) ambapo, mwaka 2016/2017 Chuo kilitoa wahitimu 44 ikilinganishwa na wahitimu 13 kwa mwaka 2015/2016. Lengo ni kuhakikisha kuwa kuna wataalam wa kutosha wa fani ya ubunifu na uzalishaji mavazi nchini.

(v) Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi

53. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Ngozi ni mojawapo ya sekta zenyenye mnyororo mrefu wa uongezaji thamani na hivyo kuwa na uwezo wa kutoa ajira nyingi. Kwa mwaka 2016/2017, Wizara imefanya kazi kwa karibu na wadau wa Sekta ya Ngozi kwa lengo la kuongeza thamani ngozi ya hapa nchini. Mawasiliano yenyenye matumaini yamefanyika na wawekezaji wa viwanda vya Mwanza na *Morogoro Tanneries* ili kuongeza uwezo wa kusindika ngozi kutoka hatua ya mwanzo hadi ya mwisho (wetblue, crust to finished). Kiwanda cha Viatu cha Bora kimesimika mtambo wenye uwezo wa kuzalisha jozi za viatu vya ngozi 25,000 kwa mwaka maalum kwa ajili ya matumizi ya usalama na viwandani. Pia, kiwanda hicho kimekamilisha kufunga mitambo mitatu yenyenye uwezo wa kuzalisha viatu jozi 500,000 kwa kutumia teknolojia ya PVC; viatu aina ya raba jozi 500,000 kwa ajili ya michezo na hospitali na viatu vya *Canvas* jozi 500,000 kwa mwaka.

54. Mheshimiwa Spika, kiwanda cha kutengeneza viatu vya ngozi kinachomilikiwa na Jeshi la Magereza kilichopo Karanga Moshi kinaendesha mradi kabambe wa kuongeza uwezo wa uzalishaji. Lengo ni kutumia kiwanda hicho kuzalisha ikiwa ni pamoja na bidhaa nyingine kama soli za viatu kwa ajili ya viwanda vingine. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF upo tayari kuwekeza Shilingi bilioni 56.64 katika mradi huo hali itakayoongeza ajira za moja kwa moja 707. Kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), mafunzo maalum ya kuchuna na kusindika ngozi yamekuwa yakiendeshwa sehemu mbalimbali za nchi. Kupitia Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi na Ajira), Chuo cha Teknolojia ya Ngozi cha Mwanza (DIT Kampasi ya Mwanza) kilitoa Mafunzo ya Stadi za Kutengeneza Viatu vya Ngozi yanayohusisha usanifu, ukataji ngozi na utengenezaji viatu vya ngozi kwa vijana 100 kutoka mikoa 11 ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza na Tanga na mafunzo ya kutengeneza mipira ya miguu kwa vijana 25 kutoka mikoa sita ya Kagera, Mara, Morogoro, Mwanza, Pwani na Shinyanga. Aidha, mkufunzi mmoja kutoka Chuo hicho amepata mafunzo huko Uturuki

ya *Eco-friendly leather production technologies, waste management in leather production* chini ya ufadhili wa UNIDO. Pia, kwa mwaka 2016/2017, sekta binafsi imejasiria uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati vya bidhaa za ngozi.

(vi) Viwanda vya Kusindika Nyama

55. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Usindikaji wa Nyama ni sekta muhimu katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Juhudi zimefanyika katika kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo ambapo eneo la ekari 6,000 limepatikana kwa ajili ya kuanzisha Kiwanda cha Nyama cha *Nguru Hills Ranch* eneo la Makunganya Wilaya ya Mvomero Mkoa wa Morogoro. Kiwanda kimeanzishwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Zubair Corporation* ya Muscat, Oman na *Busara LLC*. Mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 13.741 sawa na Shilingi bilioni 30.23 zimekwishawekezwa. Kampuni ipo katika mazungumzo na wadau wengine ili kupata Shilingi bilioni 3.892 za kukamilisha mradi huo. Kiwanda hicho ambacho kimesajiliwa na Mamlaka ya EPZ kitasindika nyama ya ng'ombe na mbuzi kwa ajili ya soko la nje na kitakuwa na uwezo wa kusindika ng'ombe 50,000 na mbuzi 60,000 kwa mwaka, kutoa ajira za moja kwa moja 350 na kutoa fursa ya ajira zisizo za moja kwa moja ikiwemo kilimo cha nafaka na majani maalum kwa ajili ya kulishia mifugo.

56. *Mheshimiwa Spika*, Kiwanda cha Nyama cha *Meat King Limited* kilichopo eneo la Moshono, Mkoa wa Arusha kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 2.5 sawa na Shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya kuongeza uwezo wa uzalishaji wa kiwanda hicho kinachosindika nyama ya ng'ombe, kuku na kondoo. Kiwanda hicho kinatoa ajira 45 za moja kwa moja na 500 zisizo za moja kwa moja. Kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kusindika kilo 900,000 za nyama kwa mwaka na kinalenga kuuza bidhaa zake katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Aidha, kufuatia kufungwa kwa kiwanda cha Nyama cha Manyara, Wizara inawasiliana na wadau ili kuona uwezekano wa kurudisha katika uzalishaji kiwanda hicho ili kuweza kusaidia kununua mifugo ya wananchi.

(vii) **Viwanda vya Chakula, Mbogamboga na Matunda**

57. *Mheshimiwa Spika*, tatozo la kuharibika kwa matunda yanayolimwa nchini limeanza kupatiwa ufumbuzi baada ya wawekezaji watatu kupatikana na kuanza ujenzi wa viwanda katika maeneo ya Mboga - Chalinze na Mapinga-Bagamoyo Mkoa wa Pwani. Kiwanda cha *Sayona Fruits Limited* kinachojengwa eneo la Mboga-Chalinze kitasindika matunda mbalimbali ikiwa ni pamoja na nyanya. Mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 55.17 sawa na Shilingi bilioni 121.374 umewekezwa na kinatarajia kuzalisha lita milioni 91.65 za juisi kwa mwaka. Kiwanda hicho kinatarajiwa kutoa ajira za moja kwa moja 825 na zisizo za moja kwa moja 30,000. Aidha, Kiwanda cha Bakhresa Food Product Ltd kinachosindika matunda katika eneo la Mkuranga - Pwani, kilifanya upanuzi na kuzinduliwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 6 Oktoba, 2016. Upanuzi huo uliongeza uwezo wa usindikaji matunda tani 37,500 hadi tani 75,000 kwa mwaka. Upanuzi huo uligharimu mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 7.0 sawa na Shilingi bilioni 15.4 na kuongeza ajira za moja kwa moja 150 kutoka 150 hadi 300.

58. *Mheshimiwa Spika*, Kiwanda cha *Elven Agri Company Limited* kinachotumia teknolojia ya kukausha matunda na mahsusii kikilenga matunda yaliyozalishwa kwa kutumia kilimo hai (organic fruits) kitakuwa na uwezo wa kukausha matunda tani 2,500 na kusindika tani 1,000 za nyanya kwa mwaka. Kiwanda kitatoa ajira za moja kwa moja 300 bila kuhusisha ajira kwa wakulima watakaozalishwa matunda kwa kiwanda hicho. Bidhaa zitakazozalishwa na kiwanda hicho zitauzwa katika masoko ya nje. Kiwanda cha *Vegeta PadraVka Limited* kilichopo Bagamoyo Mkoa wa Pwani kimewekeza katika ukaushaji wa mbogamboga kwa ajili ya kutengeneza vionjo vya chakula (*food seasoning*). Uzinduzi wa kiwanda hicho ulifanyika mwezi Machi, 2017 na kinatarajia kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 4.5 sawa na Shilingi bilioni 9.9 na kinatarajiwa kutoa ajira 63 za moja kwa moja. Aidha, kiwanda kitashirikisha wananchi ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ili washiriki katika kilimo cha mbogamboga

kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya malighafi kwa kiwanda.

59. *Mheshimiwa Spika*, Kiwanda cha Kutengeneza Makaroni (pasta) cha aina yake kimeanzishwa hapa nchini katika eneo la Vingunguti, Dar es Salaam kwa ajili ya kuzalisha makaroni (pasta) kwa kutumia malighafi ya ‘Semolina’. Dola za Kimarekani milioni 16 sawa na Shilingi bilioni 35.2 zimewekezwa. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 29,200 kwa mwaka. Kwa vile malighafi inayotumiwa na kiwanda hicho kwa sasa inatoka nje ya nchi, mwekezaji amewekeza Dola za Kimarekani milioni 2.5 sawa na Shilingi bilioni 5.5 katika mtambo wa kuongeza thamani (milling plant) wenyewe uwezo wa kusaga tani 50,000 za *Semolina* kwa mwaka. Kiwanda hicho kipo mbioni kukamilika.

60. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya *Jambo Group Ltd* imeanzisha kiwanda cha *Jambo Food Products Company Ltd* katika Mkoa wa Shinyanga cha kuzalisha maji, juisi na soda. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha lita za ujazo milioni 1.95 kwa mwaka na kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 35 sawa na Shilingi bilioni 77. Ajira 500 za moja kwa moja na 1,500 zisizo za moja kwa moja zitatengenezwa. Kampuni inatarajia kuongeza uwekezaji wa Dola za Kimarekani milioni 40 sawa na Shilingi bilioni 88 ifikapo Desemba 2017 ili kuongeza uzalishaji zaidi.

(viii) **Viwanda vya Maziwa**

61. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya *Watercom Ltd* imejenga Kiwanda cha Kusindika Maziwa eneo la Kigamboni, Mkoa wa Dar-es-Salaam ambacho kitatumia teknolojia ya *Ultra Heat Treatment (UHT)* ambayo huzalisha maziwa yenye ubora wa hali ya juu. Kiwanda hicho kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 20 sawa na Shilingi bilioni 44 na kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 67.5 za maziwa kwa mwaka na kutoa ajira 500. Kampuni hiyo pia imeanzisha Kiwanda cha *Watercom Ltd* kwa ajili ya kuzalisha maji ya kunywa aina ya Afya. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha lita milioni 125 za maji kwa mwaka, kimewekeza Dola za Kimarekani milioni 25 sawa na Shilingi bilioni 55 na kinatoa ajira 1,270. Kampuni ya *Watercom Ltd* pia iko

mbioni kuanzisha kiwanda cha kutengeneza juisi na vinywaji baridi kitakachowekeza Dola za Kimarekani milioni 40 sawa na Shilingi bilioni 88 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 275 za vinywaji kwa mwaka na kutoa ajira 3,500.

(ix) Viwanda vya Mafuta ya Kula

62. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania ina fursa ya kuzalisha mafuta ya kula kwa ajili ya matumizi ya ndani na ziada kuuzwa nje ya nchi. Uzalishaji wa mafuta ya kula kwa sasa ni tani 180,000 wakati mahitaji yanakadiriwa kuwa tani 400,000 kwa mwaka. Hivyo, asilimia 55 ya mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni mafuta ya mawese (*palm oil*) yanayoagizwa kutoka nje ya nchi. Inakadiriwa kuwa mafuta ya alizeti yanayozalishwa yanatosheleza mahitaji ya ndani kwa asilimia 40 tu. Changamoto kubwa katika uzalishaji wa mafuta ya alizeti nchini inatokana na upungufu wa mbegu zenyе ubora stahiki wa kutoa mafuta kwa wingi. Kutokana na hali hiyo, Serikali kwa kushirikisha wadau katika Sekta ya Mafuta ya Kula iliandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ndogo ya Alizeti uliozinduliwa mwezi Mei, 2016.

63. *Mheshimiwa Spika*, tangu kuzinduliwa kwa Mkakati wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Alizeti, yafuatayo yamekwishafanyika:

- a) Ekari 75 za ardhi kwa ajili ya kujenga Kongano la Mafuta ya Alizeti katika eneo la Chamwino, Dodoma limepatikana. Barabara ya urefu wa Kilometa moja kutoka barabara kuu ya Dar es Salaam - Dodoma hadi eneo la mradi na barabara za ndani zenyе urefu wa jumla ya Kilometa tano zimejengwa kwa kiwango cha changarawe;
- b) Kwa lengo la kupata malighafi ya uhakika katika kongano hilo, eneo la ekari 15,000 limebainishwa na kuunganishwa na wakulima 370;
- c) Wazalishaji wa mafuta ya alizeti 31 wamepewa mafunzo ya viwango vya ubora unaokidhi matakwa ya soko la ndani, kikanda na kimataifa;
- d) Kupitia Mradi wa SITA, mkutano kati ya wazalishaji wa mafuta ya alizeti wa Tanzania na India ulifanyika Dodoma tarehe 27 Julai, 2016 kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji na

- uhaulishaji wa teknolojia;
- e) Kuanzishwa kwa Jukwaa la Wadau wa Alizeti (*Sunflower Round Table*) chini ya Mradi wa SITA na usimamizi wa Chama cha Wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti Tanzania (Tanzania Sunflower Processors Association-TASUPA). Jukwaa hilo limezindua miradi miwili ya:
- i) Kilimo cha kuzalisha aina nne (4) ya mbegu bora (certified seeds) za Alizeti;
 - ii) Kuendeleza Kongano za Wasindikaji Mafuta ya Alizeti zikiwepo za Dodoma, Singida na Kondoa; na
- f) TASUPA imeingia makubaliano na Benki ya Dunia ya kuendeleza miundombinu katika Kongano za Kusindika Alizeti zitakazojengwa.

(x) Viwanda vya Sukari

64. *Mheshimiwa Spika*, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa sukari ya majumbani na ya viwandani kutokana na kuwa na mahitaji makubwa kuliko uwezo wa uzalishaji wa ndani. Utafiti uliofanywa na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) kwa kutumia Kampuni ya *LMC International*, ulibaini mahitaji ya sukari kwa mwaka 2016/2017 ni wastani wa tani 590,000 ambapo kati ya hizo, tani 455,000 ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na tani 135,000 kwa matumizi ya viwandani. Malengo ya uzalishaji kwa msimu wa 2016/2017 yalikuwa tani 329,169 ambapo kufikia tarehe 19 Aprili, 2017 msimu wa uzalishaji ulipofungwa, jumla ya tani 330,843.48 zilikuwa zimezalishwa. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 100.51 ya malengo ya uzalishaji.

65. *Mheshimiwa Spika*, katika kutatua changamoto ya uhaba wa sukari nichini, Serikali iliainisha maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya upandaji miwa katika mabonde mbalimbali nichini pamoja na kuvutia uwekezaji wa viwanda vipyta na kuongeza uwezo wa uzalishaji wa viwanda vilivyopo. Kiwanda cha *Kagera Sugar Estate Ltd* kinapanua uwezo wa uzalishaji kufuatia makubaliano na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSPF ya kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 20 sawa na Shilingi bilioni 44. Upanuzi huo utaongeza ajira 1,000 kutoka 2,500

za sasa hadi 3,500. Aidha, hadi kufikia Aprili 2017, Kampuni ya *Mkulazi Holdings* ambayo ni ya ubia kati ya Mifuko ya Jamii ya NSSF na PPF itawekeza katika kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza sukari ya majumbani katika eneo la *Mkulazi Morogoro*. Kiwanda hicho kitazalisha tani 200,000 za sukari kwa mwaka na kutengeneza ajira zipatazo 100,000. Aidha, Jeshi la Magereza limeingia ubia na Mifuko ya Jamii ya NSSF na PPF ili kufufua na kuendeleza mashamba na Kiwanda cha Sukari *Mbigiri Morogoro* chenye uwezo wa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka (*Jedwali Na.9*).

(xi) Viwanda vya Vifungashio

66. *Mheshimiwa Spika*, ili kukidhi mahitaji ya vifungashio kwa soko la ndani na nchi jirani viwanda vya kuzalisha vifungashio vimejengwa kwa mafanikio. Kiwanda cha *Lakairo Polybag* kilichojengwa *Mwanza* kwa gharama ya Shilingi bilioni 4 chenye uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi (polypropylene bags) milioni 10 kwa mwaka na kinaajiri watu 85. Kiwanda cha *Global Packaging* kilichopo *Kibaha* kilichowekeza Shilingi bilioni 8 kina uwezo wa kuzalisha magunia ya sandarusi milioni 11.75 kwa mwaka na kinaajiri watu 110. Wizara inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika eneo hilo ili kukidhi mahitaji ya vifungashio kwa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani.

(xii) Viwanda vya Mbolea

67. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya *Ferrostaal Consortium Ltd* kwa ushirikiano na TPDC itawekeza Dola za Kimarekani bilioni 1.982 sawa na Shilingi trilioni 4.360 kwa ajli ya kujenga kiwanda cha mbolea katika eneo la *Kilwa Masoko, Lindi*, chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 1.3 za mbolea kwa mwaka. Kampuni ya *Helm* itawekeza Dola za Kimarekani bilioni 1.2 sawa na Shilingi trilioni 2.640 ili kujenga kiwanda chenye uwezo wa kuzalisha tani milioni 1.365 za mbolea kwa mwaka katika eneo la *Msanga Mkuu, Mtwara Mikindani*. Majadiliano ya kufanikisha uanzishwaji wa miradi hiyo yanaendelea. Wizara imeshiriki katika kufanikisha miradi hiyo kwa kufuatilia ukamilishaji wa majadiliano hasa uamuzi juu ya bei ya gesi itakayotumika kutengenezea mbolea.

(xiii) Viwanda vya Dawa za Binadamu

68. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2016/2017, Serikali imefanya uhamasishaji mkubwa kuvutia uwekezaji kwenye Sekta ya Dawa za Binadamu. Lengo ni kuhakikisha viwanda vipywa vinajengwa na kufufua vilivyofungwa ikizingatiwa kuwa takriban asilimia 90 ya dawa muhimu (Essential Drugs) zinazotumika nchini huagizwa kutoka nje. Juhudi za uhamasishaji wa uwekezaji katika sekta hii zimeendeshwa kwa ushirikiano mkubwa kati ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto chini ya usimamizi mahiri wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

69. Mheshimiwa Spika, mradi wa kutengeneza vifaa tiba vitokanavyo na pamba (medical textile) utakaojengwa Mkoa wa Simiyu ulibuniwa na kamati maalum inayohusisha wataalamu kutoka taasisi za MSD, NHIF, TIRDO, TIB na TFDA. Mradi huo utakaojengwa na NHIF utakuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 36.5 sawa na Shilingi bilioni 80.3. Tani 50,000 za pamba zitatumika kwa mwaka na kutoa ajira 1,600 za moja kwa moja na 5,000 zisizo za moja kwa moja. Mradi wa *Zinga Pharmaceutical Ltd* unaoanzishwa na Watanzania katika eneo la Zinga, Bagamoyo utazalisha vidonge bilioni 1.0, capsules milioni 175, dawa za maji (syrups/suspensions) chupa milioni 15 na dawa ya kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI (ARVs) vidonge milioni 200 kwa uzalishaji wa masaa nane (single shift) kwa mwaka. Mradi utawekeza Shilingi bilioni 70 na kutoa ajira 210 za moja kwa moja. Aidha, mradi utaongeza uzalishaji hadi kufikia shift tatu baadae.

70. Mheshimiwa Spika, Miradi mingine ni pamoja na mradi wa kutengeneza sindano (syringes) milioni 80 kwa mwaka na kutoa ajira 150 za moja kwa moja unaotekelizwa na Kampuni ya *El-Dawlia Ltd* ya Misri katika Eneo la Viwanda la TAMCO. Mradi wa *Pharmaceutical Park* utakaotengeneza *Intravenous (IV) Fluids* chupa 10,000 kwa mwaka utajengwa katika Eneo la Viwanda TAMCO kwa mtaji wa Shilingi milioni 102.732 na kutoa ajira 80. Pia, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PSPF kwa kushirikiana na mwekezaji, Kampuni

ya *Pharmaceutical Investment Ltd* (PIL) wanakamilisha taratibu za kufufua Kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd* (TPI) cha kutengeneza dawa za binadamu na za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI. Miradi hiyo ikikamilika itapunguza kwa kiasi kikubwa uagizaji wa dawa kutoka nje.

(xiv) Viwanda vya Sabuni

71. *Mheshimiwa Spika*, Kiwanda cha *KEDS Tanzania Ltd* cha kuzalisha sabuni ya unga kinajengwa katika Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha. Kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka kitawekeza Dola za Kimarekani milioni 11.5 sawa na Shilingi bilioni 25.3. Aidha, kiwanda hicho kitakapokamilika kitatoa ajira za moja kwa moja 700 na 1,500 zisizo za moja kwa moja. Ujenzi wa kiwanda ulianza mwezi Februari, 2017 na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2017.

(xv) Viwanda vya Kutengeneza Sigara

72. *Mheshimiwa Spika*, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa na kiwanda kimoja cha kutengeneza sigara cha *Tanzania Cigarette Co. Ltd (TCC)*. Kiwanda hicho kimekuwa kikitumia tumbaku inayozalishwa na kusindikwa nchini na nydingine imekuwa ikiuzwa nje ya nchi baada ya kusindikwa. Tumbaku inayouzwa nje huwa imeongezwa thamani kiasi kidogo na sehemu kubwa huongezwa thamani huko inakouzw. Hivyo, uuzaji huo hufanya ajira ambazo zingekuwa za Watanzania kutengenezwa inakouzw tumbaku hiyo. Kufuatia juhudhi za kuvutia uwekezaji zinazofanyika nchini, Kiwanda cha *Philip Morris Tanzania Ltd* ambacho ni Kampuni Mshirika (affiliate company) ya Kampuni ya *Philip Morris International (PMI)* inajenga kiwanda cha kutengeneza sigara za aina mbalimbali katika eneo la Kingolwira, Morogoro. Kiwanda hicho kitawekeza Shilingi bilioni 61.7 na kusindika tani 500 za tumbaku kwa mwaka kwa kuanzia na kutoa ajira za moja kwa moja 100 na zisizo za moja kwa moja 2,000. Uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2017 ambapo sigara zitakazozalishwa zitauzwa katika soko la ndani na nje.

(xvi) Viwanda Vinginevyo

73. Mheshimiwa Spika, mbali ya makundi ya viwanda yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa 2016/2017 tumepata mafanikio makubwa katika kuanzisha viwanda vidogo na viwanda vya kati. Viwanda vya kundi hili vimeanzishwa na wajasiriamali wanaosindika chakula, mafuta ya kula, viungo, asali na mvinyo. Kundi hilo linahusisha pia viwanda vya kusaga nafaka, useketaji wa nguo, ushonaji, useremala, uchomeaji vyuma, utengenezaji samani na utengenezaji wa mashine ndogondogo kwa kutaja baadhi. Faida ya viwanda hivyo ikilinganishwa na makundi ya viwanda vilivyotajwa hapo juu ni kuwa vimesambaa nchi nzima.

e) Viwanda Vilivyobinafsishwa Visivyofanya kazi

74. Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Wizara, ni kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya kazi. Jukumu hilo tunalitekeleza kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Mikoa. Katika mwaka 2016/2017, ufuatiliaji ulifanyika ambapo jumla ya viwanda 30 vilifanyiwa ufuatiliaji na Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kati ya hivyo, viwanda 18 vinafanya kazi vizuri, vitatu (3) vinafanyakazi kwa kusuasua na tisa (9) vimefungwa. Ufuatiliaji huo unafanya jumla ya viwanda vilivyofuutiliwa katika kipindi cha 2015/2016 na 2016/2017 kuwa 110. Baadhi ya viwanda vilivyofungwa wakati wa ufuatiliaji wa mwaka 2015/2016 vilitembelewa tena mwaka 2016/2017 ili kujua maendeleo ya viwanda hivyo na hatua zilizochukuliwa na wamiliki baada ya kupata maelekezo ya Serikali (**Jedwali Na.10a**).

75. Mheshimiwa Spika, juhudii mbalimbali zimefanyika kushawishiwamiliikiwaviwandavilivyofungwailiwavifufue. Matokeo ya juhudii hizo ni pamoja na majadiliano ya kukifufua Kiwanda cha *Morogoro Canvas Mills Ltd* (MCM) ambayo yamefikia hatua nzuri. Kiwanda cha MOPROCO kilichoko Morogoro kimekarabatiwa ikiwa ni pamoja na kufungwa mitambo yenye teknolojia mpya yenye uwezo wa kusindika mbegu za mafuta na pia kusindika mashudu baada ya kukamuliwa na wakamuaji wadogo. Uzalishaji unatarajiwa

kuanza mwezi Juni, 2017. Kiwanda cha Korosho Nachingwea kiliingia Makubaliano ya Awali (MoU) na Kampuni ya *Sunshine Industry* ya China mwezi Machi, 2017 ya kufufua Kiwanda hicho kwa utaratibu wa Kujenga, Kumiliki, Kuendesha na Kuhamisha (*Build, Own, Operate and Transfer-BOOT*). Usimikaji mitambo unaendelea na uzalishaji unatarajija kuanza mwezi Septemba, 2017. Kampuni hiyo pia ilitumia utaratibu huo kufufua Kiwanda cha Korosho cha Mtama ambacho sasa kinafanya kazi vizuri. Kwa viwanda vilivyofanyiwa ufuatiliaji mwaka 2015/2016 na kubainika vimefungwa, uchambuzi wa kina wa Mikataba ya Mauzo ulifanyika chini ya usimamizi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuwezesha hatua stahiki kuchukuliwa. Msajili wa Hazina alikwishatoa kusudio la kutwaa viwanda vinane (8) kutokana na wamiliki wa viwanda hivyo kubainika wamevunja Mikataba ya Mauzo. Kufuatia kusudio hilo, Kiwanda cha Chai cha Mponde kilitwaliwa tarehe 26 Januari 2016 na juhudzi za kumpata mwekezaji wa kukifufua na kukiendeleza zinaendelea. Pia, Kiwanda cha Nyama cha Shinyanga kilichobinafsishwa kwa Kampuni ya *Triple S*, ikashindwa kukifufua, kilitwaliwa tarehe 15 Machi, 2017. Juhudi za kumpata mwekezaji wa kukifufua zinaendelea.

76. *Mheshimiwa Spika*, utwaaji na uendelezaji wa viwanda vilivyobinafsishwa unakabiliwa na changamoto kutokana na madeni makubwa ya mabenki kufuatia mikopo inayochukuliwa na mwekezaji pindi anapokabidhiwa kiwanda. Uchukuaji wa mikopo huenda sambamba na Hati Miliki ya kiwanda kushikiliwa na benki iliyotoa mkopo na hivyo kuwa vigumu mwekezaji anayepatikana kukabidhiwa mali husika bila Hati Miliki. Pia, viwanda hivyo vinakabiliwa na migogoro inayozuia uendelezaji wa kiwanda baada ya kutwaliwa. Hizo ni baadhi ya changamoto zinazokabili ufufuaji wa Kiwanda cha Chai Mponde. Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutatua changamoto husika ili kuwezesha Kiwanda cha Mponde kuanza uzalishaji.

77. *Mheshimiwa Spika*, kwa kupitia Msajili wa Hazina, TIRDO imefanya ukaguzi wa kitaalam (technical audit) wa viwanda vilivyobinafsishwa na kusimama uzalishaji, vikiwemo Kiwanda cha Chai Mponde na Kiwanda cha Ngozi Mwanza. Uainishaji huo

umesaidia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika kutoa maamuzi ya ufujuaji wa baadhi ya viwanda hivyo. Aidha, TIRDO imekwishatoa ushauri wa kitalaam kwa mifuko hiyo ya jamii katika uanzishwaji wa viwanda vya ngozi, dawa na usindikaji wa chakula.

f) Mazingira na Viwanda

78. *Mheshimiwa Spika*, Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (*Sustainable Industrial Development Policy-SIDP*), 1996-2020 inatilia mkazo juu ya uzalishaji wenyе tija unaozingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Tathmini ya utekelezaji wa Sera hiyo sambamba na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (*Environmental Management Act-EMA Act*) 2004 na Kanuni zake, unafanywa kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais; Mazingira, Baraza la Taifa la Mazingira (*NEMC*) na Mamlaka ya Usalama Mahali pa Kazi (OSHA). Tathmini hiyo inahusisha athari za miradi (*Environmental Impact Assessment-EIA*) na uzalishaji viwandani (*Environmental Audit-EA*) kwa mazingira. Tathmini ya EIA hufanya kabla ya mradi kuanza ujenzi ili kuhakikisha kuwa miradi ya uzalishaji inaanizishwa kwa misingi ya Sera na Sheria husika na viwanda kubainisha kama vinazalisha kwa kuzingatia matakwa ya uhifadhi na utunzaji mazingira kwa mujibu wa Sera na Sheria hizo. Kwa mwaka 2016/2017; jumla ya miradi 120 ilijisajili kufanya EIA ambapo 38 ilipata Vyeti vya EIA. Aidha, viwanda 59 vilijisajili kufanya EA na 30 vilifanikiwa kupata Vyeti vya EA.

g) Kujenga Kongano za Viwanda (Industrial Clusters)

79. *Mheshimiwa Spika*, uzalishaji katika makongano husaidia sana wazalishaji wadogo kushirikiana huduma na vifaa ambavyo hawana uwezo wa kuvinunua ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kuboresha uzalishaji, upatikanaji wa malighafi, masoko na ushauri. Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, juhudhi mbalimbali zilifanyika za kuanzisha makongano ya uzalishaji yafuatayo:

- (i) Kongano la Mafuta ya Alizeti katika eneo la Chamwino Dodoma;

- (ii) Kongano la Useketaji Nguo kwa kutumia mashine za mikono (handlooms) Tabora, Arusha na Dar es Salaam; na
- (iii) Kongano la Ngozi na Bidhaa za Ngozi katika eneo la Viwanda la Zuzu Magharibi, Dodoma.

Kongano hizo zitawezesha wazalishaji wadogo kuongeza uwezo wa uzalishaji, ubora wa bidhaa zitakazozalishwa na ufanisi katika uzalishaji.

h) Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda SADC

80. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilishiriki kikamilifu katika kuandaa Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda kwa Nchi za SADC, 2015-2030. Mpango Kazi wa kutekeleza Mkakati huo ulipitishwa na Wakuu wa Nchi za SADC tarehe 18 Machi, 2017 huko nchini Swaziland. Sekta za kipaumbele ni usindikaji wa mazao ya kilimo, uchenjuaji madini (mineral beneficiation) na dawa za binadamu. Katika kutekeleza Mpango Kazi husika, wafadhili mbalimbali wamejitokeza kusaidia nchi wanachama wa SADC kushiriki kikamilifu katika mnyororo wa kikanda wa uongezaji thamani (*regional value chain*) ili kufikia uchumi wa viwanda na kuongeza kasi ya maendeleo ya wananchi wake. Hivyo, Wizara imepokea ufadhili kutoka Jumuuya ya Ulaya (EU) kupitia Programu ya EDF11 kurejea Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (SIDP), 1996-2020. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa kurejea SIDP yameanza. Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya SADC inaandaa miradi katika Sekta ya Dawa za Binadamu na usindikaji mazao ya kilimo kwa ajili ya kupata ufadhili wa kuitekeleza. Miradi hiyo ikikamilika itawasilishwa Sekretariati ya SADC ili kuwasilishwa kwa wafadhili.

i) Matumizi ya Makaa ya Mawe Viwandani

81. *Mheshimiwa Spika*, nishati ni nyenzo muhimu kwa uzalishaji viwandani na ina mchango mkubwa katika kupunguza gharama za uzalishaji inapopatikana kwa uhakika na kwa bei nafuu. Makaa ya mawe ni moja ya vyanzo vya kutoa nishati kwa viwanda na kwa gharama nafuu ikilinganishwa na vyanzo vingine. Nchi

yetu kwa sasa ina machimbo manne ya makaa ya mawe ambayo ni *TANCOAL Energy Limited* iliyoko Ngaka, Mbinga Mashariki; *Magamba Coal Mine* iliyoko Rukwa; *Kabulo Ridge* iliyoko Kiwiri na *Katewaka Coal Ltd* iliyoko Maganga Matitu, Njombe. Machimbo hayo yanakadiriwa kuwa na uwezo wa kutoa makaa ya mawe tani 2,254,080 kwa mwaka. Uzalishaji wa makaa ya mawe unategemea kwa kiasi kikubwa mahitaji yaliyo tayari kwa matumizi ya viwanda ili kuepusha ukusanyaji mkubwa unaoweza kuleta athari za mlipuko wa moto kutohana na makaa yenye. Kutohana na bei ndogo na ubora wa makaa ya mawe yanayozalishwa nchini, zaidi ya viwanda 15 vimeanza kutumia makaa ya mawe kama chanzo cha nishati na hivyo kuachana na matumizi ya mafuta mazito pamoja na kuni katika kuendesha mitambo yao ya uzalishaji. Matumizi hayo ya kuni yamekuwa kwa kiasi kikubwa yakichangia katika uharibifu wa mazingira nchini. Matumizi ya makaa ya mawe kwa viwanda hivyo yanakadiriwa kuwa tani 1,048,056 kwa mwaka sawa na tani 75,338 kwa mwezi. Aidha, makaa hayo yanauzwa nje ya nchi katika nchi za Kenya, Uganda na Rwanda (**Jedwali Na 10b na 10c**).

j) KAIZEN

82. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) imekuwa ikitekeleza Mradi wa *Strengthening Manufacturing Enterprises through Quality and Productivity Improvement (KAIZEN)*. Mradi huo unalenga kuongeza ubora wa bidhaa, tija na kupunguza gharama za uzalishaji bila gharama kubwa kwa kiwanda. Awamu ya Kwanza ya Mradi ilijielekeza katika kutoa mafunzo ya uelewa wa dhana ya KAIZEN kwa Watanzania na mafunzo ya kutekeleza dhana ya KAIZEN kwa viwanda katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro. Katika awamu hiyo ambayo ilimaliza muda wake mwezi Juni 2016, Watanzania 2,100 walihamasishwa na kupata uelewa wa dhana ya KAIZEN, viwanda 52 vya mfano vilifundishwa na kuanza kutekeleza dhana ya KAIZEN, wakufunzi wa wakufunzi (Master Trainers) 13 walipata mafunzo ya kina ya KAIZEN hapa nchini na Japan ili kuwawezesha kutoa mafunzo kwa wakufunzi (Trainers) na viwandani na *Trainers* wanane walipatia mafunzo ya KAIZEN nchini.

Ili kuhamasisha viwanda vingine kuijunga na dhana ya KAZIEN, mwezi Oktoba, 2016 viwanda vilivyoshinda katika kutekeleza dhana ya KAIZEN vilipewa zawadi pamoja na wakufunzi wa wakufunzi bora. Mkakati wa kutekeleza dhana KAIZEN, 2016-2020 uliandaliwa na kupidishwa. Aidha, maandalizi yanafanyika ya kuanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa KAIZEN mwezi Julai, 2017. Awamu hiyo itaongeza mikoa mitano zaidi ya kufundisha dhana ya KAIZEN viwandani na hivyo kuwa mikoa minane inayotekeliza dhana hiyo. Mikoa mipya ni Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza na Singida.

4.2.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

a) Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

83. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilipanga kuifanyia mapitio Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003 ambapo Wizara imekamilisha hatua ya kutathmini utekekezaji wa sera ambao ni msingi muhimu katika kufanya mapitio ya sera hiyo. Lengo la tathmini hiyo ilikuwa ni kutambua mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa sera hiyo ili ziwe msingi wa mapitio. Jukumu hilo muhimu limefanikiwa kutokana na ushirikiano mzuri na Shirika la Kazi Duniani (ILO), *International Fund for Agriculture Development* (IFAD) na *Financial Sector Deepening Trust* (FSDT).

b) Kuhamasisha Halmashauri Kutenga Maeneo

84. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha utengaji wa maeneo katika Halmashauri zote nchini. Wizara imefuatilia utekelezaji wa utengaji wa maeneo katika mikoa ya Lindi, Morogoro, Singida na Tanga. Katika mikoa wa Lindi Halmashauri zilizotenga maeneo ni za Manispaa ya Lindi, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Kilwa, Ruangwa, Liwale na Nachingwea. Mikoa wa Tanga umetenga maeneo katika Manispaa ya Tanga, Halmashauri za Wilaya za Handeni, Korogwe, Mkinga,

Muheza na Kilindi. Katika Mkoa wa Singida, Halmashauri zilizotenga maeneo ni Manispaa ya Singida, Halmashauri za Wilaya za Iramba, Ikungi na Manyoni. Halmashauri zilizotenga maeneo katika Mkoa wa Morogoro ni Manispaa ya Morogoro na Halmashauri ya Wilaya ya Ifakara. Mikoa mingine ambayo imetenga maeneo ni pamoja na Arusha, Dodoma, Geita, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Njombe na Shinyanga. Pamoja na maeneo tuliyotembelea na kufanya tathmini, mwitikio wa zoezi hilo nchini ni mzuri.

85. *Mheshimiwa Spika*, kwa kutambua mahitaji ya wadau wetu (Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya) tumeandaa Mwongozo juu ya Ujenzi wa Viwanda. Kitabu hicho kinaeleza jinsi ya kuandaas taswira ya Mkoa, Wilaya, Kata mpaka Kijiji kwa kuonesha bayana fursa za kujenga viwanda. Pia, ufanuzi umetolewa jinsi ya kutenga maeneo ya kujenga viwanda kwa kulenga viwanda vidogo sana, viwanda vidogo na vya kati. Kitabu hicho kinabainisha umuhimu na majukumu ya taasisi mbalimbali katika kutoa ushauri juu ya ujenzi wa viwanda ikiwemo na ujenzi wa miundombinu wezeshi na miundombinu saidizi. Ni matumaini yetu kuwa kwa kutumia mwongozo huo mikoa na wilaya zote nchini zitakuwa na uelewa na mwamko sawa katika kujenga uchumi wa viwanda.

c) Utekelezaji wa Mradi wa MUVEI

86. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliendelea kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVEI) kwa kila robo mwaka kwa kutembelea mikoa yote ambako mradi unatekelezwa. Mradi huo umetekelizwa kwa miaka tisa kuanzia mwezi Julai, 2007 hadi mwezi Machi, 2017. Lengo la mradi lilikuwa ni kusaidia katika jitihada za kupunguza umasikini kwa kuendeleza wajasiriamali vijijini kupitia minyororo ya thamani ya mazao yaliyochaguliwa. Mradi huo ulianzhishwa na Wizara na kutekelezwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kupitia kwa wataalam waelekezi. MUVEI ilitekelezwa katika Wilaya 19 za Mikoa 7 ya Iringa, Manyara, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma na Tanga.

87. *Mheshimiwa Spika*, tangu kuanzhishwa mradi huo, huduma zimetolewa kwa familia 105,449 ambazo ni asilimia 92 ya lengo

na umeweza kuzalisha ajira za moja kwa moja 13,757. Mradi umewezesha uanzishaji wa huduma mpya ambazo zimesaidia kuongeza tija kwenye uzalishaji na zinaweza kuigwa na kuendelezwa hata baada ya mradi kukamilika. Huduma zilizoanzishwa ni pamoja na uendeshaji wa mashamba darasa ya mbegu; miradi ya uongezaji thamani mazao; miundombinu 23 ya masoko; huduma ya uuzaji kwa pamoja vikundi 618; uanzishaji wa vikundi 30 vya kuweka na kukopa (SACCOS); utaratibu wa upatikanaji wa taarifa za masoko; na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima 53,503 na kilimo biashara kwa wakulima 48,203.

88. *Mheshimiwa Spika*, huduma zote hizo zimerahisisha shughuli za uzalishaji na kuongeza tija. Kwa mfano uanzishaji wa mashamba ya mbegu bora kwa mazao ya alizeti, maharage na ufuta vimesaidia kuongeza uhakika wa upatikanaji wa mbegu kwa asilimia 68. Mafunzo ya mbinu bora za kilimo pamoja na kilimo biashara vimehamasisha wakulima kuzingatia mambo ya msingi yanayofanya uzalishaji wao kuwa na tija. Asilimia 89 ya wazalishaji washiriki walikiri kuwa uzalishaji na tija vimeongezeka na asilimia 93, kuwa mbinu za kisasa za uzalishaji walizowezeshwa kupata zimewasaidia kuongeza ufanisi na tija.

d) Mfuko wa NEDF

89. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wananchi (National Entrepreneurship Development Fund - NEDF) ulianzishwa mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Madhumuni ya Mfuko huo ni kutoa mikopo kwa wenyewe viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara kwa lengo la kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi yao. Tathmini ya utekelezaji wa Mfuko iliyofanywa inaonesha kuwa bado mahitaji ya huduma kutoka kwenye mfuko ni makubwa kuliko uwezo uliopo. Mfuko tangu ulipoanzishwa mwaka 1994 hadi Machi 2017 umepokea jumla ya maombi 211,977 yenye kuhitaji mikopo ya thamani ya Shilingi 161,589,513,000, lakini umeweza kutoa mikopo kwa maombi

85,130 tu yenye thamani ya Shilingi 61,368,432,000 ambayo ni sawa na asilimia 40 tu ya mahitaji. Kwa kipindi cha miaka 23 ya uhai wake, Mfuko umewezesha kupatikana ajira mpya 172,083 nchini kote. Mikopo hiyo ilitokana na mtaji wa Shilingi 5,051,000,000 uliotolewa na Serikali.

90. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017 jumla ya wajasiriamali 2,593 walipewa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 3.92 na mikopo hiyo iliwezesha kupata ajira 9,424. Katika mikopo iliyotolewa, asilimia 48 ilitolewa kwa wanawake, asilimia 51 ni wanaume na asilimia moja kwa ubia. Aidha, asilimia 33 ya mikopo ilitolewa chini ya NEDF ilitolewa katika miradi iliyo vijijini. Serikali inaendeleza juhudzi za kuukuza mfuko huo ili uwe kitovu cha kukuza viwanda vidogo. Fedha walizokopeshwa wajasiliamali kwa mwaka huu ni kutokana na marejesho ya wakopaji wa awali bila kuhusisha Shilingi bilioni 2.4 zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017.

4.2.3 Sekta ya Biashara

a) Biashara kati ya Nchi na Nchi

91. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na juhudzi ya kutafuta fursa za masoko na uwekezaji baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa. Kwa upande wa nchi na nchi, Wizara imeratibu na kufanya majadiliano mbalimbali ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine. Wizara iliratibu ziara ya kibiashara na ujumbe wa kiserikali kutoka Poland mwezi Julai 2016. Ziara hiyo ilikuwa ni muendelezo wa majadiliano ya kuhimiza wawekezaji kutoka Poland kuwekeza nchini. Moja ya masuala muhimu yaliyojadiliwa katika ziara hiyo ni kuharakisha uanzishwaji wa Kiwanda cha Uunganishaji wa Matrekta nchini (URSUS) na matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kuhifadhi mazao ya kilimo.

92. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China zimekubaliana kushirikiana kutekeleza Mpango wa *FOCAC Johannesburg Action Plan 2016-2018* ambao unalenga kukuza

uhusiano wa Afrika na China katika eneo la biashara, uwekezaji na uchumi. Katika kutekeleza makubaliano hayo, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Ubalozi wa China nchini imeandaa Mpango Kazi wa Kutekeleza Maazimio ya FOCAC ambayo yamewasilishwa Serikali ya China kwa ajili ya kupata ufadhili. Mpango Kazi huo umejumuisha miradi ya viwanda, nishati, miundombinu, fedha, kilimo, elimu na TEHAMA.

93. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu ziara ya ujumbe wa kiserikali kutoka Ukraine. Hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza kwa viongozi wa nchi hiyo kufanya ziara ya kibiashara nchini. Ujumbe huo ulifanya mazungumzo na Wizara na kupata fursa ya kutembelea Maonesho ya Viwanda kwenye viwanja vya SabaSaba, Dar es Salaam na kukutana na wazalishaji hususan wajasiriamali wadogo na kujiona bidhaa za viwandani. Wizara iliwaomba wawekezaji kutoka Ukraine kuhamasisha wawekezaji nchini kwao ili Maonesho ya SabaSaba yanayofuata waje kuonesha viwanda au mashine za kuzalisha bidhaa kama walizoziona kwenye maonesho hayo.

94. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilianda ziara ya kibiashara kati ya Tanzania na Ujerumanu nchini. Katika ziara hiyo, Wizara iliweza kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo nchini na kuvutia wawekezaji kutoka Ujerumanu kuja kuwekeza Tanzania. Maeneo ambayo Ujerumanu wameonesha nia ya uwekezaji ni katika uongezaji thamani wa bidhaa za kilimo na biashara ya bidhaa za kilimo (agro-processing and agri-business). Wizara pia ilianda na kuratibu ziara ya ujumbe wa kibiashara kutoka Austria. Ziara hiyo ilisaidia wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Austria kuona fursa za uwekezaji nchini na kukutana na wafanyabiashara wa Kitanzania kuititia Maonesho ya SabaSaba ambapo walipata fursa ya kubadilishana uzoefu, kuona bidhaa za Tanzania na kuahidi kuzichangamkia. Baadhi ya fursa zilizovutia ugeni huo ni sekta za gesi na mafuta, kilimo na ujenzi wa viwanda. Wizara inafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa ziara hizo zinazaa matunda. Vilevile, Wizara imefanya majadiliano na mabalozi wa nchi mbalimbali nchini zikiwemo Morocco, India, Sweden, Italy, Uingereza, Denmark, Ubelgiji, Sweden, Belarus, Czech, Cuba na Japan.

95. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeshiriki katika mikutano ya Tume ya Pamoja (Joint Permanent Commission) kati ya Tanzania na Kenya, Malawi, Rwanda, Uganda na Zambia. Lengo la mikutano hiyo ya pamoja ni kujadili na kukubaliana namna ya kurahisisha biashara, kukuza uwekezaji na kuimarisha diplomasia ya uchumi kati ya Tanzania na nchi hizo. Katika kurahisisha biashara mipakani hususan kwa wafanyabiashara wadogo, Tanzania na Malawi zimekubaliana kuanzisha Kituo cha Pamoja cha Mpakani (OSBP) na kuingia makubaliano ya kuanzisha Mkataba wa Mfumo wa Kurahisisha Biashara (*Simplified Trade Regime -STR*). Makubaliano ya kuanzisha huduma kama hiyo kati ya Tanzania na Zambia yalisainiwa tarehe 27 Januari, 2017. Aidha, katika kuimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na Uturuki, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Tume ya Pamoja ya Biashara na Uchumi uliofanyika mjini Ankara, Uturuki mwezi Januari 2017. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa makubaliano yaliyofanyika Dar es Salaam, Tanzania mwezi Novemba, 2012. Katika mkutano huo, nchi hizo mbili zilikubalina kushirikiana zaidi katika masuala yanayohusu biashara na uwekezaji.

96. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeshiriki katika makongamano mbalimbali kama sehemu ya kuendeleza mahusiano ya kibashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi nyingine,. Kupitia Kongamano la Biashara na Uwekezaji la China na Afrika (*Chinese Business and Investment Forum*) liliofanyika mwezi Septemba 2016, nchini China, mamlaka za uwekezaji ziliingia makubaliano ya ushirikiano kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji na mauzo ya bidhaa zao. Katika makongamano hayo, Wizara iliweza kutumia fursa hiyo kuhimiza upande wa China kuharakisha kukamilisha utiaji saini wa mkataba wa biashara baina ya Tanzania na China. Vilevile, Wizara iliratibu Kongamano la Biashara na Mkutano wa Pamoja kati ya Tanzania na Rwanda iliyofanyika mwezi Desemba 2016 mjini Dar es Salaam. Suala la msingi lililojadiliwa ni kuhamasisha biashara baina ya nchi hizo hususan kuondoa vikwazo vyta biashara visivyokuwa vya kiushuru ambapo Rwanda iliridhia kuondoa vikwazo hivyo kwenye mchele kutoka Tanzania. Hivi sasa wafanyabiashara wa mchele

kutoka Tanzania wanauzu mchele nchini Rwanda bila kutozwa kodi ya ushuru wa forodha. Aidha, Wizara iliratibu Kongamano la Kibiashara kati ya Tanzania na Ubelgiji lililofanyika mwezi Novemba, 2016. Kongamano hilo lilisaidia kupanua fursa zaidi za biashara na uwekezaji kwa wafanyabiashara wa nchi hizo mbili. Maeneo yaliyowavutia wawekezaji kutoka Ubelgiji ni masuala ya uzalishaji viwandani, miundombinu, dawa za binadamu, usafirishaji na ujenzi.

97. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) iliratibu kongamano la biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Morocco lililofanyika tarehe 22 Oktoba, 2016. Katika Kongamano hilo jumla ya mikataba 21 ya ushirikiano ilisainiwa. Mikataba iliyosainiwa ilihusisha masuala yafuatayo; kuanzisha ushirikiano baina ya Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) na kile cha Morocco (The Moroccan Center for Export Promotion - Maroc Export), sekta za nishati na madini, gesi, kilimo, anga, fedha, utalii na uvuvi ambapo Morocco imeonesha nia ya kujenga kiwanda kikubwa cha usindikaji samaki hapa nchini. Aidha, kupitia kongamano hilo, Serikali ya Morocco imeonesha nia ya kuanzisha safari za ndege za moja kwa moja kati ya Rabat na Dar es Salaam. Wizara pia ilishiriki katika Kongamano la Biashara kati ya Tanzania na Comoro lililofanyika Zanzibar mwezi Novemba 2016. Kongamano hilo lilikutanisha takriban wafanyabiashara 50 kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Comoro. Kupitia kongamano hilo, nchi zote mbili zilikubaliana kuruhusu Meli ya M/V Mapinduzi, inayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inayobeba tani 600 za mzigo kuanza safari za kwenda Comoro.

98. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Biashara na Uchumi kati ya Uturuki na Afrika lililofanyika mjini Istanbul nchini Uturuki mwezi Novemba, 2016 na ilinadi fursa za biashara na uwekezaji na kuhamasisha washiriki kuja kuwekeza nchini. Vilevile katika kuhakikisha mihadi iliyowekwa wakati wa kongamano hilo inatekelezwa, Wizara imeweza kuratibu ziara ya Kampuni ya *Agir Haddecilik* ya nchini Uturuki kuja nchini kuangalia fursa za uwekezaji. Kampuni hiyo ni moja ya kampuni kubwa nchini humo inayojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za chuma. Aidha,

kupitia ziara yao nchini, kampuni hiyo imeonesha nia ya kuwekeza katika Sekta ya Chuma.

99. *Mheshimiwa Spika*, Wizara iliratibu Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kibiashara (2nd Joint Commercial Committee-JCC) kati ya Tanzania na Uturuki uliofanyika mwezi Januari, 2017 nchini Uturuki. Lengo la mkutano huo lilikuwa ni kufuatilia utekelezaji wa makubaliano ya mkutano wa kwanza wa JCC uliofanyika Dar es Salaam mwezi Novemba 2012 pamoja na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano ili kukuza na kuendeleza biashara na uwekezaji. Mkutano huo pia ulijadili na kukubaliana kuhusu ziara ya kiserikali ya Mheshimiwa Rais wa Uturuki nchini Tanzania. Aidha, ziara ya Mheshimiwa Rais wa Uturuki ilifanyika mwezi Januari 2017 ambapo mikataba 9 ilisainiwa. Mikataba hiyo ilihuisha sekta za viwanda, afya, elimu, ulinzi na ujenzi. Ziara hiyo pia ilihuisha kongamano la biashara ambapo pande zote mbili ziliendelea kunadi fursa za biashara na uwekezaji.

100. *Mheshimiwa Spika*, ili kufaidika na fursa ya AGOA, Wizara kwa kushirikiana *East African Trade and Investment Hub* (EATIH) na wadau wengine nchini imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa AGOA. Mkakati huo unalenga kuhamasisha wadau nchini kuchangamkia fursa hiyo kutokana na nyongeza ya miaka 10 ya fursa ya AGOA ambayo sasa itafikia ukomo mwaka 2025. Mkakati huo umejikita kwenye sekta nne za kipaumbele ambazo ni nguo na mavazi, bidhaa za kazi za mikono, ngozi na bidhaa zake na usindikaji wa bidhaa za kilimo. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na EATIH kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati huo wa AGOA.

b) Biashara ya Kikanda

101. *Mheshimiwa Spika*, katika majadiliano ya biashara ya kikanda, Wizara imetetea msimamo wa Tanzania wa kutosaini Mkataba wa EPA na kuendelea kushawishi nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuunga mkono msimamo huo wa Tanzania. Wizara ilifanikiwa kutekeleza suala hilo kupitia Mkutano wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na

Uwekezaji (SCTIFI) uliofanyika mwezi Januari hadi Februari, 2017 jijini Arusha. Kutokana na msimamo huo, licha ya Kenya na Rwanda kutia saini, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeshindwa kusaini Mkataba huo hali inayotoa fursa kwa Tanzania na Jumuiya hiyo kutafakari kwa mapana zaidi kuhusu Mkataba wa EPA.

102. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeshiriki katika zoezi linaloeendelea la kufanya mapitio ya Ushuru wa Pamoja wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common External Tariff- CET). Zoezi hilo ni sehemu ya utekelezaji wa Itifaki ya Ushuru wa Forodha wa Pamoja wa EAC na limezingatia pia maelekezo ya Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki la kutaka kufanya mapitio ya CET kila baada ya miaka mitano. Lengo la mapitio hayo ni kushughulikia changamoto za utekelezaji wa CET kuweza kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na biashara na pia yana akisi maendeleo yanayojiteze katika utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa Jumuiya. Aidha, Wizara, kwa kushirikiana na wadau, tayari imeunda kikosi kazi cha kitaifa kitakachoshiriki katika zoezi hilo kitaifa na kikanda ambacho kitazingatia mapendekezo yenye maslahi mapana ya Taifa.

103. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeshiriki katika kuitisha Mkakati wa Viwanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mkakati huo (2015-2063). Wizara ilifanikiwa kutekeleza jukumu hilo kwa kushiriki kikamilifu kuitia Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika mwezi Machi, 2017 mjini Lozitha, Swaziland. Mkakati huo unaendana na dhima ya Serikali ya Awamu ya Tano ya ujenzi wa uchumi wa viwanda hasa ikizingatiwa kuwa Mkakati huo umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo ni: uendelezaji viwanda; kukuza ushindani; na kuhimiza mtangamano wa kikanda.

104. *Mheshimiwa Spika*, kuitia mkutano huo, Tanzania imefanikiwa kupata upendeleo maalum (dispensation) wa kutoza ushuru sukari inayotumika kwa matumizi ya nyumbani kutoka nchi za SADC. Katika upendeleo huo, Tanzania itaendelea kutoza

ushuru wa asilimia 25 kwa sukari ya aina hiyo kutoka nchi za SADC kwa kipindi cha mwaka mmoja. Wizara pia imewasilisha ombi la kupatiwa upendeleo kama huo kwa kipindi cha miaka mitatu kwa karatasi za vifungashio. Upendeleo huo unalenga kutoa fursa kwa wazalishaji wa bidhaa hizo nchini kujenga uwezo zaidi ili kukabiliana na ushindani wa bidhaa kama hizo kutoka SADC.

105. *Mhesimiwa Spika*, Wizara ilishiriki katika kuandaa na kuwasilisha Waraka Serikalini kuhusu kuomba Serikali iridhie utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma kwa nchi za SADC. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliratibu maandalizi na mawasilisho ya Waraka husika. Ni matarajio yetu kuwa utekelezaji wa Itifaki hiyo utafungua fursa zaidi kwa watoa huduma katika sekta mbalimbali nchini kuweza kutoa huduma zao bila vikwazo vyta kibiashara katika nchi wanachama wa SADC. Aidha, Itifaki hiyo pia inatoa fursa kwa kila nchi mwanachama kuruhusu huduma na watoa huduma kutoka nchi nyininge wanachama kutoa huduma kwenye maeneo watakayopendekeza. Hali hiyo itaongeza ushindani katika sekta za huduma zitakazofunguliwa na hivyo kuongeza tija na urahisi kwa watumiaji wa huduma hizo.

106. *Mhesimiwa Spika*, Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu-Tripartite Free Trade Area-TFTA kwa jumuiya za COMESA-EAC- SADC. Majadiliano hayo yalikamilika mwezi Aprili, 2015 na hatimaye wakuu wa nchi na serikali wa nchi zinazounda Jumuiya hizo walihitimisha majadiliano ya awamu ya kwanza na kusaini Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu mwezi Juni 2015. Majadiliano katika baadhi ya maeneo ambayo hayakuwa yamekamilika wakati wa uti waji saini, yamekamilika mwezi Novemba, 2016. Faida kubwa inayotarajiwa kupatikana katika utekelezaji wa Mkataba huo ni pamoja na kuongezeka kwa fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania kwenye Soko la TFTA kutokana na kupunguzwa kwa vikwazo vyta kufanya biashara pamoja na kuwa na vigezo vyta uasilia wa bidhaa vilivyo rahisishwa vinavyowezesha bidhaa zinazozalishwa ndani ya Jumuiya hizo kufikia vigezo hivyo na kutambulika katika Soko la TFTA. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau tayari inaendelea

na zoezi la kukusanya maoni ya wadau kwa lengo la kuandaa Waraka kuomba Serikali kuridhia Mkataba wa uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara la Utatu- *TFTA*.

107. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeshiriki na kuweza kutetea kikamilifu misimamo ya Taifa katika majadiliano yanayoendelea yanayohusu uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Barani Afrika (Continental Free Trade Area-CFTA). Katika mkutano uliofanyika mjini Addis Ababa, Ethiopia mwezi Machi, 2017, Wizara ilichangia katika mjadala na kupitisha rasimu ya Taratibu za Majadiliano ya CFTA (Draft Modalities for CFTA) kwenye maeneo ya Biashara ya Bidhaa na Huduma. Maeneo mahsusini yanayojadiliwa na ambayo Wizara inayasimamia ni kuhusu masuala ya Usalama wa Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea (SPS); Vikwazo Visivyo vya Kiushuru vya Kibiashara (NTBs) na Vikwazo vya Kiufundi vya Kibiashara (TBT); Uasili wa Bidhaa (RoO); Biashara ya Huduma; masuala ya Sheria; *Trade Remedies*; na Taratibu za Forodha na Uvezeshaji wa Biashara. Wizara imejizatiti katika kuhakikisha kuwa maslahi ya Tanzania yanazingatiwa katika majadiliano hayo.

c) Biashara ya Kimataifa

108. *Mheshimiwa Spika*, katika kupanua fursa za masoko na biashara kupitia majadiliano ya biashara ya kimataifa, Wizara imeshiriki katika kuandaa mwongozo wa miaka minne ijayo wa Shirika la UNCTAD. Mpango huo ulipitishwa katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Mawaziri wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD XIV) uliofanyika mjini Nairobi, Kenya mwezi Julai, 2016. Kwa kuzingatia mpango huo, UNCTAD itajikita katika kutafiti, kuchangia pamoja na kutatua changamoto za kibashara na maendeleo hususan kwa nchi maskini na zinazoendelea. Hiyo ni pamoja na kukuza uchumi shirikishi na endelevu kupitia biashara na kuchangia utekelezaji na ufuataliaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs, 2030). Wizara ilitumia fursa ya mkutano huo kufanya majidiliano ya kuhamasisha biashara na uwekezaji nchini ambapo ujumbe wa Tanzania uliweza kukutana na kufanya mazungumzo

na ujumbe kutoka Austria, Cuba, Hungary, Jamaica, Kenya, Poland, Sudani ya Kusini, Uganda, Venezuela, Umoja wa Ulaya; na mashirika ya UNCTAD, WTO, TRAPCA na Sekretariati ya nchi za ACP.

109. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeanzisha Kituo cha Taarifa za Biashara za Kimataifa (*WTO Reference Center*) ambacho kipo Wizarani. Kituo hicho kitawezesha taasisi za Serikali na binafsi kupata nyaraka na taarifa mbalimbali za biashara ambazo zitasaidia kukuza Sekta ya Biashara nchini. Wizara pia imewasilisha taarifa za viwango vipyta 44 vya ubora (*notifications of technical Standards*) kwenye Shirika la Biashara la Dunia kwa bidhaa za mbolea, matunda, vyakula vya wanyama na vileo. Tayari Wizara imetua ufanuzi na kutetea *notifications* kwa viwango vilivyowasilishwa kuitia Mkutano wa Kamati ya Vikwazo vya Kiufundi vya Shirika la Biashara Duniani (*WTO TBT Committee*) uliofanyika Uswisi, Geneva mwezi Machi, 2017.

110. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imewajengea uwezo maafisa watano kuitia mafunzo ya mfumo wa kieletroniki (*ePing notification alert system*) yaliyofanyika Desemba, 2016 Kampala – Uganda, ili waweze kushiriki kikamilifu katika kutekeleza mikataba ya WTO hususan kwenye eneo la utoaji na upokeaji wa taarifa za kibashara katika masuala ya Vikwazo vya Kiufundi na Kibashara (TBT); na Usalama wa Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea (SPS).

111. *Mheshimiwa Spika*, ili kusogea karibu huduma ya kuwajengea uwezo wadau kwenye masuala ya kibashara, Wizara imeratibu zoezi la upatikanaji wa kozi maalum ya majadiliano ya biashara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Chini ya ufadhilli wa WTO, wanafunzi kutoka nchi zote wanachama wanaoongea kiingereza watapata mafunzo katika chuo hicho. Hiyo ni fursa muhimu ya kuwapatia mafunzo wataalamu wetu, lakini pia kutokana na wingi wa washiriki kutoka sehemu mbalimbali duniani, chuo chetu kikongwe kitapata fursa ya kutangazwa zaidi kote duniani. Mafunzo hayo yanayotegemewa kuanza mwaka ujao wa fedha yataendelea kwa miaka mitatu mfululizo.

112. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) wa Uwezeshaji Biashara (WTO Trade Facilitation Agreement). Mkataba huo, unalenga kupunguza gharama za ufanyaji biashara kwa kuhakikisha kuwa miundombinu muhimu inakuwepo na inaratibiwa kwa pamoja ili kupunguza muingiliano wa majukumu. Katika maandalizi hayo, Wizara imeunda Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (National Trade Facilitation Committee) mwezi Agosti, 2016 kwa kuzingatia matakwa ya Mkataba huo ili kusimamia utekelezaji wa Mkataba huo. Aidha, Wizara imewasilisha maombi ya kupata ridhaa ya Tanzania kuridhia Mkataba wa Urahisishaji Biashara.

113. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha Kamati za Kitaifa ya Kuondoa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Ushuru (Non Tariff Barriers-NTBs), Vigezo vya Biashara vya Afya ya Mimea na Wanyama (Sanitary and Phytosanitary Measures- SPS), Vigezo vya Biashara vya Kiufundi (Technical Barriers to Trade-TBT) na Uwezeshaji Biashara (Trade Facillitation-TF), Wizara imeendelea kuratibu mikutano ya kamati hizo nchini na kushiriki mikutano ya kamati za kikanda kwa lengo la kujadili na kutatua changamoto katika maeneo hayo kwa lengo la kurahisisha biashara.

114. *Mheshimiwa Spika*, baadhi ya mafanikio ya juhudii hizo ni kuondolewa kwa NTBs nane (8) ambazo ni tozo ya Dola za Kimarekani 300 kwa malori ya Rwanda yanayobeba chumvi kuititia njia ya Mbuga ya Saadani, tozo ya asilimia 1.5 ya maendeleo ya reli, ucheleweshaji wa kutoa mizigo bandarini kwa kutumia siku 10, idadi ya mizani kutoka 17 hadi kufikia mizani 3 kwa ushoroba wa kati (central corridor), tofauti ya masaa ya kazi katika mipaka ya Rusumo na Kabanga kwa kuanzisha mfumo wa OSBP; tozo kwa bidhaa za dawa kutoka Kenya, tozo ya asilimia 35 kwenye mafuta ya kula kutoka Kenya na maafisa wa TRA wanaofanya kazi Kenya chini ya mfumo wa himaya moja wa forodha (single customs territory), na kumaliza muda wa kazi mapema (kufunga ofisi saa 9 alasiri). Uondoaji wa NTBs hizo umechangia kwa kiasi kikubwa katika kurahisisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya

ya Afrika Mashariki. Kupitia Kamati ya Kitaifa ya NTBs, Wizara imeshirikiana na *Tanzania Gender Networking Programme (TGNP)* na TMEA kuendesha mafunzo kwa wafanyabiashara wanawake 34 wanachama wa Chama cha Wanawake wa Tanzania Wafanyabiashara Mipakani (WATABAM) wanaofanya biashara katika mipaka ya Holili, Mutukula na Namanga. Mafunzo hayo yalihu masuala ya vikwazo vya biashara visivyo kuwa vya kiushuru na fursa za masoko zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla.

115. *Mheshimiwa Spika*, katika kupambana na bidhaa zinazotoka nje ya nchi na kuuzwa nchini chini ya bei halisi ya sokoni duniani, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeratibu zoezi la kuandika upya Sheria ya *Anti-dumping and Countervailing Measures*. Aidha, Wizara imekwishaandaa rasimu ya Sheria na Waraka wa kupata maamuzi ya Serikali ili iridhie kuandika upya sheria hiyo. Sheria hiyo inalenga kuzuia uingizwaji wa bidhaa nchini zinazouzwa nchini chini ya bei halisi ya bidhaa hizo sokoni (Dumping price) ili kuhakikisha kunakuwepo na ushindani wa haki kwenye soko. Vilevile, sheria hiyo itasaidia kulinda viwanda na wafanyabiashara nchini kwa kuweka utaratibu wa kisheria wa kujilinda na bidhaa zinaouzwa nchini chini ya bei halali ya soko kwa kipindi husika. Kutokana na umuhimu wake, tunatarajia sheria hiyo ianze kutumika rasmi katika mwaka 2017/2018.

4.2.4 Sekta ya Masoko

116. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Masoko ina jukumu la kuvipatia viwanda malighafi, kuvilinda, kuuza bidhaa za viwanda, kumlinda mlaji na kuhakikisha ubora na ushindani ulio haki. Katika kujenga uchumi wa viwanda, Wizara imesimamia majukumu chini ya sekta hiyo kwa lengo la kuongeza tija katika sekta zote husika.

a) Udhibiti wa Ubora na Viwango vya Bidhaa

117. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia mashirika yake ya TBS, WMA na FCC ina jukumu la kuhakikisha kuwa bidhaa na

huduma zinazozalishwa na kutolewa kwa mlaji zinakidhi viwango. Kwa mwaka 2016/2017, taasisi ya TBS na FCC kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali hususan TRA, Jeshi la Polisi na TFDA imeendelea kudhibiti ubora wa bidhaa ili kulinda afya za watumiaji, mazingira pamoja na kuleta ushindani wa haki katika biashara. Pamoja na kusimamia ubora wa bidhaa za viwanda vyetu, kipaumbele kimewekwa katika kuzuia bidhaa zisizo na ubora na bidhaa bandia kuingia katika soko. Umuhimu wa kuzuia bidhaa unatokana na ukweli kuwa bidhaa hizo huuzwa kwa bei ya chini na hivyo kuleta ushindani usio wa haki kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda kwa kuzingatia viwango. Hivyo, udhibiti wa bidhaa bandia na zisizo na ubora ni hatua muhimu katika kulinda viwanda vya ndani.

118. *Mheshimiwa Spika*, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea na ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi kabla ya kuletwa nchini, kukagua bidhaa bandarini na mipakani na bidhaa zilizopo sokoni. Ili kuimarisha mifumo ya udhibiti ubora wa bidhaa nchini, Wizara inaandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Quality Policy) pamoja na Mkakati wake ambapo andiko la kitaalamu (Concept Note) limeandaliwa na Taasisi ya *Trade Mark East Africa* (TMEA) imeridhia kugharamia maandalizi yake. Pamoja na maandalizi ya Sera, Wizara imeanza kufanya mapitio ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya Mwaka 2009 ili kuongeza kasi ya maendeleo ya viwanda nchini. Maoni ya wadau yamekusanywa na uchambuzi unaendelea ili kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo katika ngazi inayofuata. Vilevile, Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Ushindani na kuyawasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa hatua zaidi.

119. *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia imeendelea kufanikisha juhudzi za kulinda haki za wabunifu na rasimu ya Sera ya Miliki Bunifu pamoja na mkakati wake imeandaliwa na kujadiliwa ngazi ya awali ya maamuzi Serikalini. Wizara inaboresha rasimu hiyo ili iwasilishwe kwa maamuzi ya mwisho. Aidha, Wizara imeandaa marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya mwaka 1999 ili kuimarisha ulinzi wa haki miliki za wadau mbalimbali.

b) Bei ya Bidhaa, Mazao Makuu ya Chakula na Mifugo

(i) Bei za Mazao Makuu ya Chakula

120. *Mheshimiwa Spika*, jukumu la Wizara yetu ni pamoja na kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kutoa taarifa ya bei za mazao makuu ya chakula, mifugo na baadhi ya bidhaa muhimu nchini kwa wadau. Katika msimu wa 2016/2017, bei ya mazao makuu ya chakula kama vile mahindi, maharage, mchele, ngano, uwele, ulezi na mtama zimeongezeka kwa viwango tofauti ikilinganishwa na msimu wa 2015/2016. Kwa mfano, wastani wa bei ya mahindi kwa gunia la kilo 100 iliongezeka kutoka Shilingi 59,873 msimu wa 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 99,527 msimu wa 2016/2017, sawa na ongezeko la asilimia 66.23. Bei ya mchele kwa gunia la kilo 100 iliongezeka kutoka wastani Shilingi 177,340 msimu wa 2015/16 hadi Shilingi 191,289 msimu wa 2016/17. Bei ya gunia la maharage la kilo 100 iliongezeka kutoka Shilingi 162,383 mwaka 2015/2016 hadi kufikia Shilingi 178,101 mwaka 2016/2017, sawa na ongezeko la asilimia 9.68. Kupanda huko kwa bei ya mazao makuu ya chakula kumechangiwa na kushuka kwa ugavi kutokana na uhaba wa mvua katika msimu wa kilimo wa 2016/2017. Bei ya mazao mengine ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.11**.

(ii) Bei za Mifugo

121. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, wastani wa bei ya jumla ya ng'ombe wa daraja la pili ilishuka kutoka wastani wa Shilingi 1,110,227 mwaka 2016 hadi Shilingi 1,105,321 mwezi Machi, 2017, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Bei ya ng'ombe wa daraja la tatu ilishuka kutoka Shilingi 830,888 mwaka 2016 hadi shilingi 731,300 mwezi Machi, 2017, sawa na upungufu wa asilimia 11.9. Kushuka kwa bei hizo kumechangiwa na kushuka kwa ubora wa mifugo kutokana na uhaba wa malisho. Aidha, uhaba wa malisho uliwafanya wafugaji kuuza mifugo kwa wingi na hivyo bei kushuka. Wastani wa bei ya mifugo ni kama ilivyooonekana katika **Jedwali Na.12a**.

(ii) Bei ya Mbogamboga na Matunda

122. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na TAHA kupitia ufadhili wa Serikali ya Uswisi, imeanzisha Mfumo wa Taarifa za Masoko ya Matunda na Mbogamboga ambapo programu maalum inayotumia simu za kiganjani huwafikishia wakulima taarifa za bei na masoko kwa wakati. Wakusanya taarifa za masoko 20 wa TAHA wamepatiwa mafunzo na simu za kiganjani zinazotumika katika kukusanya na kusambaza taarifa hizo.

123. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusambaza taarifa za mazao na mifugo kwa wadau kwa njia ya radio, luninga, ujumbe wa simu za kiganjani, mitandao ya kompyuta na magazeti. Taarifa za bei za mazao makuu ya chakula zilikusanywa kutoka katika masoko 26 ya miji ya mikoa na bei za rejareja kutoka masoko 114. Aidha, Wizara imeboresha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa hizo kwa kuwapatia wakusanyaji taarifa wote 140 simu za kiganjani za kisasa (smart phones) zinazotumika kukusanya na kutuma taarifa hizo kwa wakati.

(iii) Bei ya Baadhi ya Bidhaa za Viwandani (Sukari na saruji)

124. *Mheshimiwa Spika*, bei ya sukari imeongezeka kutoka wastani wa Shilingi 2,256 kwa kilo mwezi Aprili, 2016 hadi kufikia wastani wa Shilingi 2,628 mwezi Aprili, 2017 sawa na ongezeko la asilimia 17. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji ambazo zimesabisha sukari kuuzwa kwa bei ya jumla ya wastani ya Shilingi 2,000 kwa kilo. Bei ya saruji imeshuka kutoka wastani wa Shilingi 12,000 kwa mfuko wa kilo 50 jijini Dar es Salaam mwezi Aprili, 2016 hadi kufikia wastani wa Shilingi 9,500 mwezi Aprili, 2017 sawa na punguzo la asilimia 20.83. Bei ya saruji jijini Mwanza imepungua kutoka Shilingi 16,800 hadi Shilingi 16,500 na Arusha kutoka Shilingi 14,000 hadi Shilingi 12,500. Kushuka kwa bei ya saruji nchini ni matokeo ya ongezeko ya uzalishaji wa bidhaa hiyo kutoka katika viwanda vya ndani (*Jedwali Na. 12b*).

c) Kutangaza Bidhaa za Tanzania

125. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kuptitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) iliwezesha Maonesho ya 40 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF). Katika maonesho hayo, mataifa 30 yalishiriki ikilinganishwa na mataifa 25 yaliyoshiriki katika Maonesho ya 39 mwaka 2015. Makampuni 2,500 yalishiriki katika maonesho ya mwaka 2016 ikilinganishwa na makampuni 2,305 yaliyoshiriki katika mwaka 2015, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.6. Kati ya makampuni hayo, 501 yalikuwa ya kutoka nje ya nchi na 1,999 yalikuwa ni makampuni ya ndani ya nchi. Aidha, Wizara sita (6) na taasisi 37 za Serikali zilishiriki.

126. *Mheshimiwa Spika*, katika maonesho hayo, maulizo ya bidhaa kwa soko la nje (export enquiries) yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani milioni 119.91 yakilinganishwa na maulizo ya thamani ya Dola za Kimarekani milioni 108.6 katika Maonesho ya 39 ya mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 10.41. Bidhaa zilizopata maulizo kwa wingi ni kahawa, korosho, chai, bidhaa za vyakula, asali, viungo (iliki na tangawizi) na bidhaa za sanaa za mikono. Maulizo ya bidhaa kutoka nje (import enquiries) yamepungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 90.5 katika maonesho ya mwaka 2015 hadi Dola za Kimarekani milioni 89.77 katika maonesho ya mwaka 2016.

127. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara pamoja na Taasisi 11 zilizo chini yake zilishiriki Maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Ngongo Mkoani Lindi. Katika maonesho hayo, jumla ya wajasiriamali 28 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mbeya, Mtwara, Pwani na Zanzibar waliwezesha kushiriki na kuonesha bidhaa zao kuptitia banda la Wizara ya Viwanda ya Biashara na Uwekezaji.

d) Kuimarisha Biashara za Mipakani

128. *Mheshimiwa Spika*, jitihada za kuimarisha biashara za mipakani zimewesha kuanzishwa kwa vituo nane (8) vya

Ukaguzi wa Pamoja Mipakani (One Stop Border Posts – OSBP) baina ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC. Vituo hivyo ni:- Holili/Taveta (Tanzania na Kenya); Sirari/Isebania (Tanzania na Kenya); Namanga/Namanga (Tanzania na Kenya); Kabanga/Kobero (Tanzania na Burundi); Rusumo/Rusumo (Tanzania na Rwanda); Mtukula/Mtukula (Tanzania na Uganda); Horohoro/Lungalunga (Tanzania na Kenya) na Tunduma/Nakonde (Tanzania na Zambia). Pamoja na ukaguzi wa pamoja katika mipaka hiyo, utaratibu wa biashara kwa wafanyabiashara wadogo katika mipaka hiyo (Simplified Trade Regime – STR) unatumika katika mipaka yote yenye vituo hivyo.

129. *Mheshimiwa Spika*, katika kufanikisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Mpaka wa Tunduma/Nakonde upande wa Tanzania, mkandarasi wa ujenzi wa Kituo hicho Kampuni ya *Nadhra Engineering Construction Company Limited* ameanza ujenzi mwezi Novemba, 2016. Ujenzi huo unagharamiwa na Shirika la *Trade Mark East Africa* (TMEA). Ujenzi unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18. Aidha, Serikali inatarajia kujenga Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja cha Mpakani katika mpaka wa Kasumulu/Songwe (Tanzania/Malawi) ili kuendeleza biashara na nchi jirani ya Malawi.

4.2.5 Sekta ya Uwekezaji

a) Kuhamasisha Uwekezaji wa Ndani

130. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara iliendelea na jukumu lake la kuratibu na kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi nchini kwa kushirikiana na taasisi nyingine za sekta ya umma na sekta binafsi kupitia njia mbalimbali. Mnamo mwezi Septemba, 2016, Wizara ilishiriki katika Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Morogoro lililolenga kuhamasisha uwekezaji katika mkoa huo na mikoa ya jirani. Vile vile, Wizara ilishiriki katika uzinduzi wa Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja ya Mkoa wa

Simiyu ambayo inalenga kuhamasisha uwekezaji utakaotumia fursa na rasilimali zinazopatikana katika wilaya za mkoa huo.

b) Kuhamasisha Uwekezaji Kutoka Nje ya Nchi

131. *Mheshimiwa Spika*, katika kuvutia wawekezaji wa nje na kuwaunganisha wafanyabishara wa Tanzania na wale wa nje, Wizara ilianda makongamano mahsusiyaliyofanyika nchini kati ya Tanzania na nchi za nje. Nchi ambazo zililetu ujumbe wa wafanyabiashara nchini ni pamoja na Austria, Belgium, China, Finland, India, Morocco, Rwanda na Uturuki. Vilevile, Wizara kuitia Kituo cha Uwekezaji kilienda mikutano ya uwekezaji katika nchi rafiki kwa uratibu wa ofisi za ubalozi na sekta binafsi katika nchi za China, India, Israel, Italia, Kenya, Misri na Rwanda. Wizara immeanzisha utaratibu wa kuwasiliana na wawekezaji wa nje kuitia balozi zetu za nje. Chini ya utaratibu huo, mabalazi wetu wanapewa taarifa maalum zinazowasadida kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje.

132. *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Wizara immeendelea kupokea wageni binafsi na taasisi za umma kutoka nchi za nje kuja kuangalia fursa za uwekezaji nchini. Wageni hao walitoka nchi za Afrika ya Kusini, China, India, Italia, Lebanon, Marekani, Misri, Ufaransa, Uganda, Uingereza na Umoja wa Falme za Kiarabu. Baadhi ya sekta zilizoonesha kuvutiwa kwa uwekezaji ni pamoja na uzalishaji wa betri za kuhifadhi nishati ya juu, uzalishaji wa magadi soda, dawa za binadamu na vifaa tiba, ufugaji wa ng'ombe wa kisasa na usindikaji wa maziwa, kilimo cha miwa na uzalishaji sukari, nguo na mavazi, mbolea, saruji, juisi za matunda, bidhaa za kemikali za petroli, sigara, usindikaji wa kahawa, mita za maji, uzalishaji wa umeme, ujenzi wa miundombinu, kuanganisha magari na ujenzi wa nyumba za makazi. Ili kufanikisha wageni hao kuwekeza, Wizara iliratibu mikutano na Wizara na taasisi mbalimbali kwa lengo la kupata taarifa mbalimbali za uwekezaji kutoka kwenye sekta husika ili kuwawezesha wawekezaji kufanya uamuhi sahihi wa uwekezaji.

c) Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji

133. *Mheshimiwa Spika*, ili kuharakisha ujenzi wa uchumi wa viwanda nchini, ni jukumu la Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuhakikisha sheria, kanuni na utendaji wa sekta ya umma unakuwa rafiki. Tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani imeonesha nia ya dhati ya kuendelea kuimarisha mazingira ya uwekezaji kama inavyojidhihirisha katika juhudzi za kupiga vita rushwa, kuongeza uwajibikaji na utendaji kwenye sekta ya umma na kudhibiti ukwepaji wa kodi.

134. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na jitihada zinazoendelea, Tanzania imepanda nafasi katika ripoti za dunia za urahisi wa kufanyaji biashara. Kwa mfano, katika Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu Urahisi wa Kufanya Biashara (*Ease of Doing Business*) ya mwaka 2017 inaonesha Tanzania imepanda nafasi 12 kutoka nafasi ya 144 mwaka 2016 mpaka nafasi ya 132 mwaka 2017 kati ya nchi 190 duniani. Katika ripoti hiyo, Tanzania pia imepanda kwa kigezo cha kasi ya maboresho kutoka wastani wa 50.59 mwaka 2016 mpaka 54.48 mwaka 2017 ambao ni juu ya wastani wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara wa 49.51. Baadhi ya vigezo ambavyo Tanzania imefanya vizuri ni upatikanaji wa mikopo na usimamizi wa mikataba ambapo kati ya nchi 190 Tanzania imekuwa ya 44 na 59 mtawalia. Vigezo ambavyo hatujafanya vyema na nafasi zake kwenye mabano vinajumuisha taratibu za kuanzisha biashara (135), kupata vibali vyya ujenzi (136), urahisi wa kulipa kodi (154) na urahisi wa taratibu za forodha (180). Aidha, katika ripoti ya mwaka 2016 ya Taasisi ya *Heritage Foundation* ya Marekani inayopima uhuru wa kiuchumi, imeonesha kuwa katika Afrika Mashariki, Tanzania ni ya pili kwa kuwa nafasi ya 105 baada ya Rwanda iliyoshika nafasi ya 51 kati ya nchi 180 duniani.

135. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na kuwa na unafuu kwa baadhi ya vigezo, Serikali inatambua mapungufu ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi. Utafiti uliofanywa wa Timu ya Serikali uliofadhliliwa na Benki ya Dunia chini ya uratibu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji umeainisha mambo yanayopaswa kufanyiwa kazi ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

136. *Mheshimiwa Spika*, shughuli za uwekezaji zinahitaji uratibu na ushirikiano mzuri wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, Serikali inatambua pia changamoto wanazopata katika kuanzisha au kupanua shughuli zao za uzalishaji na uwekezaji. Katika kuimarisha mahusiano na ushirikiano huo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ilitisha mukutano wa mashauriano (Dialogue Meeting) pamoja na sekta binafsi tarehe 11 Aprili, 2017 uliohudhuriwa na viongozi wa Serikali, Waheshimiwa Wabunge na wafanyabiashara zaidi ya 200. Majadiliano ya mukutano huo yalienda vizuri na yalisaidia sana kuongeza ari na utashi wa sekta binafsi kushirikiana na Serikali katika jitihada za maboresho ya sekta ya umma na usimamizi ili kurahisisha mazingira ya biashara na kukuza uchumi. Aidha, sekta binafsi ilielezea pia changamoto ambazo kama zitafanyiwa kazi zitasaidia kuimarisha ubia na upendo kwa sekta ya umma na sekta binafsi.

d) Uboreshaji wa Mazingira ya Kufanya Shughuli

137. Mheshimiwa Spika, ili nchi ivutie na kukuza uwekezaji wa ndani na kuvutia wawekezaji kutoka nje, yapo mambo manne muhimu ya kufanya. Kwanza, ni lazima nchi iwe na amani na utulivu. Katika hilo tunamshukuru Mungu nchi yetu inafanya vizuri. Pili, ni lazima mwenendo wa uchumi wa nchi uwe na utulivu, uimara na uendelevu, yaani kuwe na macroeconomic stability and sustainability. Vigezo mbali mbali vyaa kiuchumi vinaonesha kuwa nchi yetu inaendelea kufanya vizuri kwenye mwenendo wa uchumi. Tatuhii, ni lazima nchi iwe na miundombinu na huduma nzuri za kuwezesha ufanyaji wa shughuli za uchumi. Hii ni pamoja na kuwa na barabara nzuri, reli inayofanya kazi kwa ufanisi, bandari zinazofanya kazi kwa ufanisi, usafiri mzuri wa barabara, anga na kwenye maji na kadhalika. Kadhalika ili kufanikisha uwekezaji ni muhimu kuwa na nishati ya uhakika na ya bei nafuu, na ni lazima upatikanaji wa maji uwe na uhakika. Jambo la nne la muhimu katika kuvutia na kukuza uwekezaji ndani ya nchi ni kuweka mazingira ya kisera, kisheria, kikanuni na kiutendaji ambayo ni wezeshi kwa ajili ya kuendesha shughuli za kiuchumi. Tunapozungumzia mazingira mazuri ya kufanya shughuli za kiuchumi tunazungumzia hayo mambo manne,

yaani; amani na utulivu, mwenendo mzuri wa uchumi wa nchi, miundombinu bora na huduma nzuri wezeshi na mwisho ni kuwa na sera, sheria, kanuni na utendaji ambao unalenga kuwezesha shughuli za kiuchumi za wananchi na wawekezaji kwa ujumla.

e) Uratibu wa Urahisi wa Kufanya Shughuli

138. *Mheshimiwa Spika*, uendelezaji na uimarishaji wa uwekezaji pamoja na mambo mengine unahitaji kuwepo kwa mfumo thabiti wa uratibu wa urahisi wa kufanya shughuli. Chini ya mfumo huo, taarifa mbalimbali toka kwa wadau hupokelewa, huchambuliwa na kufanya majadiliano na Serikali au sekta binafsi kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara. Kwa kutambua umuhimu wa kurahisisha ufanyaji wa shughuli, mwezi Oktoba, 2016, Wizara ilianzisha rasmi Dawati la Kuratibu Wepesi wa kufanya Shughuli (*Ease of Doing Business - EODB*) ili kushughulikia changamoto zinazojitokeza katika kufanya shughuli za kiuchumi kwa ufanisi.

139. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Dawati la Kuratibu Wepesi wa kufanya Shughuli limepokea na kushughulikia masuala yanayohusu kodi kwenye sukari na marejesho ya kodi; Ushuru wa Forodha kwenye uagizaji wa mafuta na sabuni; na malighafi yanayotumika kuzalisha *Automotive Leaf Spring; Gypsum Board* na bidhaa zake. Dawati limeshughulikia kwa kina vigezo vinavyopelekea bidhaa zinazozalishwa nchini kuwa aghali katika soko la ndani ikilinganishwa na bidhaa zinazotoka nje. Kwa kutaja baadhi, lipo tatizo linalohitaji ufumbuzi kwani, kwa mfano, wakati vyandarua vinavyotoka nje ya nchi havitozwi baadhi ya ushuru na kodi, malighafi za kuzalisha bidhaa hizo nchini hutozwa ushuru. Katika Sekta ya Ngozi ambayo tunaitegemea kuzalisha ajira nyingi, ngozi zinazozalishwa nchini moja ya vigezo vinavyoinyima faida ya ushindani ni kemikali zinazotumika kuongeza thamani ya ngozi hizo kutozwa kodi wakati ngozi zinazotoka nje hazitozwi kodi huko zinakozalishwa.

140. *Mheshimiwa Spika*, uratibu chini ya Dawati hilo ni endelevu na unahuishwa uratibu wa masuala yanayopokelewa,

kuyachambua, kuyaelekeza katika sekta husika, kuwa na vikao vya kisekta na wadau wake kwa lengo la kuchambua hoja na hatimaye kuwasilisha mapendekezo katika *Tax Task Force* wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya kila mwaka. Hivyo, nitoe rai kwa wadau wote kuwasilisha masuala yanayokwamisha utekelezaji wa ujenzi wa uchumi wa viwanda na masuala yote ya kisekta kwa wakati. Wizara itashukuru kupata ushirikiano wa uhakika pale tutakapohitaji maelezo au taarifa zaidi za kuwezesha kuyafahamu kwa undani masuala husika, kufanya tathmini na hivyo kushauri na kutoa maamuzi sahihi.

4.3 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI CHINI YA WIZARA

4.3.1 Shirika la Maendeleo la Taifa

(i) *Makaaya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga - Njombe*

141. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara kuptitia NDC iliendelea na majadiliano juu ya mauziano ya umeme kati ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Kampuni ya Ubia ya TCIMRL. Mfumo uliokubalika na pande zote mbili ni mwekezaji kujenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuendesha (Build Own and Operate - BOO). Mauzo ya umeme kwa TANESCO hayajumuishi gharama za uwekezaji. Kuhusu ujenzi wa mradi, Kamati ya Taifa ya Uwekezaji imepitia kwa mara nyingine vivutio vilivyoombwa na mwekezaji kwa lengo la kutafuta manufaa zaidi kwa Taifa katika mradi huo. Suala la umeme na vivutio litawasilishwa kwa mamlaka za maamuzi wakati wowote ili mradi uanze. Aidha, mwekezaji amekwisha wasilisha nchini fedha za fidia na ameihekikishia Wizara kuwa yupo tayari kulipa fidia kwa watu watakaopisha mradi pindi apatapo Tangazo la Serikali (Government Notice - GN) kuhusu vivutio.

(ii) Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha

142. *Mheshimiwa Spika*, mradi unaojengwa katika Eneo la Viwanda la TAMCO, Kibaha lenye ukubwa wa ekari 232 utahusisha sekta za uunganishaji magari, viwanda vya nguo na mavazi na viwanda vya dawa za binadamu. Hadi Aprili, 2017, mgawanyo wa Eneo la Viwanda la TAMCO, Kibaha ulikuwa umekamilika. Katika mgawanyo huo, viwanda vya nguo na mavazi vimetengewa ekari 95, viwanda vya magari ekari 64 na eneo la ekari 73 limetengwa kwa ajili ya Sekta ya Viwanda vya Dawa za Binadamu na Vifaa Tiba. Wawekezaji waliokwishajitokeza mpaka sasa ni pamoja na Kampuni ya *Global Packaging* walioanzisha kiwanda cha vifungashio na Kampuni ya Kuunganisha Matrekt ya *URSUS*. Aidha, wawekezaji walio katika majadiliano ili kuwekeza katika eneo hilo ni pamoja na Kampuni ya Magari ya *TATA* na Kampuni ya *URSUS* inayopanga kuunganisha mabasi hapa nchini.

143. *Mheshimiwa Spika*, katika eneo la ekari 95 lililotengwa kwa ajili ya viwanda vya nguo na mavazi katika eneo la Viwanda TAMCO, Wizara kupitia NDC inajadiliana na *Gatsby Africa* kupitia Kitengo cha Nguo na Mavazi (Textile Development Unit -TDU) kwa ajili ya kusaidia kuendeleza eneo kwa kuandaa Mpango Kabambe (*detailed Master Plan*) na kuvutia uwekezaji. Andiko la Makubaliano (MoU) tayari limetiwa saini kati ya Wizara na *Gatsby Africa*.

144. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia NDC imekamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu (Biolarvicides), *Tanzania Biotech Ltd* na uzalishaji umeanza. Ili kukamilisha mradi huo, Serikali kupitia Wizara ilitoa Shilingi bilioni 2.1 kulipia gharama za ukandarasi na madeni ya wafanyakazi. Aidha, NDC ilipata mkopo wa Shilingi bilioni 4.553 kutoka NSSF kama mtaji wa kuanza uzalishaji wa kibiashara. Uzalishaji ulianza mwezi Januari, 2017 na kufikia Aprili, 2017 lita 101,080 za Viuadudu zilikuwa zimeuzwa. Kati ya hizo, lita 100,000 ziliuzwa nchini Niger kwa Dola za Kimarekani 460,000 sawa na Shilingi bilioni 1.012; lita 440 zenye thamani ya Shilingi milioni 17.424 ziliuzwa kwa Taasisi ya Madaktari

Wasio na Mipaka (Doctors Without Borders); lita 200 zenye thamani ya Shilingi milioni 2.64 ziliuzwa kwa Kampuni ya *Mabao Investment and General Pest Control*, na lita 440 zenye thamani ya Shilingi milioni 5.808 ziliuzwa kwa Halmashauri ya Mji wa Geita.

145. *Mheshimiwa Spika*, wakati uzalishaji wa Viuadudu ukiendelea, mazungumzo yanakamilishwa na Wilaya ya Mbogwe kununua lita 800 zenye thamani ya Shilingi 10,560,000 na Madaktari Wasio na Mipaka kununua lita 500 zenye thamani ya Shilingi 19,000,000. Aidha, juhudzi za kutafuta soko la ndani na nje zinaendelea kwa kuhusisha Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba wa Manunuzi (Offtake Agreement) kati yake na NDC. Kampuni ya *LABIOFAM* imeonesha utayari wa kuuza Viuadudu vinavyozalishwa katika kiwanda hicho kwenye masoko yake katika nchi mbalimbali. Aidha, Kampuni ya *Tanzania Biotech Ltd* inayozalisha Viuadudu husika imeelekezwa kuimarisha Kitengo cha Masoko ili kuweza kutangaza na kuuza bidhaa hiyo muhimu katika kupambana na ugonjwa wa malaria.

(iii) Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha

146. *Mheshimiwa Spika*, Mradi wa Uchimbaji Magadi Soda unatekelezwa na Wizara kuititia NDC katika Bonde la Engaruka, Wilaya ya Monduli. Mradi unahusu ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha magadi soda tani milioni moja kwa mwaka kwa ajili ya matumizi ya viwanda hususan vya dawa, vioo na sabuni. Aidha, katika mwaka 2016/2017, utafiti wa kina wa maji safi (detailed hydrological study) kwa ajili ya matumizi ya kiwanda, usanifu wa miundombinu ya maji na utayarishaji wa *Bill of Quantities* (BoQ) vimefanyika. Taarifa ya BoQ inategemewa kuwasilishwa mwezi Juni, 2017.

147. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kuititia NDC imekutana na kampuni mbili kutoka China ambazo zimeonesha nia ya awali ya kuwekeza katika Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka. Kampuni hizo ni *Inner Mongolia Berun Holding Company Ltd* ambayo ilitembelea mradi huo mwezi Julai, 2016 na *China National Complete Plants Import and Export Cooperation Ltd* iliyotembelea mradi husika mwezi

Agosti, 2016. Katika ziara hizo, Kampuni hizo zilichukua sampuli za magadi soda kwa ajili ya utafiti wa kimaabara. Pia, makampuni hayo yalifanya ukaguzi wa reli na barabara kutoka Arusha hadi Tanga na Bandari ya Tanga ili kuwa na uhakika wa usafirishaji. Taarifa kuhusu nia ya kuwekeza katika mradi huo itapatikana pindi makampuni husika yatakapowasilisha mapendekezo yao. Aidha, upekuzi wa makampuni hayo unafanyika kupitia balozi zetu.

(iv) Kiwanda cha Kutengeneza Matairi Arusha

148. *Mheshimiwa Spika*, kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imefanya utafiti uliolenga kuangalia namna bora ya kufufua Kiwanda cha Matairi Arusha. Taarifa ya awali imebaini kuwa ili kiwanda hicho kiweze kuendelea mambo makuu manne yanatakiwa kuzingatiwa. Kwanza, mitambo iliyopo ambayo ilifungwa kwenye miaka ya 60 ikiwa imetumika haifai kwa uzalishaji wa kiushindani. Pili, inatakiwa kufungwa mitambo inayotumia teknolojia ya kisasa itakayowezesha kiwanda kufanya kazi kwa ufanisi na kwa kuzingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Tatu, kiwanda kipanuliwe ili kiweze kuzalisha matairi ya aina mbalimbali na kwa wingi ili kupata faida ya uzalishaji kwa wingi (economies of scale). Nne, kiwanda hicho kiendeshwe na Sekta Binafsi, Serikali ikiwa mbia kwa hisa zinazolingana na rasilimali za kiwanda zilizopo.

4.3.2 Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji wa Bidhaa kwa Ajili ya Mauzo Nje

(i) Bagamoyo SEZ

149. *Mheshimiwa Spika*, mradi wa Bagamoyo SEZ unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya Kwanza itaendelezwa kwa ubia kati ya Kampuni ya *Merchants Port Holdings Company Limited* (CMPort) ya China na Mfuko wa Hifadhi ya Hazina wa Serikali ya Oman (State General Reserve Fund-SGRF). Awamu hiyo itahusisha eneo la hekta 3,000 kwa ajili ya ujenzi wa Bandari (Sea Port) kwenye eneo la hekta 800 na uendelezaji wa Eneo Maalum la Viwanda

(Portside Industrial City) kwenye eneo la hekta 2,200. Awamu hiyo inahusisha pia ujenzi wa miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) ili kuunganisha eneo la mradi na maeneo mengine ya nchi. Eneo linalobakia la hekta 6,800 litaendelezwa katika Awamu ya Pili itakayokwenda sambamba na awamu ya kwanza kwa kuzingatia Mpango Kabambe wa mradi.

150. *Mheshimiwa Spika*, ili kuongeza kasi ya ulipaji wa fidia kwa watu ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kupisha mradi wa Bagamoyo SEZ, tarehe 7 Desemba, 2016 Serikali iliamua sekta binafsi ipewe nafasi kubwa ya kutekeleza mradi huo ikiwepo kulipa fidia. Kufuatia maamuzi hayo, tarehe 30 Machi, 2017, wawekezaji waliwasilisha andiko la kuendeleza hekta 3,000. Eneo litakaloendelezwa na wawekezaji hao linajumuisha eneo ambalo halijalipiwa fidia. Andiko hilo linapitiwa na wataalam wa Serikali kabla ya kuendelea na majadiliano kati ya Serikali na wabia hao.

151. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa huduma muhimu zinafika katika eneo la mradi, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa miundombinu wezeshi ikiwemo barabara kutoka Tegeta hadi Bagamoyo na kutoka Bagamoyo hadi Mlandizi; mradi wa maji kutoka Bwawa la Kidunda hadi Bagamoyo; na Bomba la Gesi kutoka Tegeta hadi Bagamoyo. Aidha, maandiko ya miradi ya miundombinu wezeshi (barabara, reli, umeme, maji, gesi na mifumo ya mawasiliano) kwa ajili ya kupata fedha kutoka vyanzo mbalimbali likiwemo Jukwaa la Ushirikiano baina ya China na Afrika (FOCAC) yamekamilika.

(ii) Kuendeleza Mradi wa Kurasini Logistic Centre

152. *Mheshimiwa Spika*, eneo la Kurasini lina ukubwa wa ekari 62, ambapo kiasi cha fidia kilicholipwa ni Shilingi bilioni 101 kwa kaya 1,019. Eneo hilo limetangazwa kwa wawekezaji tarehe 20 Desemba, 2016 kupitia Gazeti la *Daily News*. Jumla ya makampuni matatu yameonesha nia ya kuendeleza eneo hilo. Taratibu za kumpata mwekezaji atakayeliendeleza kwa kujenga miundombinu pamoa na kuleta waendeshaji wa viwanda mbalimbali zinaendelea

chini ya Mamlaka ya EPZ. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya EPZ inakamilisha mapendekezo mahsus ikuhusu utaratibu wa ubia utakaotumika kwa ajili ya maamuzi ya Serikali.

(iii) Star City SEZ

153. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya *Star City* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Watanzania na Wasingapore inayojishughulisha na ujenzi wa maeneo ya uwekezaji wa viwanda (industrial parks) nchini, inaendeleza eneo la ekari 10,661 lililoko eneo la Kingolwira, Mkao wa Morogoro. Kati ya eneo hilo, ekari 500 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu, ekari 100 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya rufaa na ekari 1,000 kwa ajili ya makazi ya wananchi wa Morogoro wanaopisha mradi huo. Eneo litakalobakia la ekari 9,061 ni mahsus kwa utekelezaji wa mradi wenyewe. Kwa kuanzia Kampuni ya ubia itaweka miundombinu kwa ajili ya viwanda. Jiwe la msingi la kiwanda cha kwanza katika eneo hilo cha mavazi ya michezo cha *Mazava Fabrics Ltd* kitakachotumia eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 25,000 liliwekwa tarehe 19 Desemba, 2016. Kiwanda hicho kinategemewa kutoa ajira 7,000. Hata hivyo, mradi huo haukuanza kwa kasi ya kuridhisha kutokana na madai ya Manispaa ya Morogoro kutaka mradi utekelezwe baada ya Mpango Kabambe wa Mji wa Morogoro kukamilika, kutokuwepo kwa kituo kikubwa cha kupoozea umeme (Power Station) na uvamizi wa sehemu ya eneo la mradi.

(iv) SEZ Zilizotangazwa

154. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Maeneo Maalum ya Uwekezaji (Special Economic Zone - SEZ) manane (8) yalikidhi vigezo vyta kuanzisha SEZ na kutangazwa. Maeneo hayo ni: *Manyara Special Economic Zone, Magnis Technologies (Tanzania) Ltd, Eliyafood Overseas Ltd, Texland Africa Ltd, Spincast Engineering Ltd, Mara Special Economic Zone, Kigamboni SEZ Co. Ltd* na *Nuts Depots and Plus Co. Ltd*. Uanzishaji wa maeneo hayo maalum ya uwekezaji utaongeza kasi ya ujenzi wa viwanda kutokana na faida za vivutio vinavyoendana na maeneo hayo.

(v) Mafunzo ya Ufundı Stadi

155. *Mheshimiwa Spika*, katika juhudı za Serikali kuongeza ajira nchini, Wizara kupertia Mamlaka ya EPZ kwa kushirikiana na wawekezaji na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi na Ajira) kupertia Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi ilibuni na kuanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa vijana juu ya stadi za uzalishaji viwandani. Mafunzo hayo yanahusu usanifu, ukataji na ushonaji wa mavazi yanayosafirishwa nje ya nchi na kuuzwa katika masoko ya kimataifa kama vile AGOA. Mpango wa mafunzo hayo umeanza kutekelezwa kwa Kiwanda cha *TOOKU Garments Ltd* kilichoko katika Eneo Maalum la Viwanda la Benjamin William Mkapa (BWM SEZ) lililopo Mabibo, Dar es Salaam na Kiwanda cha *Mazava Fabrics* kilichopo Morogoro. Lengo ni kukuza na kuimarisha mfumo huo ambao unaunganisha fursa za mafunzo na ajira viwandani. Kwa sasa uwezo wa Kituo cha Mafunzo cha Mabibo ni kudahili vijana katı ya 300 hadi 400 kila baada ya miezi mitatu na Kituo cha Morogoro ni kudahili vijana wasiopungua 200. Mpaka sasa jumla ya vijana 2,000 wamepata mafunzo hayo ambapo Kiwanda cha *TOOKU Ltd* kimefundisha vijana 1,600 na *Mazava* vijana 400.

156. *Mheshimiwa Spika*, lengo la mafunzo hayo ni kukidhi mahitaji na kwenda sambamba na kasi ya uwekezaji wa viwanda vya Tanzania hususan Kiwanda cha *TOOKU Garments Ltd* kilichopo Mabibo na *Mazava Fabrics* kilichopo Morogoro. Viwanda hivyo viwili vitaongeza idadi ya wafanyakazi kufikia 7,000 kila kimoja ambapo kwa sasa idadi ya wafanyakazi walioajiriwa ni 2,000 kila kila kiwanda. Aidha, uwepo wa wafanyakazi wengi wenye ujuzi na weledi katika Sekta ya Mavazi utavutia viwanda vya aina hiyo kuwekeza nchini. Mamlaka ya EPZ itaendelea kuanzisha na kuendeleza mfumo na utaratibu huo katika maeneo mengine yatakayoanzishwa kama *Special Economic Zone (SEZ)*.

4.3.3 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania

157. *Mheshimiwa Spika*, maendeleo endelevu ya viwanda yanahitaji pia masuala ya utafiti na hususan katika kubuni teknolojia mpya na rahisi zinazotumika katika uzalishaji ubora unaokidhi masharti ya soko la ndani na nje. Katika mwaka 2016/2017, TIRDO imeendelea na taratibu za kukamilisha usimikaji wa mtambo wa kurejeleza taka za ngozi. Baada ya kukamilika usimikaji, TIRDO imeanza kutoa mafunzo kwa Sekta ya Ngozi kuhusu uhifadhi na urejelezaji (recycling) wa taka za ngozi kwa kuziongezea thamani na kuhifadhi mazingira. Mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalam yamefanyika kwa Afisa Mtafiti mmoja na mafundi mchundo wawili kwa lengo kuijandaa kuendesha mafunzo mara baada ya kusimika mtambo.

158. *Mheshimiwa Spika*, katika juhudini za kuhakikisha malighafi za hapa nchini zinatumika katika uzalishaji viwandani, TIRDO kupitia maabara yake ya makaa ya mawe iliweza kupima na kutoa takwimu za ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana nchini. Kupitia takwimu hizo, Serikali iliweza kumaliza mgogoro uliokuwepo baina ya wawekezaji wa viwanda vya saruji kikiwemo Kiwanda cha DANGOTE kuhusu ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana nchini. Maabara hiyo ya makaa ya mawe ya TIRDO inatambulika kitaifa na imerasimishwa kuwa ndio maabara mahsusii katika kuainisha ubora wa makaa ya mawe nchini. Hivi sasa maabara hiyo imepewa jukumu la kubuni na kuboresha teknolojia ya briketi ya makaa ya mawe kwa ajili ya matumizi ya majumbani. Tayari Wizara imeunda kamati inayowahusisha TIRDO, NDC na Nyumbu (TATC) kuanzisha kiwanda kikubwa cha briketi ya makaa ya mawe. Mara kiwanda hicho kitakapofanya kazi kitasaidia kupunguza athari ya utumiaji wa kuni na mkaa. Katika kutekeleza jukumu hilo, TIRDO inashirikisha Washirika wa kimataifa, mionganii mwao ni Ubalozi wa India kupitia taasisi ya CSIR – India, na Serikali ya Uturuki kupitia taasisi yake ya Utafiti ya Tubitak. TIRDO tayari imeshapata mwekezaji kutoka Uturuki kupitia taasisi ya Tubitak ambaye ataweweza kwenye teknolojia ya kuzalisha briketi.

159. *Mheshimiwa Spika*, katika juhudii za kuhaulishaa teknolojia zitakazowezesha uanzishwaji wa viwanda, TIRDO kwa kushirikiana na wilaya ya Maswa inafanya tathmini juu ya teknolojia ya uzalishaji chaki iliyobuniwa na TIRDO na kuhaulishwa SIDO ili iweze kuboresha chaki zinazozalishwa ziweze kuwa katika ubora zaidi. Wilaya ya Maswa kuititia kiwanda chake cha uzalishaji chaki tayari imekwishaanza uzalishaji na kusambaza maeneo mbalimbali nchini. TIRDO pia inaongoza timu ya wataalamu kutoka Taasisi za Serikali zinazounda kamati ya kuanzisha viwanda vya pamba za mahospitali pamoja na maji ya dripu katika Mkoa wa Simiyu.

160. *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za kuimarisha ushiriki wa taasisi na wataalamu wa ndani katika Sekta ya Mafuta na Gesi (Wahandisi na Mafundi), TIRDO kwa kushirikiana na sekta binafsi imeanzisha program ya kutoa mafunzo maalum ya kuhakiki na kuwapatia vyeti tambuzi vya kimataifa (international certification) wanaofanya kazi za ufundi kama vile kuchomelea, kuhakiki ubora wa maungio na kuimarisha usalama kazini. Mafunzo hayo yanalenga kuhakikisha kuwa ushiriki wa Watanzania (local content) katika sekta hiyo muhimu ikizingatiwa kuwa Taifa linatarajia kuendesha miradi mikubwa kama vile ya Bomba la Mafuta Ghafi toka Uganda mpaka Tanga. Sekta hiyo inahitaji wataalam walio hakikiwa (certified) na wenye umakini na weledi katika kufanya kazi. Mafunzo hayo yakitolewa hapa nchini yatasaidia kupunguza gharama za kupeleka wataalam nje ya nchi kupata mafunzo hayo.

4.3.4 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo

161. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) limebuni na kuendeleza teknolojia zitakazowezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo na vya kati. Teknolojia zilizobuniwa na kuendelezwa katika mwaka 2016/2017 ni pamoja na mashine ya kutengeneza tofali zinazohifadhi joto (refractory bricks); jokofu litakalotumika kuhifadhi maiti au bidhaa mbalimbali; kiteketezi kidogo kinachobebeka (portable incinerator) kwa ajili ya zahanati na maabara za afya. TEMDO wamebuni mtambo wa kusindika na kusafisha mafuta ya

kula na mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji. Vilevile, chini ya ufadhili wa REA imekamilisha usimikaji wa mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya upepo na juu katika Kituo cha Olduvai Gorge, Ngorongoro inayozalisha KW 20 (**Jedwali Na. 13**).

4.3.5 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini

162. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia CAMARTEC kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeweza kutatua changamoto iliyopo kwenye upatikanaji wa mashine au vifaa vya kupandia, kupalilia, kuvunia na kuchakata mazao kabla ya kwenda sokoni au viwandani. Katika juhudzi za kuondokana na changamoto hizo, CAMARTEC imeshirikiana na Kampuni ya *ELMI* kuboresha vipandio vya kutumia trekta (tractor-drawn planters) ambavyo sasa vinafanya kazi kwa ufanisi zaidi kwenye mikoa ya Arusha na Manyara. Pia taasisi imeshirikiana na shirika lisilo la kiserikali la *BIORE* kutengeneza vipandio vya pamba vinavyokokotwa na ng'ombe kwa wakulima wa mkoa wa Simiyu. CAMARTEC kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Selian (SARI) imefanya majaribio ya mashine inayoendeshwa na trekta za matairi mawili (power tiller) za kupandia mazao.

163. *Mheshimiwa Spika*, CAMARTEC kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya *biogas* wa kujenga mitambo mikubwa katika Shule ya Sekondari Visitation Sanya Juu Mkoa wa Kilimanjaro, Sekondari ya Emboret na Mswakini Mkoa wa Manyara, Shule ya Msingi Msasani iliyopo Dar es Salaam, na Gereza la Karanga Mkoani Kilimanjaro. Teknolojia hiyo pia imetumika kwenye ujenzi wa mtambo wa maji taka katika hospitali ya CCBRT na nyumba za kuishi za TBA Bunju B kupitia mafundi waliopata mafunzo CAMARTEC.

4.3.6 Kampuni ya Mbolea Tanzania

164. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya Mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Co. Ltd -TFC) iliendelea na jukumu lake la kusambaza mbolea nchini. Katika mwaka 2016/2017 Kampuni

ilipewa jukumu la kusambaza mbolea yote iliyokuwa na ruzuku ya tani 32,394. Hadi tarehe 30 Aprili, 2017, jumla ya tani 27,500 sawa na asilimia 85 ya mbolea imesambazwa katika Halmashauri za mikoa 20 ya Iringa, Ruvuma, Njombe, Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Songwe, Mbeya, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Morogoro, Dodoma, Pwani, Mtwara, Kagera, Mara, Arusha, Singida. Usambazaji unaendelea katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro na Tanga. Kampuni hiyo pia imesambaza mbolea tani 1,753 ambayo haina ruzuku katika baadhi ya Mikoa hiyo. Hatua hiyo inafanya jumla ya mbolea iliyosambazwa na Kampuni ya TFC kuwa tani 29,253 hadi tarehe 30 Aprili, 2017.

165. *Mheshimiwa Spika*, Kampuni ya TFC imekuwa ikifanya majadiliano na Kampuni *Sirius Metals* ya Uingereza inayomiliki mashapo ya *Polyhalide* ya Yorkshire, Uingereza. Nia ya majadiliano hayo ni kuanzisha kampuni ya ubia ya kutengeneza mbolea za aina ya NPKs kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini na *Potash* kutoka Uingereza mbolea ambayo itakuwa na ubora wa hali ya juu. Kampuni ya TFC pia ilisaini Makubaliano ya Awali na Kampuni ya OCP ya Morocco tarehe 24 Oktoba, 2016 kwa ajili ya kununua mbolea za aina mbalimbali kabla ya uzalishaji haujaanza nchini.

4.3.7 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo

166. *Mheshimiwa Spika*, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ndio Taasisi ya Serikali yenye dhamana ya kuendeleza viwanda vidogo nchini. Chini ya dhamana hiyo, Shirika la SIDO linajikita zaidi katika kuwezesha Watanzania wenyewe nia ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo popote pale walipo. Aidha, katika mwaka 2016/2017 SIDO imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Uendelezaji na Uenezaji wa Teknolojia

167. *Mheshimiwa Spika*, SIDO inamiliki vituo vyataga maendeleo ya teknolojia saba katika mikoa ya Arusha, Kigoma,

Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Lindi na Shinyanga. Vituo hivyo vinajihuisha na uendelezaji wa teknolojia na utengenezaji wa mashine na vipuli na kutoa huduma za kiufundi kwa wajasiriamali wadogo mijini na vijiji. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya teknolojia mpya 30 zimetengenezwa na kuboreshwa kuititia vituo vya SIDO vya uendelezaji teknolojia (Technology Development Centre-TDCs). Huduma za ushauri wa kiufundi zilitolewa kwa wajasiriamali 3,433. Juhudi za kutafuta teknolojia kwa ajili ya mahitaji ya wajasiriamali wadogo ziliendelea, jumla ya teknolojia 73 zilipatikana kwa ajili ya matumizi ya wajasiriamali wadogo. Teknolojia zilizosambazwa zililenga uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo, upunguzaji wa matumizi ya miti na mazao yake kama nishati, zana za kilimo, vifaa vya ujenzi, usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa bidhaa zake, uchujaji wa asali na utengenezaji wa mishumaa, sabuni na useketaji. Teknolojia hizo zimesaidia kuongeza tija na kuimarisha ubora wa bidhaa za wajasiriamali.

b) Uanzishaji wa Miradi ya Viwanda Vidogo Vijijini

168. *Mheshimiwa Spika*, Shirika limeendelea kutoa huduma vijiji ili kuwawezesha wananchi walio wengi waweze kutumia fursa zilizopo. Mwelekeo wa utekelezaji ulilenga zaidi kuhakikisha kuwa kila wilaya inakuwa na bidhaa ya kuitambulisha kutokana na rasilimali zilizopo wilayani humo. Chini ya Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (One District One Product – ODOP) viwanda vidogo vipyta 161 ambavyo vilitengeneza ajira 1,098 katika wilaya mbalimbali vimeanzishwa mwaka 2016/2017. Pia, mkakati huo unatekeleza Sera ya Maendeleo ya Viwanda ambayo inalenga kusambaza viwanda hadi ngazi za vijiji.

c) Mafunzo

169. *Mheshimiwa Spika*, SIDO imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wajasiriamali ikiwa ni moja ya chachu ya kuimarisha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji. Mafunzo yaliyotolewa ni ya ujasiriamali; ujuzi maalum wa kiufundi katika uzalishaji mali na kuimarisha mbinu za kibashara na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi kwa walengwa hasa menejimenti, masoko, ubora

wa bidhaa, mbinu za uzalishaji mali, na uongozi wa vikundi/vyama. Jumla ya wajasiriamali 5,750 kuitia kozi 230 wamepata mafunzo yaliyowawezesha kupata maarifa na stadi za kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali. Mafunzo hayo yalifanyika mikoa yote nchini.

d) Ushauri

170. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya wajasiriamali wahitaji 8,911 walipatiwa huduma za ushauri katika maeneo mbalimbali yanayohusiana na uendelezaji wa biashara na shughuli za uzalishaji. Aidha, katika kukuza na kuchochea viwanda vidogo jumla ya wajasiriamali 3,433 waliweza kupatiwa ushauri wa ki-ufundi na maendeleo ya teknolojia. Ushauri ulilenga zaidi kupunguza ama kumaliza matatizo ya biashara ya wajasiriamali, kuwawezesha kuweka mipango yao ya biashara vizuri na kuitekeleza, kudhibiti ubora wa bidhaa, utengenezaji na utunzaji wa mitambo.

e) Huduma za Masoko

171. *Mheshimiwa Spika*, SIDO huwaelimisha wajasiriamali mbinu za kukabiliana na changamoto za masoko. Wajasiriamali husaidiwa kutambua hali na mahitaji ya soko kutohana na tafiti zilizofanyika na pia hushirikishwa katika maonesho mbalimbali ya bidhaa na huduma zinazoandaliwa na SIDO au Taasisi nydingine za ndani na nje ya nchi. Jumla ya maonesho matatu (3) ya kanda yaliyowashirikisha wajasiriamali 603 yaliandaliwa na SIDO na kuwawezesha washiriki kufanya mauzo taslimu na oda ya shilingi milioni 237.7. Aidha, vituo vya habari vya SIDO vimeweza kutoa habari za fursa mbalimbali kwa wajasiriamali 2,732. Huduma hiyo imewawezesha wajasiriamali licha ya kupata taarifa mbali mbali za biashara kutangaza bidhaa zao kuitia 'website' ya SIDO. Pia Shirika liliendelea kujenga uwezo wa wajasiriamali kupata na kutumia taarifa za masoko kuitia TEHAMA, ambapo jumla ya wajasiriamali wadogo 3,535 walinufaika na huduma hiyo.

f) Huduma za Fedha

172. *Mheshimiwa Spika*, Shirika limeendelea kutoa mikopo kutoka Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara

na Wananchi (NEDF), na Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiriamali Wadogo (*Credit Guarantee Scheme*.) Jumla ya wajasiriamali 2,593 walipewa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 3.92 na mikopo hiyo iliwezesha kupata ajira za watu 9,424. Katika mikopo iliyotolewa asilimia 48.4 ilitolewa kwa wanawake na asilimia 33 ya mikopo ilitolewa kwa miradi iliyo vijijini kuititia NEDF. Aidha, Mfuko wa Dhamana kwa Wajasiriamali Wadogo iliwezesha wajasiriamali tisa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 215 katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya, Morogoro na Singida.

g) Viatamizi

173. *Mheshimiwa Spika*, mpango wa viatamizi hutumika kuwalea wajasiriamali wenye ubunifu wa teknolojia, mawazo na bidhaa mpya kwa kuwajengea miundo mbinu ya kisasa na kuwapatia ushauri ili waweze kukuza ubunifu wao na hatimaye kunufaisha jamii. Katika mwaka 2016/2017, Mkakati wa kuendeleza ubunifu wa teknolojia, mawazo na bidhaa mpya kwa wananchi umeendelezwa kuititia viatamizi. Wajasiriamali wenye ubunifu wamejengewa uwezo kwa kuwezeshwa kupata mahali pa kufanya kazi, kupewa miundombinu ya kisasa na kuwapatia ushauri ili waweze kukuza ubunifu wao na hatimaye kuzalisha bidhaa. Jumla ya bidhaa 35 zilibuniwa na kutengeneza zikihusisha usindikaji wa vyakula, nishati jadidifu, bidhaa za ngozi, na mashine za aina mbalimbali. Aidha, SIDO imeendelea kufanya kazi na Washirika wa Maendeleo ili iweze kupeleka huduma zake kwa wananchi wengi zaidi. Kwa ufadhili wa UNIDO, SIDO imeweza kukamilisha kongano ya ubanguaji wa korosho iliyopo katika Mtaa wa Viwanda wa SIDO Mkoani Mtwara.

h) Kuboresha Huduma Zitolewazo na SIDO

174. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha 2016/2017, SIDO imetengeneza mifumo mbalimbali ili kuimarisha usimamizi wa kazi za shirika ambayo ni:

- (i) Mfumo wa TEHAMA wa kusimamia taarifa za shirika (Management Information System);
- (ii) Kuimaimarisha Mfumo wa kusimamia mfuko wa kuendeleza

- wajasiriamali na mahesabu ya shirika (Loan Performer) katika shughuli za uhasibu na mikopo;
- (iii) Kutengeneza Mfumo wa kuratibu utendaji wa vituo vya kuendeleza teknolojia (Manufacturing); na
- (iv) Kuanza utengenezaji wa Tovuti ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO Web Portal*).

4.3.8 Shirika la Viwango Tanzania

175. *Mheshimiwa Spika*, Shirika la Viwango limeendelea na udhibiti wa ubora wa bidhaa kutoka nje ya nchi kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa hizo katika nchi zinakotoka. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, jumla ya vyeti vya ubora (*Certificate of Conformity - CoCs*) 23,606 vimetolewa sawa na asilimia 73 ya malengo ya kutoa jumla ya vyeti 32,000 vya ubora wa bidhaa zitokazo nje ya nchi ikilinganishwa na vyeti 29,872 vilivyotolewa mwaka 2015/2016. Aidha, Shirika la Viwango limeendelea kushirikiana na mashirika mengine ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake na limesaini hati ya makubaliano (MoU) na Tume ya Ushindani (FCC) Februari, 2017, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) mwezi Novemba, 2016 na liko katika hatua za kufikia makubaliano ya kusaini hati ya makubaliano na SIDO.

176. *Mheshimiwa Spika*, vilevile katika kutekeleza majukumu yake, TBS inashirikiana na taasisi mbalimbali za serikali kama vile NIT, TPA, PBPA, TIRDO na BRELA. Katika kuimarisha udhibiti ubora, Shirika la Viwango Tanzania kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na taasisi zingine za serikali kama TRA, GCLA, EWURA, TanTrade, SUMATRA na NEMC limefanya ukaguzi wa kushtukiza sokoni ili kuhakikisha kuwa bidhaa hafifu, zilizo chini ya kiwango na ambazo si salama kwa mazingira pamoja na afya ya mlaji zinaondolewa sokoni.

177. *Mheshimiwa Spika*, TBS kwa kushirikiana na Taasisi nyingine waliteketeza tani 6.9 ya nguo za ndani zilizotumika, tani 1.2 za nyama na soseji, lita 106,909 za vilainishi vya injini (lubricants), betri 244 za magari, betri 1430 za sola. Vilevile, Shirika lilifanya

ukaguzi wa mabati kanda ya ziwa na pwani kwa waagizaji na watengenezaji (viwanda 24), zoezi ambalo lilifanikisha kuteketeza mabati 84,000 ambayo hayakukidhi viwango. Takribani lita 94,869 za vilainishi vyatia injini na Bendera za Taifa katoni 200 zilirudishwa katika nchi zilikotoka pamoja na aina 11 za pombe kali katoni 123,942 zilizofungashwa kwenye vifungashio vyatia plastiki vilizuiliwa kuingia sokoni.

178. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia mwezi Machi, 2017, leseni 179 za nembo ya ubora ya TBS zimetolewa, sawa na 81.4% ya lengo la kutoa leseni 220 kwa mwaka 2016/2017. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 42 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo kwa bidhaa za korosho, maji ya kunywa, mafuta ya alizeti, mvinyo, mikate, rosella, siagi ya karanga, jemu, hiliki, pilipili manga, unga wa soya, unga wa mahindi, kahawa, mafuta ya kujipaka, chaki, sabuni ya maji, sabuni ya kuogea, mabati, vigae, simenti na grisi. Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo nchini kwa kutumia fedha za ndani na msaada wa Mfuko wa Maendeleo wa Ulaya (EDF). Hadi kufikia Machi, 2017, mafunzo yalitolewa kwa wajasiriamali wadogo pamoja na wadau mbalimbali wapatao 1,523 wa sekta ndogo za viungo, mbogamboga na matunda, asali, alizeti pamoja na waagizaji wa bidhaa kutoka nchi na mawakala wa forodha. Wajasiriamli hao walitoka katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Singida na Tabora. Aidha, mafunzo hayo ambayo yaliwalenga zaidi wajasiriamali wadogo na wadau mbalimbali yalijikita zaidi katika dhana nzima za kuzingatia mifumo bora ya kuzalisha bidhaa zenyetani ubora ili kupata masoko pamoja na kusimamia ubora wa bidhaa hizo.

179. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia mwezi Aprili 2017, jumla ya mitambo 4,283 ilifanyiwa ugezi ikiwa ni sawa na asilimia 57.1 ya lengo la mwaka la kufanya ugezi wa mitambo 7,500. Katika kipindi hicho, Shirika limeandaa viwango 173 katika kilimo, chakula, uhandisi na vifungashio, sawa na asilimia 57.7 ya lengo la kutayarisha viwango 300 kwa mwaka. Shirika pia liliendelea kusimamia viwango vyatia kitaifa kwa kutumia mifumo iliyopo ya kuhakiki ubora.

180. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya sampuli 11,832 zilipimwa katika maabara mbalimbali za Shirika kwa lengo la kuhakiki ubora wake, hii ni sawa na 157.8% ya lengo la kupima sampuli 7,500 kwa mwaka. Ongezeko hili limesababishwa na Shirika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa nchini hususan Bandari ya Dar es Salaam. Pia, kufuatia makubaliano na TRA kutumia mfumo wa TANCIS kubaini mizigo inayopitia bandarini hali ya udanganyifu uliokuwa ukifanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu wakati wa kutoa mizigo imepungua. Juhudi hizi ziliongeza idadi ya sampuli za kupima na hivyo kuongeza mapato ya Shirika ambapo kufikia mwezi Machi 2017, Shirika lilivuka lengo kwa kukusanya asilimia 126 ya lengo la makusanyo ya mwaka mzima.

181. *Mheshimiwa Spika*, Shirika liliendelea kudumisha umahiri katika maabara zake nne ambazo zilishapata vyeti vyaa umahiri kwa kukaguliwa na *Southern African Development Community Accreditation* (SADCAS) tarehe 2 hadi 4 Novemba, 2016. Maabara hizo ni maabara ya ugezi, kemia, chakula na nguo. Aidha, mipango ya kupanua wigo wa umahiri ili kuongeza kiwango cha upimaji (*tests and matrices*) ulifanyika. Halikadhalika, miongozo ya ubora (Quality manuals) kwa kila maabara iliandikwa na kuiasili katika maabara zote za Shirika. Maabara ya uhandisi Ujenzi (Building and Construction) iko tayari kutuma maombi ya kupata umahiri. Vilevile, maabara ya uhandisi umeme na maabara ya uhandisi mitambo zipo katika hatua za kuhakikiwa uwezo wao zikilinganishwa na maabara nyingine katika upimaji (proficiency testing) kabla ya kutuma maombi ya kupatiwa cheti cha umahiri. Shirika la Viwango Tanzania linafanya juhudi za kuhakikisha maabara za uhandisi umeme, uhandisi mitambo, uhandisi ujenzi na vifungashio zinapata umahiri.

182. *Mheshimiwa Spika*, kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, jumla ya vyeti vyaa ukaguzi wa magari 24,634 vimekwishatolewa, sawa na asilimia 61.6 ya malengo ya vyeti 40,000. Aidha, kati ya magari hayo yaliyokaguliwa, magari 1,381 yalikaguliwa upya baada ya matengenezo (failed and re-tested after repair) na magari 29 yalikataliwa baada ya kushindwa kukidhi matakwa ya viwango vyaa ubora.

183. *Mheshimiwa Spika*, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi, 2017, Shirika lilifungua ofisi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Mbeya. Shirika pia limefungua ofisi mbili katika mipaka ya Tunduma na Kasumulo. Shirika limeimarisha vituo vilivyopo kwa kuongeza watumishi kutoka mmoja hadi wawili kwa kila kituo. Aidha, Shirika liko katika mpango ya kufungua ofisi katika mikoa ya Mtwara na Dodoma kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017.

184. *Mheshimiwa Spika*, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2016 hadi Machi, 2017, Shirika lilifanikiwa kufungua ofisi mbili katika mipaka ya Tunduma na Kasumulo. Shirika halikufungua ofisi ya Mtambaswala kutokana na uhaba wa watumishi katika Shirika. Aidha, shirika liliimarisha vituo vilivyokuwepo kwa kuongeza watumishi kutoka mmoja hadi wawili kwa kila kituo. Katika kipindi hicho, Shirika lilifanikiwa kufungua ofisi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Mbeya. Aidha, Shiriki liko katika mpango wa kufungua Shirika ofisi katika mikoa ya Mtwara na Dodoma kabla ya mwisho wa mwaka 2016/2017.

4.3.9 Chama cha Hakimiliki Tanzania

185. *MheshimiwaSpika*, hadikufikiaMachi2017, COSOTA imesajili wanachama (Kampuni, Vikundi na watu binafsi) wapatao 376 ikilinganishwa na wanachama 283 mwaka 2015/2016. Pia, imesajili kazi 2,074 ikilinganishwa na kazi 1,586 mwaka 2015/2016. Aidha, jumla ya Hati ya Uthibitisho wa Kazi (clearance certificate) 716 zilitolewa ikilinganishwa na hati 356 mwaka 2015/2016. Ongezeko la usajili kwa mwaka 2016/2017 ukilinganishwa na mwaka 2015/2016 limetokana na elimu iliyotolewa sambamba na uhamasishaji uliofanyika. Vilevile, katika kipindi hicho, COSOTA imekusanya mirabaha ya Shilingi 130,646,678.30 na kutoa leseni 482 kwa matumizi ya maonesho kwa umma na utangazaji. Makusanyo ya mwaka 2016/2017 yameongezeka ukilinganisha na mwaka 2015/2016 kutokana na kuweza kufika kwenye maeneo

ambayo awali hayakuwa yamefikiwa hususan katika Mkoa wa Dar es Salaam. Katika makusanyo hayo, asilimia 70 hugawanywa kwa wasanii, asilimia 30 hutumika kwa uendeshaji wa shughuli za COSOTA. Makusanyo ya Julai hadi Disemba 2016 ambayo yallikuwa Shilingi. 86,979,997 yaligawiwa mwezi Februari 2017 na makusanyo ya Januari hadi Juni 2017 yatagawiwa mwishoni mwa mwezi Juni au Julai 2017.

186. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia COSOTA imeendelea kusuluuhisha migogoro ya hakimiliki na hakishiriki ambapo migogoro 9 kati ya migogoro 26 imeshughulikiwa. Kesi nyingine za hakimiliki na hakishiriki za jinai na za madai zilizofunguliwa na Jamhuri au wadau wenyewe zinaendelea katika mahakama mbalimbali ndani na nje ya Dar es Salaam. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara kupitia COSOTA imefanya ukaguzi wa kazi za sanaa zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Manyara na Mwanza.

187. *Mheshimiwa Spika*, utaratibu wa urasimishaji wa kazi za filamu na muziki unasimamiwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Habari Utamaduni, Michezo na Wasanii. Kwa kupitia taasisi zake (Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki Tanzania (COSOTA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) na Bodi ya Filamu imeandaa utaratibu wa pamoja wa kurasimisha kazi za filamu kwa wamiliki wa kazi za filamu na muziki au waliopewa mamlaka ya kuzalisha na kusambaza kazi za filamu na muziki zenye stempu za TRA baada ya kupata uthibitisho toka taasisi zilizotajwa hapo juu. Matumizi ya Stempu yanarasimisha uuzwaji wa CD, DVD na kanda ili kukusanya kodi, kuzuia na kupunguza uharamia wa kazi za sanaa. Matumizi ya stempu pia husaidia katika kutofautisha kazi zilizo halali na zile zisizo halali. Aidha, kutokana na ushirikiano huo, takwimu za mwaka 2016/2017 kwa operesheni moja ya mwaka 2017 zimekamatwa kazi zaidi ya 1,964,605. Ongezeko hilo limetokana na ushirikiano wa Kamati ya Urasimishaji kwa Usimamizi iliyoongozwa na kuratibiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa.

4.3.10 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania

188. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) ina jukumu la kuendeleza biashara ya ndani na ya nje kwa kuendeleza bidhaa (product development), masoko, kuwezesha biashara, kutoa taarifa za biashara na ushauri kuhusu masuala ya sera za biashara. Katika jitihada za kuendeleza bidhaa za ngozi, TanTrade kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) Kampasi ya Mwanza iliratibu mafunzo ya uboreshaji wa ngozi katika hatua mbalimbali za mnyororo wa thamani kuanzia uchinjaji, uchunaji, usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za ndani. Mafunzo hayo yalifanyika Mkoani Kilimanjaro ambapo washiriki 51 wakiwemo wafanyabiashara, maafisa ugani wa Manispaa na Kata, wasimamizi wa machinjio, wasindikaji na watengenezaji wa bidhaa za ngozi walishiriki mafunzo hayo.

189. *Mheshimiwa Spika*, kulingana na takwimu za Shirika la Chakula Duniani (FAO), Tanzania huzalisha tani 34,000 za asali kwa mwaka ikiwa ni ya pili barani Afrika baada ya nchi ya Ethiopia. Uzalishaji wote ni asilimia 24.6 ya uwezo wake wa uzalishaji. Changamoto za sekta ya asali ni pamoja na uzalishaji wa asali yenye ubora, vifungashio na masoko ya uhakika. Ili kutatua changamoto hizo, TanTrade kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Chuo cha Nyuki Tabora, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO) na Taasisi ya *Singida Youth Entrepreneurs Consultancy and Cooperative Society* (SYECCOS) imeratibu mafunzo ya uzalishaji, usindikaji, ufungashaji na biashara ya asali kwa kuzingatia mahitaji ya soko ndani na nje ya nchi. Jumla ya wadau 197 kutoka mikoa ya Katavi, Singida na Tabora wamepewa mafunzo kwa vitendo kwa kutembelea na kutumia mitambo iliyopo SIDO- Singida, Chuo cha Nyuki Tabora na Shamba la Nyuki la Iyungi (Iyungi Bee Farm).

190. *Mheshimiwa Spika*, TanTrade iliandaa mafunzo ya ujasiriamali kuhusu ubora na ufungashaji wa bidhaa za viungo. Mafunzo yalitolewa kwa wazalishaji 202 waliowakilisha vikundi 45 vya wakulima na wafanyabiashara wa viungo kutoka Halmashauri za Wilaya za Morogoro Vijijini (Matombo), Mvomero (Nyandira) na Kilosa (Malolo). Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wazalishaji na wafanyabiashara wa viungo na malimbichi nchini kuongeza ubora wa bidhaa, kujua mbinu za namna ya kuongeza thamani na kutumia vifungashio sahihi ili kukidhi ushindani katika soko. Mathalani, mahitaji ya viungo katika soko la Ulaya ni wastani wa tani 750,000 kwa mwaka. TanTrade inahamasisha na kuunganisha wazalishaji wa viungo ili kuwezesha Tanzania kuuza wastani wa tani 100,000 kwa mazao ya pilipili manga, tangawizi kavu na mdalasini.

191. *Mheshimiwa Spika*, TanTrade iliandaa mafunzo ya mbinu za uzalishaji, ubora, ufungashaji na masoko kwa wasindikaji wa Mafuta ya Alizeti, Ufuta, Nazi na Mbogamboga Wilayani Ruangwa na Masasi. Mafunzo yalitolewa kwa watu 89 ambaao ni wawakilishi wa vikundi mbalimbali vya wasindikaji, wakulima na wafanyabiashara katika sekta hiyo ndogo. Mikoa ya Lindi na Mtwara huzalisha wastani wa tani 50,000 za ufuta na alizeti kwa mwaka. Hivyo mafunzo hayo yalilenga kuhamasisha uongezaji thamani mazao hayo ili kuongeza uzalishaji. Mahitaji ya ufuta na alizeti kwa soko la ndani ni mara mbili ya uwezo wa kuzalisha mazao hayo.

192. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendeleza soko la ndani na nje, TanTrade imefanya utafiti wa mazao ya ufuta na mbaazi ili kuweza kubaini hali halisi ya uzalishaji, ubora, vifungashio na matumizi ya vipimo sahihi. Utafiti ulisaidia kubaini bidhaa ambazo zinahitajika katika soko na kuendeleza masoko hayo kuititia mnyororo mzima wa thamani ili kuhamasisha uongezaji wa thamani katika mazao hayo. Kutokana na utafiti huo TanTrade imepanga kutoa mafunzo kwa wakulima katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kuratibu upatikanaji wa mbegu kwa vikundi vya wakulima ili kukidhi mahitaji ya masoko na kutathmini mifumo ya masoko ya ufuta ikiwa ni pamoja na kuondoa madalali ambaao ni kikwazo kikubwa kwa mkulima mdogo.

193. *Mheshimiwa Spika*, mwaka 2016 TanTrade iliratibu Maonesho ya 40 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) 2016 yaliyofanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl. Julius K. Nyerere, Barabara ya Kilwa kuanzia tarehe 28 Juni hadi tarehe 8 Julai, 2016. Jumla ya makampuni 2,500 yalishiriki katika Maonesho hayo, ukilinganisha na makampuni 2,302 yaliyoshiriki katika Maonesho ya 39 mwaka 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.6. Kati ya makampuni yaliyoshiriki, 501 ni washiriki kutoka nje ya nchi na 1,999 ni washiriki kutoka ndani zikiwemo Wizara sita (6) na Taasisi za Serikali thelathini na saba (37).

194. *Mheshimiwa Spika*, maonesho hayo yalishirikisha jumla ya nchi 30 za kigeni ambazo ni Afrika Kusini, Australia, Bulgaria, Brazil, China, Ghana, Ufaransa, India, Indonesia, Italia, Iran, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Malawi, Mauritius, Misri, Msumbiji, Pakistani, Singapore, Syria, Uganda, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Bulgaria, Rwanda, Sudani ya Kusini, Urusi na Vietnam. Ushiriki huu ni sawa na ongezeko la nchi tano ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo jumla ya nchi 25 zilishiriki. Ongezeko hilo lilitokana na jitihada za uhamasishaji Maonesho kuititia Balozi za Tanzania nje ya nchi na Balozi zinazowakilisha Nchi zao hapa Nchini.

195. *Mheshimiwa Spika*, TanTrade pia iliandaa mikutano baina ya wafanyabiashara "B2B" kuanzia tarehe 02 – 06 Julai, 2016 ambapo jumla ya wafanyabiashara wa ndani 200 na 15 kutoka nje ya nchi walikutana. Lengo kuu lilikuwa kuwaunganisha wazalishaji na wanunuzi mbalimbali katika sekta za ufugaji wa kuku, biashara ya maziwa, ufuta na asali; mbogamboga, matunda, alizeti na korosho. Katika mikutano huo, mikataba ya mauzo isiyofungani yenye thamani ya Shilingi. 320,000,000 ilisainiwa.

196. *Mheshimiwa Spika*, TanTrade iliandaa Maonesho ya Kwanza ya Viwanda vya Tanzania yaliyofanyika katika Uwanja wa Maonesho wa Mwalimu J. K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam kuanzia tarehe 7 – 11 Desemba, 2016. Maonesho hayo yalishirikisha jumla ya Taasisi 16 za Serikali zikiwemo Wizara na

Mashirika ya Umma; viwanda vikubwa na vya kati 80 na Taasisi 3 za Fedha. Katika Maonesho hayo, viwanda vidogo vipatavyo 340 vilishiriki chini ya uratibu wa Taasisi zinazowezesha Wajasiriamali. Taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

- (i) SIDO - Taasisi ya SIDO iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 80 katika Banda lililotengwa kwa ajili ya Viwanda vidogo vilivyopo chini ya SIDO;
- (ii) TALEPA - Taasisi ya TALEPA iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 23 wenye viwanda vya ngozi;
- (iii) TAFOPA - Taasisi ya TAFOPA iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 30 wenye viwanda vya usindikaji wa vyakula; na
- (iv) Kijani Kibichi - Taasisi ya Kijani Kibichi iliratibu ushiriki wa Wajasiriamali 200 wenye viwanda vidogo kwenye sekta za kilimo, maliasili, uvuvi, ufugaji na sanaa za mikono.

197. *Mheshimiwa Spika*, TanTrade ilishiriki katika Maonesho ya SIDO yaliyofanyika Mkoani Tabora kuanzia tarehe 7 hadi 12 Septemba, 2016, Maonesho ya Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika Mbeya kuanzia tarehe 27 Septemba hadi 3 Oktoba, 2016 pamoja na Maonesho ya Kanda ya Pwani yaliyofanyika Wilayani Bagamoyo kuanzia tarehe 26 Oktoba hadi 30 Oktoba 2016. Lengo kuu la ushiriki wa Mamlaka katika Maonesho hayo ni kutangaza huduma mbalimbali za TanTrade kwa wananchi. Aidha, TanTrade kuititia maonesho hayo ilifanya tathmini ya bidhaa zinazozalishwa na wajasirilamali wenye viwanda vidogo ili kubaini hatua za kuchukua kwa ajili ya kuendeleza bidhaa zao.

198. *Mheshimiwa Spika*, TanTrade ilisimamia Maonesho na semina ya ufugaji kuku na ndege "Tanzania Poultry Show" yaliyofanyika katika Hoteli ya *Blue Pearl* kuanzia tarehe 7 hadi 8 Oktoba, 2016. Maonesho hayo yaliandaliwa na Umoja wa Watotoleshaji wa Vifaranga vya Kuku na Ndege Wanaofugwa (TPBA) Tanzania "Poultry Breeders Association" ambayo yalitoa fursa na kuwakutanisha wadau mbalimbali katika kujenga na kutengeneza mtandao wa biashara.

4.3.11 Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala

199. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, makampuni 22 yalisajiliwa kutumia stakabadhi za ghala na ghala 28 zilitumika katika kuhifadhi mazao ya korosho, kahawa, mpunga na mahindi. Bodi ya Kusimamia Stakabadhi za Ghala kwa kushirikiana na wadau ilirejesha matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwa zao la korosho katika Wilaya ya Tunduru ambapo kilo 15,301,004 za korosho zimekusanywa na kuuzwa kupitia Mfumo katika msimu huu wa 2016/2017 ukilinganisha na kilo 7,394,705 zilizokusanywa na kuuzwa katika msimu wa 2011/2012 ambao ndio ulikuwa msimu wa mwisho kuuza kupitia Mfumo wa Stakabadhi. . Aidha, mafunzo kwa wadau wakuu wa mfumo yalitolewa kwa njia ya semina kwa kushirikiana na Taasisi za fedha za NMB PLC Ltd, CRDB PLC Ltd, Baraza la Nafaka la Afrika Mashariki (EAGC), Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi za Mazao.

200. *Mheshimiwa Spika*, kuundwa kwa Kamati za Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufuatia marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala Na. 10 ya mwaka 2005 yaliyofanyika mwaka 2015 kumeongeza ufanisi katika kusimamia mfumo wa stakabadhi za ghala msimu wa 2016/2017. Bei ya zao la korosho kwa wakulima imeongezeka hadi wastani wa Shilingi 3,400.00 kwa kilo ikilinganisha na Shilingi 2,350.00 kwa kilo msimu wa 2015/2016 ikiwa ni ongezeko la asilima 44.6. Usimamizi huo pia umeongeza kiwango cha korosho kilichokusanywa na kuuzwa kupitia mfumo wa stakabadhi kufikia tani 249,912.00 ukilinganisha na tani 155,244 zilizokusanywa msimu wa 2015/16. Aidha, ufanisi wa utendaji wa Waendesha Ghala umezidi kuimariika kwa kupungua kwa wastani wa upotevu kutoka 0.072% kwa msimu 2015/2016 hadi kufikia 0.0024% kwa msimu wa 2016/17.

201. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhamasisha uanzishwaji wa soko la bidhaa, Bodi ya Kusimamia Stakabadhi za Ghala kwa kushirikiana na Mamlaka ya Masoko na Mitaji (CMSA), imetoa

mafunzo kwa wadau wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Singida na Dodoma. Mafunzo hayo pia yalitolewa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kanda ya Kusini ambao walipatiwa mafunzo ya uanzishwaji wa soko la bidhaa. Aidha, Bodi kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia imeanzisha mfumo wa kieletroniki wa utoaji wa taarifa kati ya wadau ili kufanikisha uanzishwaji wa minada ya kieletroniki ya soko la bidhaa. Aidha, Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Greenwich na ufadhili wa Umoja wa Ulaya pamoja na *African Rural & Agricultural Credit Asociation (AFRACA)* Bodi iliandaa mafunzo ya Mfumo wa Stakabadhi kwa washiriki 25 kutoka nchi za Nigeria, Ghana, Zambia, Msumbiji na Kenya yalifanyika Mkoani Arusha.

4.3.12 Tume ya Ushindani

202. *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Ushindani ina jukumu muhimu la kulinda ustawi wa viwanda vya ndani kwa kuzuia bidhaa bandia kuingia katika soko la ndani. Wawekezaji katika viwanda wa ndani na wanaotoka nje ya nchi hufanya uwekezaji baada ya kujiridhisha kuwa bidhaa watakazozalisha zitalindwa na sera za ushindani wa haki. Hivyo, Tume ya Ushindani ni Taasisi muhimu katika maendeleo ya viwanda nchini. katika mwaka 2016/2017, Tume ya Ushindani imeendelea kulinda na kuendeleza ushindani katika soko. Jumla ya mashauri 25 ya mikataba ya miungano ya makampuni yamefanyiwa mapitio ili kubaini kama miungano hiyo inaweza kufifisha ushindani katika soko na uchumi kwa ujumla. Jumla ya malalamiko 22 yamefanyiwa uchunguzi, kati ya hayo malalamiko 20 yameamuliwa na uchunguzi unaendelea kwa malalamiko mawili. Aidha, katika kumlinda na kumtetea mlaji, malalamiko 15 ya walaji yamepokelewa, malalamiko 13 yametatuliwa kwa mlaji kurudishiwa fedha, kupatiwa bidhaa nyingine au kutengenezewa bidhaa. Malalamiko mawili yako kwenye majadiliano.

203. *Mheshimiwa Spika*, katika kushughulikia uondoaji wa mikataba inayomkandamiza mlaji anaponunua bidhaa au

huduma (standard form consumer contracts); kanuni zimeandaliwa na kuwekwa kwenye tovuti ya Tume. Notisi imeshatolewa kuwa, uwasilishaji wa mikataba hiyo kwa uhakiki umeanza tangu Januari, 2017. Uchunguzi wa awali pamoja na uandaaji wa notisi ya kesi moja inayohusu kuondolewa/ kutengenezwa kwa magari yaliyookuwa na hitilafu vimekamilika. Aidha, uchunguzi katika makampuni mawili ya magari kuhusu ubovu uliokwishesagundulika kimataifa unaoweza kuhatarisha maisha ya mtumiaji unaendelea.

204. *Mheshimiwa Spika*, katika kudhibiti bidhaa bandia, ukaguzi bandarini na bandari kavu (ICDs) Dar es Salaam uliwezesha kukamatwa kwa makontena 46 yaliyokuwa na bidhaa bandia. Wahusika waliadhibiwa kulingana na Sheria ya Alama za Bidhaa (merchandise Mark Act, 1963) kama ilivyorekebishwa na zoezi hilo ni endelevu. Vilevile, Tume ilifanya kaguzi 12 za kushtukiza katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Shinyanga na Dar es Salaam ambapo watuhumiwa 29 walikamatwa wakiuza bidhaa bandia kinyume na Sheria. Bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na nyembe, viatu, pombe kali, dawa za kung'arisha viatu, dawa za kuua waduu na simu za viganjani.

205. *Mheshimiwa Spika*, Tume inashirikiana na Wizara kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji. Andiko la kitaalamu (Concept Note) pamoja na Hadiduza Rejeazimeandaliwailikumtafuta Mshauri Mwelekezi kufanya utafiti na kuandaa Rasimu ya Sera hiyo. Aidha, marekebisho ya sheria ya ushindani ambayo yalisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza mwaka 2015 na kurejeshwa kwa mapitio zaidi yameandaliwa na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

4.3.13 Baraza la Ushindani

206. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2016/2017, Baraza limeendelea kusikiliza mashauri yatokanayo na mchakato wa ushindani wa biashara na udhibiti katika sekta za nishati na maji, usafirishaji na mawasiliano. Katika kipindi cha Julai, 2016

hadi Machi, 2017 Baraza lilikua na jumla ya kesi za rufaa 12 na maombi 26 na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa 38. Katika kipindi hicho, Baraza liliweza kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri 14 na mashauri 24 yanaendelea na yapo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Baraza linaendelea kupokea mashauri mapya na kusikiliza mashauri yaliyobaki. Aidha, Baraza limeendelea kuwapatia mafunzo watumishi wake katika jitihada za kuboresha utendaji wao na kuwaongezea weledi wa kushugulikia mashauri yanayowasilishwa katika Baraza. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya watendaji 8 waliwezeshwa kupata mafunzo hayo ndani ya nchi.

207. *Mheshimiwa Spika*, katika jitihada za kutangaza shughuli za Baraza kwa wadau wake, Baraza limeweza kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuititia Maonesho ya Kimataifa ya Kibashara ya Saba Saba pamoja na Maonesho ya Wakulima ya NaneNane yaliyofanyika Mkoani Lindi. Pia, Baraza limeweza kuendesha semina kwa Madiwani, Wenyevit wa Serikali za Mitaa na viongozi mbalimbali wa asasi za kiraia katika Mkoa wa Dodoma kwa nia ya kulitangaza Baraza kwa wadau wake. Aidha, Baraza limeweza kuendesha vipindi kwa njia ya redio, kufanya machapisho na semina mbalimbali kwenye mikoa kwa nia ya kujitangaza.

4.3.14 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni

208. *Mheshimiwa Spika*, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeendelea na kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau, chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212; Sheria ya Kusajili Majina ya Biashara Sura ya 213; Sheria ya Alama za Biashara na Huduma Sura ya 326; Sheria ya Hataza Sura ya 217 na Sheria ya Leseni za Viwanda Sura 46..

a) Usajili wa Majina ya Biashara

209. *Mheshimiwa Spika*, Wakala imejiandaa kutoa huduma kwa wananchi na wawekezaji wa ndani na wa nje kwa njia

ya kielektroniki na tayari huduma zifuatazo zinatolewa kwa njia ya mtandao: usajili wa Majina ya Biashara (Online Business Names Registration), mabadiliko ya baada ya usajili wa majina ya biashara (post registration activities for Business Names), upekuzi wa majina (Online Company Name clearance), kuomba taarifa mbali mbali za makampuni, majina ya biashara yaliyosajiliwa (official search for Companies and Business Names), na taarifa za alama za biashara. Hivi sasa wateja hawalazimiki kuandika barua na kufuata majibu katika ofisi za BRELA Dar es Salaam kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Aidha, malipo ya ada yanafanyika kwa njia ya mtandao Mobile NMB bank na CRDB Simbanking, Mpesa na Tigopesa au kupitia matawi ya Benki za CRDB na NMB popote Tanzania Bara.

b) Kupeleka huduma karibu na wananchi

210. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na kutoa huduma kwa njia ya mtandao kwa baadhi ya huduma zilizotajwa hapo juu, Wakala imefungua Ofisi Mtwara ambayo inahudumia mikoa ya Ruvuma na Lindi; Mjini Mbeya kwa ajili ya kuhudumia mikoa ya Iringa, Njombe, Katavi na Songwe; Mjini Mwanza kuhudumia mikoa ya Kagera, Mara, Geita, Simiyu na Shinyanga. Wakala inaendelea na taratibu za kufungua ofisi nyingine Dodoma na Mjini Arusha. Kufanikiwa kwa ufunguzi wa ofisi za kanda umechangiwa pia na juhudui kubwa za Wakuu wa Mikoa husika.

c) Kupunguza muda wa kuhudumia wateja

211. *Mheshimiwa Spika*, Wakala imeendelea kutekeleza mipango ya kupunguza muda wa kuwahudumia wananchi na hivi sasa cheti cha usajili wa majina ya biashara kinapatikana kwa saa 1-2, Usajili wa Kampuni unafanyika ndani ya siku 1-3 ikiwa mwombaji amewasilisha nyaraka zote zilizotimiza masharti ya kisheria. Aidha, Wakala imeweka bayana muda wa kuhudumia mteja kwenye tovuti pamoja na namba za simu na majina ya wakuu wa Idara na vitengo wanaohusika ikiwepo namba ya simu ya kiganjani ya Afisa Mtendaji Mkuu. Utaratibu huu umesaidia kupunguza malalamiko na kuondoa kero mbali mbali kwa kusaidia wananchi wengi wanaotaka maelezo

d) Kutoa huduma za BRELA kwa njia ya mtandao

212. *Mheshimiwa Spika*, BRELA iliingia mkataba na Kampuni ya Norway Registers Development AS (NRD) ya Norway tarehe 28 Agosti, 2016 kwa ajili ya kujenga mfumo mpana wa kutoa huduma zote za Wakala kwa njia ya Mtandao. Mfumo huu, utaunganishwa na taasisi nyingine kama vile Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, OR-TAMISEMI (leseni za Biashara) Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, TRA, NIDA, RITA, TIC, TCRA, Uhamiaji, PPRA, SSRA na Taasisi nyingine za udhibiti zitakazokuwa tayari kuunganishwa na mfumo huu. Hivyo, mfumo huo unategemewa kutoa huduma kwa kielektroniki kwa pamoja (Electronic One Stop Shop) ili kupunguza na kuondoa urasimu katika kuanzisha biashara. Aidha, mkakati huu utaboresha nafasi ya nchi yetu kwenye viwango vya ufanyaji biashara duniani (Doing Business Ranking) na hususan uanzishwaji wa Biashara (starting business ranking) na hivyo kuvutia wawekezaji wa nje.

e) Uhamasishaji wa usajili na urasimishaji wa Biashara

213. *Mheshimiwa Spika*, Wakala imetoa elimu ya usajili na kuhamasisha umuhimu wa kurasimisha biashara kwa njia mbali mbali ikiwemo vipindi/onyesho fupi kwenye runinga kwa kuitia TBC, ITV na Clouds TV, sambamba na vipindi vya radio na TV. Pia, Wakala imeshiriki maonesho ya Nanenane na Sabasaba na kutoa vipeperushi na majarida mbali mbali yanayoonyesha taratibu za usajili na gharama zake. Vilevile, Wakala imeanzisha utaratibu mpya wa kuelimisha umma juu ya umuhimu wa usajili na urasimishaji wa biashara katika ngazi za Wilaya na Tarafa kwa kutumia vyombo vya habari na kutoa huduma za usajili papo kwa hapo. Elimu na uhamasishaji huo umefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Songea, Njombe, Arusha, Tanga, Mwanza, Mara, Geita, Simiyu, Shinyanga, Songwe na Rukwa.

f) Shughuli za Usajili

214. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa shughuli za usajili tangu kuanzishwa rasmi kwa Wakala hadi Marchi 2017

jumla ya Makampuni 134,187 yalikuwa yamesajiliwa; Majina ya Biashara 428,576 yamekwisha sajiliwa, alama za biashara na huduma 55,418 na hataza 624 zimekwisha tolewa na leseni 6,606 za viwanda zimetolewa. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 wakala ilisajili Makampuni 6,014, Majina ya Biashara 14,066, Usajili alama za Biashara na Huduma 2,544, Usajili Leseni za Biashara 105 na Hataza 15. Kutokana na jitihada za uhamasishaji katika kipindi cha 2016/2017 idadi ya usajili imeongezeka ukilinganisha na mwaka 2015/2016.

4.3.15 Wakala wa Vipimo

215. *Mheshimiwa Spika*, Wakala wa Vipimo imeendelea kutekeleza majukumu yake ya usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini ambapo hadi kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2016/2017, vipimo 453,524 vilihakikiwa na vipimo 12,459 vilirekebishwa. Wakala pia imeimarisha ukaguzi wa bidhaa zote zilizofungashwa katika mipaka ya Nchi, Mikoa na Wilaya. Wakala imendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia Maonesho ya Sabasaba na Maonesho ya NaneNane yaliyofanyika kitaifa mkoani Lindi. Aidha, Wakala kupitia vyombo mbalimbali vyta habari kama vile luninga, redio na mitandao ya kijamii imeendelea kutoa elimu kuhusu ufungashaji na matumizi ya vipimo sahihi.

216. *Mheshimiwa Spika*, Wakala wa Vipimo imeendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi sahihi ya vipimo katika maeneo yaliyohusu ufungashaji batili maarufu kama ‘lumbesa’. Pamoja na matakwa ya kisheria, Wakala imetekeliza jukumu hili kwa mafanikio kwa kuzingatia ushauri wa waheshimiwa wabunge na maagizo ya Mhe. Waziri Mkuu. Kutokana na ukaguzi kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi, 2017, kaguzi 6,249 zilifanywa na kukuta wakosaji 4,620 (74%) ambaao wote walitozwa faini ya jumla ya Shilingi 639,144,000. Jitihada za ukaguzi wa mizani ikiwemo uelimishaji wa wadau ulichangia kwa kiasi kikubwa wakulima kupata malipo stahiki kwa mazao ya pamba na korosho kwa msimu huu.

217. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa udhibiti wa udanganyifu na wizi kupitia mizani wakati wa ununuzi wa zao la pamba; Wizara kupitia Wakala wa Vipimo ilifanya ukaguzi wa mizani ya kununulia pamba kabla na wakati wa msimu wa ununuzi ili kubaini udanganyifu unaofanywa na wanunuzi. Ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa ya Tabora, Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga, Simiyu na Geita. Timu ya wakaguzi ilizifikia wilaya 21 za mikoa hiyo, kufanya uhakiki wa mizani pamoja na kutoa Elimu kwa wadau katika maeneo hayo hususani wakulima wa zao la Pamba. Katika ukaguzi huo mizani 668 ilikaguliwa, kati ya hiyo mizani 640 ilikuwa ikipima kwa usahihi ambayo ni sawa na asilimia 96.8 ya mizani yote iliyokaguliwa, mizani 28 ilichezewa kwa makusudi ambayo ni asilimia 4.2. Jumla ya kesi 29 zilifunguliwa mahakamani, kati ya hizo watuhumiwa 19 walitozwa faini na mahakama kwa makosa waliyofanya. Watuhumiwa 3 walihukumiwa vifungo na mizani 8 ilitaifishwa mahakamani. Kesi ambazo zinaendelea mahakamani zipo 7. Aidha, elimu iliyotolewa kwa wakulima imewafanya wao wenyewe kuwa walinzi na kuzuia mizani kuchezewa na hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya kudhibiti udanganyifu kwa wakulima wanapouza pamba.

218. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na elimu kabla na baada ya msimu wa ununuzi kuanza, wakosaji wote kufikishwa mahakamani na sio kutumia utaratibu wa kuwafilisha (compounding) na kutozwa faini na mkaguzi wa vipimo kwa mujibu wa sheria ya Vipimo sura na. 340 iliyofanyiwa mapitio 2002 uliokuwa ukitumika miaka ya nyuma angweza kufilishwa Uamuzi wa kuwapeleka mahamani ilikuwa ni mbinu za kiutendaji kukabiliana na adhabu ndogo/faini zilizokuwa zikitozwa na hivyo kutoshawishi kuacha kufanya makosa kwa makusudi. Ukaguzi huo umeonekana kurudisha ari ya wakulima kulima pamba kwa wingi msimu ujao. Aidha, wakulima wengi waliuza pamba safi isiyochanganywa na mchanga au maji kutokana na wakulima kulipwa kulingana na uzito halisi wa pamba yao.

219. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo ilifanya ukaguzi maalum wa mizani itumikayo katika ununuzi wake ni zao la korosho kwa mikoa ya Mtwara na Ruvuma, ambapo wilaya za Tandahimba, Mtwara vijiji, Newala na Tunduru zilifikiwa.

Uhakiki huo ulikwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wakulima na wanaushirika wa Vyama vya Msingi. Ugaguzi huo ulifanyika kwa Vyama vya Msingi 271 na kuhakiki mizani 900 ambapo mizani 575 (64%) ilikuwa sahihi na mizani 325 (36%) zilikatazwa kutumika. Elimu iliyotolewa na wakulima kuweza kushuhudia uhakiki wa mizani ya kununulia korosho umesaidia wakulima wengi kuacha kuuza korosho kwa kutumia vipimo batili maarufu ‘kangomba’. Hali hii imepunguza kwa kiasi kikubwa wanunuzi “vishoka” kwenda kuwarubuni wakulima. Hivyo wakulima wengi walihamasika kuuza korosho katika Vyama vya Msingi na kunufaika na bei nzuri iliyopangwa na Serikali, kwani mazao yao yalipimwa na kulipwa kwa haki sawa na jasho lao. Hali hiyo imewatia moyo wakulima na kuhamasika kuongeza uzalishaji zaidi wa zao hilo.

220. *Mheshimiwa Spika*, Wakala wa Vipimo pia iliendelea kufanya uhakiki wa mizani inayotumika kununulia ufuta wakati wa msimu. Uhakiki ulifanyaika katika mkoa wa Lindi katika Wilaya za Lindi Vijiji, Kilwa na Ruangwa ambapo ilifanikiwa kuvifikia vijiji 24 na vyama vya msingi nane. Mizani 72 zilihakikiwa na mizani 8 (11%) zilipitishwa wakati mizani 64 (89%) zilikataliwa. Wakosaji wote walitozwa faini, Mizani zote zisizoruhusiwa kwa matumizi ya biashara zilizuiwa na Wanunuzi walipewa ushauri kuhusu mizani inayotakiwa kutumika katika biashara. Wakati ugaguzi wa mizani ukiendelea elimu ilitolewa kwa wakulima na wanunuzi wa ufuta kuhusu matumizi sahihi ya vipimo.

221. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo imeendelea kuongeza juhudini katika ugaguzi wa vituo vya kuuzia gesi ya majumbani (LPG). Ugaguzi umefanyika katika *Gas plant* zinazopokea na kufungasha gesi, vituo vya kuuzia gesi vya jumla na rejareja ili kuwalinda walaji na udanganyifu katika uzito wa mitungi ya gesi. Aidha, katika kudhibiti udanganyifu huo, Wizara imechukua hatua zifuatazo;

- (i) Kuitisha mikutano na wadau katika sekta ya gesi hususan wafungashaji ili kuwakumbusha kuzingatia uzito sahihi wakati wa ufungashaji, kusisitiza matumizi ya *seal*

zinazowezesha kuzuia refilling inayofanywa na baadhi ya wauzaji wa jumla wasio waaminifu;

- (ii) Ukaguzi katika Makampuni yanayofungasha gas ili kuhakiki mifumo ya ujazaji gesi na mizani inayotumika. (Gas plant) Oryx, Mihan, Cam Gas, Lake Gas, Alpha Gas, Manji's O Gas), na
- (iii) Ukaguzi wa kushitukiza kwa wauzaji wa jumla na rejareja lengo kuu lilikuwa kwanza ni kuhakikisha kila kituo kinachouza gesi kinakuwa na mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2016 mpaka Februari, 2017.

222. *Mheshimiwa Spika*, Wakala imefanya ukaguzi kwa wauzaji wa jumla na rejareja kwa vituo 1,038 ambapo vituo 715 (69%) vilikuwa na mizani na vituo 323 (31%) havikuwa na mizani. Kutohana na mapungufu yaliyobainika, wahusika walipewa elimu kuhusu matumizi sahihi ya vipimo na kwa wasio na mizani walipewa muda wa kuhakikisha wanunu mizani na ukaguzi na ufuatiliaji unaendelea. Aidha, Wakala iliendelea kutoa elimu kwa wadau ili kuhakikisha mlaji anapata uzito stahiki wa gesi.

223. *Mheshimiwa Spika*, Wakala imeendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa katika viwanda vya ndani ya nchi, mipakani na bandarini na kutoa elimu ya ufungashaji kwa wadau. Ukaguzi umeimarishwa kwa bidhaa zote zilizofungashwa kutoka nje ya nchi kupitia katika mipaka ya Namanga mkoani Arusha, Horohoro - Tanga, Holili - Kilimanjaro, Sirali -Mara, Mtukura- Kagera, Kasumuru Mbeya na Bandari ya Dar es salaam. Ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kupitia Bandarini na Mipakani, umefanikishwa kiasi kikubwa kwa kutumia Mfumo wa TANCIS wa Mamlaka ya Mapato (TRA). Mfumo huu umewezesha kupokea taarifa za bidhaa zote zinazoingia nchini kupitia mipakani na bandari ya Dar es Salaam.

4.3.16 Kituo cha Uwekezaji Tanzania

a) Usajili, Umiliki na Mgawanyo wa Miradi ya Uwekezaji

224. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Kituo kilifanikiwa kusajili jumla ya miradi 242 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 2,079 inayotarajiwa kutoa ajira mpya zipatazo 17,385. Sekta ilioongoza kwa idadi ya usajili wa miradi ni uzalishaji/usindikaji viwandani, ikifuatiwa na sekta ya majengo ya biashara, utalii, na usafirishaji. Sekta zinazotarajiwa kutoa ajira kwa wingi zaidi ni sekta ya uzalishaji viwandani, ikifuatiwa na sekta ya majengo ya biashara, usafirishaji na sekta ya utalii. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa katika kipindi hicho, wawekezaji wageni waliongoza kwa kusajili miradi 105, sawa na asilimia 43 ya miradi yote; wakati miradi ya ubia kati ya Watanzania na wageni ni 76 sawa na asilimia 32, miradi 61 iliyobaki sawa na asilimia 25 inamilikiwa na watanzania. Aidha, katika kipindi hicho, Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kusajili miradi 119, sawa na asilimia 49 ya miradi yote ilioandikishwa. Mkoa wa Arusha ulifuatia kwa kusajili miradi 30 (sawa na asilimia 12), na kufuatiwa na Mkoa wa Pwani ukiwa na miradi 26 (sawa na asilimia 11). Mkoa wa Mwanza ulikuwa na miradi 19 (sawa na asilimia 8), na mikoa iliyobaki kila mmoja ilisajili chini ya miradi 10. Nchi kumi zinazoongoza kwa uwekezaji nchini katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ni China, ikifuatiwa na India, Kenya, Uingereza, Mauritius, Oman, Falme za Kiarabu (U.A.E), Canada na Marekani.

b) Huduma kwa Wawekezaji

225. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Kituo kimeimarisha mfumo wake wa utoaji wa Huduma za Mahala Pamoja za Kuhudumia Wawekezaji (One Stop Centre), na pia kufanya maboresho ya mfumo huo. Katika kuendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani, Kituo kipo katika hatua za mwisho za kukamilisha utaratibu wa utoaji huduma zake kupitia njia ya mtandao ili kuwawezesha wawekezaji popote pale walipo duniani waweze kuwasilisha maombi yao ya vibali na leseni mbalimbali.

Huduma hiyo ya utoaji leseni na vibali inatekelezwa kuitia mradi wa *Tanzania Investment Window* (TIW) ambao unalenga kuweka mtandao wa ushirikiano wa mifumo ya usajili, leseni na vibali mbalimbali kuitia wadau hususan usajili wa ardhi (Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi), usajili wa makampuni (BRELA), utoaji vivutio na ulipaji kodi (TRA), utoaji vibali vya kazi (Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Walemvu) na utoaji vibali vya ukaazi (Uhamiaji). Baada ya kukamilika kwa mradi huo, huduma zote zikiwepo za utoaji Cheti cha Uwekezaji, Uhamiaji, Vibali vya Kazi, Upatikanaji wa Ardhi na Kufungua Kampuni zitazotolewa kwa mfumo wa mtandao (online registration).

c) Huduma Zilizotolewa kwa Wawekezaji

226. *Mheshimiwa Spika*, katika kuitikia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa kupanua Huduma za Mahala Pamoja (One Stop Centre), Kituo cha Uwekezaji kimefanya ukarabati wa jengo linalotumika hivi sasa ili kuongeza ufanisi ikiwa ni pamoja na kuongeza Idara nyingine za Serikali ambazo zinahusika katika kutoa vibali na leseni. Taasisi zilizoongezwa ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Baraza la Mazingira (NEMC) na Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Ujenzi (AQRB). Kitengo hicho kilifunguliwa rasmi mwezi Oktoba, 2016.

227. *Mheshimiwa Spika*, kitengo cha Leseni za Biashara kilifanikiwa kushughulikia masuala 244 yanayohusu leseni ambapo leseni za biashara 71 zilitolewa. Kitengo cha Kazi kilifanikiwa kutoa jumla ya vibali 3,117 vya daraja A kwa ajili ya wamiliki wa makampuni (wenye hisa) na daraja B kwa ajili ya wafanyakazi. Idara ya Uhamiaji ilitoa Hati za Ukaazi daraja A zipatazo 283 na daraja B zipatazo 2,295. Kitengo cha TRA kilifanikiwa kuhudumia jumla ya wateja 1,311 kwa kuwapatia huduma za ushauri wa masuala yanayohusu kodi kama vile usajili wa Namba ya Mlipa Kodi, aina za kodi zinazotakiwa kulipwa na wawekezaji.

228. *Mheshimiwa Spika*, kitengo cha Ardhi kiliendelea kutoa huduma za ushauri kwa wawekezaji katika masuala mbalimbali ya ardhi pamoja na kuainisha maeneo yenye ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Kitengo kilifanikiwa kutoa Hati Zisizo Asili (Derivative title) 28 kwa wawekezaji. Pia Ofisi za Kanda zimeshirikiana na viongozi wa mikoa husika katika kutafuta na kutenga maeneo mahususi kwa ajili ya uwekezaji kwenye mikoa yao. Tayari Kituo kimeanza kuandaa taarifa mahususi kuhusu miundombinu ya maji, umeme, barabara na reli kwenye maeneo husika kwa ajili ya kilimo cha miwa na uanzishwaji wa viwanda nya sukari.

d) Miradi ya Uwekezaji

229. *Mheshimiwa Spika*, kituo kimeendelea kuvutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya maombi sita mapya ya miradi ya uwekezaji mahiri yalisajiliwa na kufanyiwa kazi ili kuwasilishwa katika Kamati ya Taifa ya Uwekezaji Rasilimali (NISC) kwa maamuzi. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Kusindika Matunda wa *Sayona Fruits*, Mradi wa Kuzalisha Vigae (ceramic tiles) wa *Goodwill Ceramics*, Mradi wa Hospitali wa *Pan African Multispeciality Health Centre*, Mradi wa Kusindika Gesi ya LPG wa *Mihan Gas*, Mradi wa Kuzalisha Vigae wa *Twyford* na Mradi wa Kiwanda cha Saruji wa *Hengya Cement*. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa pamoja itagharimu Dola la Kimarekani bilioni 2.68 na itazalisha jumla ya ajira za moja kwa moja 13,885 na zaidi ya ajira 38,520 zisizo za moja kwa moja. Miradi mitano kati ya sita tayari iko katika hatua za ujenzi.

e) Elimu kuhusu Uwekezaji

230. *Mheshimiwa Spika*, kituo kimeendelea kutekeleza Mkakati wa Mahusiano na Elimu kwa Umma kwa kutoa elimu kuititia redio, televisheni, mtandao na makala mbalimbali kwenye magazeti yetu ya ndani ili kuelimisha jamii kuhusu faida za uwekezaji na kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya Watanzania inafikiwa. Mkakati huo umelenga kuongeza ushirikiano kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii ili kuondoa dhana hasi kuhusu uwekezaji zinazotokana na

uelewa duni juu ya manufaa ya uwekezaji. Pia, Kituo kililenga katika kuelimisha wawekezaji wa ndani kujisajili na Kituo ili kupatiwa huduma mbalimbali zinazotolewa kituoni. Katika utoaji wa elimu, Kituo kimejikita katika kuwaelimisha wawekezaji wa ndani na wa nje kufuata Sheria na taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na kulipa kodi kwa wakati.

f) Uhamasishaji Uwekezaji

231. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Kituo cha Uwekezaji kiliratibu ushiriki katika makongamano ya uwekezaji katika nchi za China, Israeli, Kenya, Mauritius na Misri. Makongamano hayo yalihudhuriwa na zaidi ya wafanyabiashara 420 kutoka nchi mbalimbali. Ushiriki katika makongamano hayo ulitupatia fursa ya kutoa taarifa mbalimbali zenye lengo la kuhamasisha uwekezaji nchini ikiwemo mada juu ya hali ya uchumi, fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini, mazingira ya uwekezaji na vivutio vinavyotolewa kwa wawekezaji. Makongamano hayo yalitoa nafasi ya kufanyika kwa mikutano baina ya wafanyabiashara na kati ya wafanyabiashara na Serikali. Pia Kituo kiliweza kushiriki katika Maonesho ya Uwekezaji Afrika (Africa Investment Forum) yaliyofanyika nchini Rwanda.

232. *Mheshimiwa Spika*, Kituo cha Uwekezaji kilishiriki katika maandalizi ya ushiriki wa Tanzania katika makongamano na mikutano ya uwekezaji na kupokea ujumbe wa wafanyabiashara kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Afrika ya Kusini, China, Ethiopia, Finland, India, Japan, Korea ya Kusini, Mauritius, Marekani, Misri, Morocco, Oman, Singapore, Ubelgiji, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Urusi, Uturuki na Zimbabwe. Aidha, kituo kilihamasisha uwekezaji wa ndani ya nchi uliohusisha zaidi ya washiriki 700 wengi wao wakiwa ni wafanyabiashara. Makongamano hayo yalihuisha washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi na yalilenga kukutana na wafanyabiashara na kuwapatia taarifa muhimu kuhusu masuala ya uwekezaji na pia kuwawezesha kuzitambua na kuchangamkia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali hapa nchini. Vilevile kituo kwa kushirikiana na Ofisi za

Mikoa na Wilaya, Kituo kilihamasisha uwekezaji kwa kuandaa na kuibua fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo hayo na kuzitangaza kwa wawekezaji wa ndani na wa nje.

233. *Mheshimiwa Spika*, kituo kimekuwa kikishiriki kila mwaka katika maonesho mbalimbali ya kitaifa kama vile Sabasaba, na Nanenane ikiwa na lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma zitolewazo na Kituo, faida za kituo kwa wawekezaji hasa wananchi, kutoa elimu ya uwekezaji, fursa za uwekezaji zilizopo katika maeneo husika na vivutio vitolewavyo kupitia Kituo kwa wawekezaji. Aidha, Kituo kiliweza kushiriki katika Maonesho ya Nanenane katika Kanda za Kusini (Lindi), Kaskazini (Arusha) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) pamoja na Maonesho ya Sabasaba, SIDO na Maonesho ya Viwanda ya Tanzania ambapo wananchi wengi waliweza kutembelea banda la Kituo na kupata elimu hiyo.

4.3.17 Chuo cha Elimu ya Biashara

234. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) ilipanga kujenga na kuboresha miundombinu ya Chuo katika Kampasi za Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya; kuongeza uwezo wa wahadhiri katika mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu; na kupitia upya mitaala yote ili kuendana na uhitaji wa soko la ajira. Katika kukabiliana na uhaba wa miundombinu, Chuo cha Elimu ya Biashara tunatekeleza mradi wa kuongeza ghorofa tatu (Vertical Extension) katika jengo la sasa la “Cafeteria” kwa ajili ya maktaba mpya, madarasa, ofisi pamoja na kumbi za mihadhara kwa Kampasi ya Dar es Salaam.

235. *Mheshimiwa Spika*, katika juhudhi hizo Chuo kilinunua eneo lote lenye ekari 10.9 la shule ya sekondari iliyokuwa inaitwa *Hill Crest* kule Nyasaka, Mwanza. Ukarabati wa majengo na kuongeza miundo mbimu umeenza ili kuendeleza kampasi ya Mwanza. Chuo pia kimekamilisha kazi ya kuandaa Mpango Kabambe wa eneo lenye ukubwa wa ekari 54.9 lililopo Iganzo jijini Mbeya kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya Mbeya. Juhudi hizo zinatoa nafasi kubwa

ya kusogeza huduma ya elimu ya biashara kwa wananchi walio wengi. Kwa ujumla wake, kumekuwa na mabadiliko chanya katika kuboresha miundo mbinu kwa mwaka 2016/2017. Mabadiliko hayo yamejikita katika kuboresha miundo mbinu ya madarasa, kumbi za mihadhara, hosteli, na ofisi za waalimu katika kampasi za Dar es Salaam na Dodoma. Kuboreshwa kwa miundo mbinu pamoja na ujenzi wa Kampasi za Mwanza, Mbeya na Zanzibar kutakiwezesha Chuo kukidhi mahitaji yake ikiwa ni pamoja na kuwa na mazingira wezeshi katika kutoa huduma zake za kufundisha, utafiti pamoja na ushauri elekezi.

236. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Elimu ya Biashara imeendelea kuimarisha uwezo wa wahadhiri wake ambapo katika kipindi cha mwaka 2016/2017, jumla ya watumishi saba, (6 mafunzo ya Shahada ya Uzamili na 1 mafunzo ya Shahada ya Uzamivu) wamehitimu mafunzo yao na sasa wanalitumikia Taifa kwa kutumia elimu na ujuzi wao katika kufundisha. Aidha, watumishi 52 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali na Wahisani.

Watumishi wa CBE waliopo katika mafunzo ya muda mrefu

Na.	Ngazi ya Elimu ya Mafunzo	Idadi	Me	Ke	Ndani ya Nchi	Nje ya Nchi
1	Shahada ya Uzamivu (Ph.D)	27	21	6	14	13
2	Shahada ya Uzamili (Masters Degree)	21	19	2	16	5
3	Shahada ya Awali	2	0	2	2	0
4	Stashahada (Diploma)	2	0	2	2	0
	Jumla	52	40	12	34	18

**Ufunguo: Me - Wanaume
Ke - Wanawake**

Chanzo: CBE, 2017

237. *Mheshimiwa Spika*, Chuo kupitia watumishi wake kimefanya tafiti na kutoa machapisho ya jumla ya tafiti 36, kati ya hizo 34 zimechapishwa ndani na mbili nje ya chuo. Machapisho hayo yanayolenga kuisaidia jamii na Taifa kwa ujumla kujikwamua kutoka kwenye changamoto mbalimbali zinazotukabili. Baadhi ya chapisho hizo ni:

- i) *Adoption of Bus Rapid Transit (BRT) as a Solution in Combating Traffic Congestion and Fostering Economic Development in Africa;*
- ii) *Enhancing Access and Usage of Agricultural Information Towards Poverty Eradication and Environmental Degradation in Muleba and Misenyi in Kagera, Tanzania;*
- iii) *Stigmatization Among Female Students in Science Related Courses in TVETS in Tanzania;*
- iv) *Role of the College of Business Education (CBE) In The Fast Growing Business in The Energy and Mineral Sector in Tanzania; na*
- v) *Improving Public Service Delivery in Tanzania through Kaizen: A Review of Empirical Evidence.*

238. *Mheshimiwa Spika*, katika kutimiza azma ya Serikali na kufuata Diraya Maendeleo ya Taifa 2025 na Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo 2016/17 – 2020/2021 unaolenga kuifanya Tanzania kuwa na Uchumi wa kati kupitia ukuaji wa viwanda, Chuo kimepitia upya na kuifanya marekebisho mitaala yake yote ili kuendana na uhitaji wa soko. Sambamba na hilo Chuo kimekamilisha uanzishwaji wa shahada mbili ya Uzamili kwa mwaka 2016/2017 ambazo ni “Master in International Business Management” na “Masters in International Supply Chain Management” ambazo zinatarajiwaa kuanza rasmi mwaka wa masomo 2017/2018 mara idhini itakapopatikana kutoka NACTE. Aidha, Chuo kimeanzisha shahada za uzamili kwenye TEHAMA na Maendeleo (ICT for Development) na TEHAMA katika Usimamizi Miradi (IT- Project Management) kwa

kushirikiana na Chuo Kikuu cha Stockholm cha nchini Sweden. Kozi zimeanza rasmi mwaka 2016/2017.

239. *Mheshimiwa Spika*, Chuo cha Elimu ya Biashara kimeendelea kuleta chachu ya maendeleo nchini kwa kutoa idadi kubwa ya wataalamu katika nyanja mbalimbali za biashara na viwanda kwa ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya wanafunzi 3,118 walihitimu katika fani mbalimbali.

Idadi ya Wanafunzi waliohitimu Mwaka 2016 katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)

Na.	Ngazi ya Elimu	Me	Ke	Jumla
1	Astashahada	474	489	963
2	Stashahada	607	599	1206
3	Shahada	445	491	936
4	Stashahada za Uzamili	11	2	13
	Jumla Kuu	1,537	1,581	3,118

240. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia ubora wa Chuo cha Elimu ya Biashara kwa kuhakikisha kuwa kinazingatia viwango na vigezo vilivyowekwa na mamlaka za kusimamia elimu nchini ikiwemo NACTE na TCU. Kutokana na usimamizi huo na kwa ushirikiano mkubwa na uongozi wa Chuo, CBE imefanikiwa kushinda tuzo ya ubora ya Mwaka (College of the Year) ya mwaka 2016 katika mashindano yanayoandaliwa na “Tanzania Leadership Award.”

241. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara katika mwaka 2016/2017 imeendelea na mikakati ya kukiwezesha Chuo kuwa kituo cha Ubora (Centre for Excellence) katika kutoa wataalamu wa fani ya Sayansi ya Vipimo katika Viwanda (Legal and Industrial Metrology) katika Ukanda wa Nchi za Kusini mwa Afrika – SADC. Katika kutekeleza hilo, Chuo kimeendelea

kuboresha maabara zake kwa kuongeza vifaa mbalimbali na kuboresha miundombinu na vitendea kazi katika majengo yanayotumika kutolea elimu hiyo. Vilevile, Serikali imeendelea kusomesha wahadhiri katika ngazi ya shahada ya uzamivu (PhD) katika nchi ya Urusi na ndani ya nchi. Hadi sasa jumla ya wahadhiri watano wako masomoni, kati yao wahadhiri wanne (akiwemo mwanamke 1) wako nchini Urusi na Mhadhiri mmoja yupo nchini katika mafunzo hayo.

242. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara iliweza kufanya tafiti kubwa za kibiashara, kiuchumi na kijamii kufuatia hatua ya Serikali ya awamu ya tano kuhamia Dodoma. Kufuatia tafiti hizo, Chuo cha Elimu ya Biashara kiliandaa kongamano kubwa la kitaaluma lililoshirikisha wadau mbalimbali kwa lengo la kuibua na kujadili zaidi juu ya fursa zinazopatikana katika mkoa wa Dodoma.

4.4 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA UTOAJI WA HUDUMA

a) Ajira za Watumishi

243. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa Ikama ya mwaka 2016/2017 iliyoidhinishwa, Wizara ilikuwa na jumla ya watumishi 256 ambapo wanawake walikuwa 102 sawa na asilimia 40 na wanaume 154 sawa na asilimia 60. Kwa taarifa ya hadi mwezi Machi, 2017, Wizara ina jumla ya Watumishi 249, kati ya hao Viongozi ni 4, Wachumi ni 50, Watakwimu 14, Wahandisi 5, Maafisa Tawala 7, Maafisa Utumishi 5, Maafisa Sheria 4, Maafisa TEHAMA 5, Maafisa Ugavi 6, Maafisa Biashara 68, Maafisa Habari 2, Wakaguzi wa Ndani 6, Wahasibu 18, Wasaidizi wa Maktaba 2, Wasaidizi wa Kumbukumbu 12, Wapokezi 3, Fundi Sanifu 2, Makatibu Mahsus 17, Wasaidizi wa Ofisi 6 pamoja na Madereva 13. Hata hivyo, Wizara haikuweza kuajiri wala kupandisha vyeo watumishi kwa mwaka 2016/2017 kwa kuwa, Serikali iliahirisha utekelezaji wa utoaji ajira mpya, ajira mbadala pamoja na masuala yote yanayohusisha marekebisho ya mishahara yanayotokana na upandishwaji vyeo kwa watumishi hadi maelekezo yatakapotolewa.

b) Mafunzo

244. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara iliandaa Mpango wa Mafunzo wa muda wa mwaka mmoja ili kujenga uwezo kwa rasilimali watu na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Wizara ilipanga kuwapeleka watumishi kumi na sita (16) katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi kumi na nane (18) katika mafunzo ya muda mfupi. Hadi kufikia Aprili, 2017, Wizara imekwisha peleka watumishi nane (8) katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi (28) katika mafunzo ya muda mfupi, ndani na nje ya nchi.

c) Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi

245. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2016/2017, Wizara imehakikisha kuwa watumishi wote wanasantini mikataba yao ya kazi kwa wakati ili kutekeleza programu ya kuboresha utumishi wa umma na kuimarisha utendaji unaojali matokeo na uwajibikaji katika utumishi wa umma. Kwa kuzingatia hayo, jumla ya watumishi 248 kati ya 256 wamesantini mikataba ya kazi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA) na kufanya mapitio ya nusu mwaka mwezi Desemba, 2016 na wasimamizi wao. Watumishi nane (8) hawakuweza kusaini mikataba yao kwa kuwa wapo mafunzioni. Aidha, inatarajiwa kufikia mwisho wa mwezi Juni, 2017 kila mtumishi atafanyiwa tathmini ya utendaji wake wa kazi kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kutumia utaratibu huo wa MWAMTUKA.

d) Michezo na Afya za Watumishi

246. *Mheshimiwa Spika*, katika dhana ya michezo kwa afya, furaha na ufanisi kazini, kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeshiriki katika mabonanza mawili (2) yaliyohusisha washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma. Lengo la kushiriki michezo hiyo ilikuwa ni kujenga afya za watumishi kuititia mazoezi na michezo. Aidha, kufuatia agizo la Serikali kwa watumishi kufanya mazoezi jumamosi ya pili kila mwezi, Wizara imewahimiza watumishi kujenga tabia ya kufanya mazoezi ili kuimarisha afya zao na kujikinga

na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) yanayoweza kuepukika kama vile, uzito uliopitiliza, shinikizo la damu na kisukari.

e) Baraza la Wafanyakazi

247. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuwashirikisha watumishi katika vikao vya maamuzi kupitia Baraza la Wafanyakazi ili waweze kutetea maslahi yao. Kwa mwaka 2016/2017, Wizara imefanya kikao kimoja tarehe 24 Machi, 2017 ambapo Baraza la Wafanyakazi lilipitia, kushauri na kuridhia mapendekezo ya Wizara kuhusu Mipango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2017/2018.

f) Kuhamia Makao Makuu Dodoma

248. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia Agizo la Serikali la kuhamishia shughuli zake Makao Makuu ya Nchi Dodoma, Wizara imepanga kuhamisha watumishi wake katika awamu nne: Awamu ya kwanza Watumishi 43, awamu ya pili Watumishi 58, awamu ya tatu watumishi 81 na Awamu ya nne watumishi 67. Aidha, kila awamu inahusisha kuhamisha vifaa na mifumo ya utendaji ikiwemo Mifumo ya Mitandao ya Kompyuta. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Wizara imekwishahamisha watumishi 43 wakiwemo viongozi wake wakuu (Waziri, Katibu Wakuu wawili (2) na Naibu Katibu Mkuu). Awamu ya pili inategemewa kukamilika ifikapo Agosti, 2017, Awamu ya Tatutakamilika ifikapo mwezi Februari, 2018 na awamu ya nne ifikapo mwezi Januari, 2019 kama ilivyoelekezwa.

g) Usimamizi wa Mapato na Matumizi

249. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuhakikisha kwamba, kila anayefanya biashara hapa nchini anakuwa na leseni halali inayolingana na biashara anayoifanya. Aidha, Maafisa Biashara wa Wizara na Sehemu ya Ufutiliaji na Uperembaji (M & E Section) wakishirikiana na Maafisa Biashara walio katika Halmashauri na Manispaa zote nchini wamefanya ukaguzi na kuchukua hatua za kisheria kwa mfanyabiashara yejote aliyepatikana akifanya biashara bila leseni au leseni stahili.

250. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia leseni za biashara, Wizara imehakikisha kuwa kila anayefanya biashara anakuwa na leseni halali kulingana na biashara anayofanya. Aidha, Wizara imeweka mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ambapo mtandao huo utaunganishwa na BRELA na hivyo kurahisisha leseni zote za biashara kupatikana katika kituo kimoja kadhalika, hali hii itarahisisha ufuutiliaji na uperembaji kupitia ofisi za kanda na BRELA.

251. *Mheshimiwa Spika*, kuhusu matumizi, Wizara imehakikisha kuwa matumizi ya fedha yanafanywa kulingana na Sheria, kanuni, taratibu za fedha na Ununuzi Serikalini. Ili kufanikisha lengo hili, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo na kuimarisha Kitengo cha Ugagazi wa Ndani, Kitengo cha Uhasibu na Kitengo cha Ununuzi na Ugavi.

h) Usimamizi wa Ununuzi

252. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia shughuli mbalimbali za Ununuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi Na.7 ya mwaka 2011(iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016) na Kanuni zake za mwaka 2013, GN 446. Katika kutekeleza majukumu yanayohusu usimamizi wa ununuzi, Wizara kupitia Kitengo chake cha Ununuzi kimetekeleza majukumu yafuatayo;

- (i) Mpango wa Ununuzi umeandaliwa ambao utekelezwaji wake ulikuwa ni wa kiwango cha wastani kutokana na kukosekana kwa fedha za kutosha kwenye Idara na Vitengo kwa mwaka 2016/2017;
- (ii) Vikao vya Bodi ya Zabuni vitatu viliratibiwa, vikiwemo viwili vya dharura na kimoja cha kawaida na kufanikisha upatikanaji wa ridhaa ya Bodi katika mambo mbalimbali yanayohusu ununuzi Wizarani;
- (iii) Ununuzi na kugawa bidhaa na huduma mbalimbali kwa mujibu wa Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2016/2017

umefanyika ambapo taarifa za Ununuzi za kila mwezi na kila robo ya mwaka ziliandaliwa na kuwasilishwa kwenye Taasisi ya kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA);

- (iv) Mali za Wizara (Physical Verification and stock taking) kwa mwaka 2016/2017 zimehakikiwa na kufanikisha uhuishaji wa Daftari la Mali za Wizara (Updating Asset Register) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake, GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004; na
- (v) Ushirikiano na Idara ya Utawala na Rasilimali Watu katika kufanikisha zoezi la kuhamisha vifaa vya Wizara kuhamia Dodoma awamu ya kwanza umefanyika kwa ufanisi.

i) **Masuala ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

253. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia matumizi bora na sahihi ya vifaa na mifumo ya TEHAMA kwa watumishi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa wadau wa ndani na wa nje. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wakala wa Serikali Mtandao imekamilisha kazi ya utengenezaji wa Mfumo na Mtandao wa Tovuti ya Biashara ya Kitaifa (National Business Portal). Mafunzo juu ya matumizi ya mfumo huo yamefanyika kwa ngazi mbali mbali, na sasa Wizara imeanza maandalizi ya kuuzindua rasmi mfumo huo ili uanze kutumika. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha tovuti yake kwa kuhuisha taarifa zake na kuuhabarisha umma juu ya kazi mbalimbali zinazotekelezwa kwa kuititia tovuti yake (www.mit.go.tz). Wizara itaendelea kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa miaka inayofuatia ili kuboresha utoaji huduma na taarifa kwa umma ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

j) **Huduma za Sheria**

254. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza majukumu yanayohusu usimamizi wa sheria, Wizara kuititia Kitengo cha Sheria imetekeleza majukumu yafuatayo;

- i) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Vipimo (Sura 340)"The Weight and Measures Act (Cap 340) kupitia marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 3/ 2016 ili kudhibiti vipimo visivyo sawa na kuhakikisha kuwa sheria hii inaendana na muda uliopo sasa;
- ii) Imefanya marekebisho Kanuni za Vipimo (The Weight and Measures (General) Regulations 2016. Pia, imeandaa Kanuni za Vipimo vya Umeme na Gesi asilia "The Weight and Measures (Metrological Control of Electricity and Natural gas Meters) Regulations 2017 ili kuendelea kumlinda mtumiaji;
- iii) Imeandaa alama za Viwango 21(Prescribed Standards Marks) kwa bidhaa mbalimbali ili kuendelea kumlinda mtumiaji wa bidhaa kupitia GN No. 290 ya 2016; na
- iv) Imeandaa Mikataba ya watoa huduma wote kwa Wizara.

4.5 MASUALA MTAMBUKA

a) Kushughulikia Malalamiko

255. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2016/2017, Wizara imeweza kutoa huduma kwa wadau wa ndani na nje kupitia Dawati la Kutoa Msaada kwa kushughulikia malalamiko na kero mbalimbali hususan katika Sekta za viwanda, biashara, masoko na uwekezaji. Wadau wamenufaika kupitia huduma hiyo kwa malalamiko na kero zao kupatiwa ufumbuzi. Katika kushughulikia malalamiko ya wateja, Wizara imebaini kuwepo kwa muingiliano wa sekta zetu na sekta nyingine kama vile sekta za kilimo, uvuvi, nishati na mawasiliano. Malalamiko ya sekta nyingine hupelekwa katika wizara na taasisi husika kwa hatua stahiki.

b) Kupambana na Rushwa

256. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa kutoa elimu na maelekezo kwa watumishi

wake juu ya kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazini na utoaji wa huduma bora bila kupokea au kutoa rushwa. Hadi kufikia Mei, 2017 hakuna mtumishi yeyote wa Wizara aliyeshitakiwa kwa kupokea au kutoa rushwa.

c) Usimamizi wa Mazingira

257. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imefanya tathmini ya athari ya mazingira kwa kushirikiana na NEMC kabla viwanda kuanzishwa, imekagua hali ya mazingira viwandani katika viwanda vilivyoanza uzalishaji, na imeshiriki kutoa maoni kuhusu utekelezaji wa usitishaji wa vifungashio vya plastiki vya ujazo mdogo vinavyofungashiwa pombe kali (maarufu kwa jina la VIROBA) linalotekelawa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. Aidha, Wizara kupitia, CAMARTEC imekuwa ikihamasisha matumizi ya biogas badala ya mkaa na kuni ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti.

d) Mapambano ya UKIMWI

258. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, usafiri na virutubisho kwa Watumishi watatu (3) wenye maambukizi ya VVU na walijitambulisha ili kuwaweka katika hali ya afya bora na kudumu zaidi kwenye utumishi wa umma. Aidha, Kamati ya UKIMWI ya Wizara ilifanya kikao mwezi Desemba, 2016 kwa ajili ya kufanya maandalizi ya semina elekezi kabla ya mwezi Juni, 2017 itakayotoa elimu kwa watumishi wote kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza.

e) Jinsia

259. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Tanzania Gender Networking Programme (TGNP) mwezi Julai, 2016 ilifanya mafunzo kwa wanawake wafanyabiashara 34 wa mipakani; Namanga, Holili na Mutukula ambao ni wanachama wa chama cha Wanawake wa Tanzania Wafanyabiashara Mipakani (WATABAM). Mafunzo hayo yalihu masuala ya vikwazo vya biashara visivyokuwa

vya kiushuru na kuelimishwa juu ya fursa za masoko zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na duniani kwa ujumla; kushiriki mafunzo ya kuwawezesha wafanyabiashara wanawake katika kukuza uchumi kupitia biashara mwezi Novemba, 2016; na kushiriki warsha kuhusiana na taarifa ya wafanyabiashara wanawake ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Novemba, 2016. Lengo la warsha hiyo lilikuwa ni kuelezea changamoto zinazowakabili mipakani na kuzitafutia ufumbuzi ili waweze kukuza biashara zao.

260. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na *UN Women* ilifanya tafiti mbalimbali za kuangalia fursa na changamoto zinazowakabili wanawake walioajiriwa viwandani, wanaofanya biashara au wenye viwanda ambazo ni:-

- i) Utafiti kwenye maeneo maalum ya uwekezaji ya viwanda (EPZ/SEZ) katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Shinyanga. Utafiti ulibaini kuwa kuna pengo kubwa la ajira *Gender Gap* kati ya wanawake na wanaume kwenye maeneo hayo ya uwekezaji pamoja na changamoto nyingi zinazowakabili wanawake wanao fanya kazi katika maeneo hayo;
- ii) Utafiti katika Maonesho ya Kimataifa ya 40 ya Sabasaba kuanzia tarehe 28 hadi 8 Julai, 2016 utafiti huo ulibaini changamoto iliyokuwa ikiwakabili wajasiriamali wadogo ambayo ni pamoja na kiingilio kikubwa katika maonesho hayo kilichopelekea watu kushindwa kuingia kwa wingi kujionea bidhaa walizokuwa wakizonesha na uhaba wa vifungashio bora;
- iii) Utafiti juu ya utekelezaji wa Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo (2008) katika mikoa ya, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro na Morogoro. Utafiti huo ulilenga kujua fursa zilizopo, changamoto na pengo lililopo katika masuala ya kijinsia katika utekelezaji wa sera hiyo. Utafiti huo ulionesha kuwa watendaji wengi na wajasiriamali hawaifahamu sera na kupelekea utekelezaji wake kuwa mgumu. Aidha, katika utafiti huo wajasiriamali walishauriwa kuongeza juhudhi katika kuongeza thamani mazao ya kilimo na kuepuka kuuza bidhaa ghafi hasa kwa wale wanaosafirisha nje ya mipaka ya Tanzania ili kujiongezea kipato zaidi.

261. *Mheshimiwa Spika*, Wizara pia ilishiriki kwenye kikao cha 61 cha Hali ya Wanawake Duniani (CSW 5961) kilichofanyika New York, Marekani mwezi Marchi, 2017. Kikao hicho pamoja na mambo mengine kilifanikiwa kupima utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia - MDG pamoja na kuangalia changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa juhudzi za kuleta usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa (Women Economic Empowerment in the Changing World of Work.)

262. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nitoe Malengo ya Mwaka 2017/2018 ya Wizara (Idara za Kisekta) na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

5.1 MALENGO YA MWAKA 2017/2018

5.2 IDARA ZA KISEKTA

5.1.1 Sekta ya Viwanda

263. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara ina malengo yafuatayo:-

- (a) *Kuendeleza jitihada za kuhamasisha sekta binafsi kuendeleza viwanda viliyopo na kuanzisha viwanda vipyta*
 - i) Kuwekeza nguvu kwenye viwanda vinavyotoa ajira nyingi (nguo na mavazi na ngozi);
 - ii) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya vioo baada ya kupata mafanikio ya ujenzi wa viwanda vya saruji na vigae;
 - iii) Kuendeleza Sekta ya Mafuta ya Kula;
 - iv) Kuhamasisha uongezaji wa uzalishaji wa sukari kwa kuhimiza viwanda vinavyozalisha chini ya uwezo wa uzalishaji kuongeza uzalishaji;
 - v) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya madawa ya binadamu; na

- vi) Kuhamasisha ujenzi wa viwanda vyta kuunganisha magari na matreka.
- (b) *Kuendeleza viwanda mama na miradi ya kimkakati*
- i) Kukamilisha mapitio ya vivutio vyta uwekezaji na kuanza utekelezaji wa Mradi wa Mchuchuma na Liganga;
 - ii) Kutafuta mwekezaji atakeyeingia ubia na Serikali kwa ajili ya kuendesha Kiwanda cha Matairi Arusha kwa misingi ya kibashara; na
 - iii) Kukamilisha utafiti wa faida za kiuchumi za Mradi wa Magadi wa Engaruka na kuanza utekelezaji.
- (c) *Kuendeleza jitihada za kubainisha na kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda*
- i) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa kuzingatia msambao wa viwanda nchi nzima;
 - ii) Kuhamasisha sekta binafsi kuendeleza maeneo ya uwekezaji yaliyokwishatengwa; na
 - iii) Kuendeleza makongano ya viwanda kwa sekta za nguo, ngozi na mafuta ya alizeti.
- (d) *Kujenga mfumo wa taarifa za sekta mbalimbali za viwanda nchini*
- i) Kuanzisha utambulisho maalum wa viwanda vidogo, vyta kati na vikubwa;
 - ii) Kukusanya taarifa za viwanda kisekta na kuzichambua kwa lengo la kufuatilia mwenendo wa viwanda wakati wote; na
 - iii) Kutafuta rasilimali za kujenga mfumo wa kielektroniki wa kuendesha taarifa za viwanda.
- (e) *Kufanya tathmini ya mahitaji ya ujuzi maalum wa viwanda na kuuendeleza*
- i) Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Nguo na Mavazi;
 - ii) Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta

- ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi;
- iii) Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Samani; na*
 - iv) Kubainisha wataalam wenye ujuzi maalum katika Sekta ya Vito na Madini.*
- (f) Kujenga uwezo wa taasisi za utafiti zilizo chini ya Wizara*
- i) Kuongeza uwezo wa mifumo ya uvumbuzi;*
 - ii) Kuimarisha uwezo wa maabara za utafiti;*
 - iii) Kuhamasisha usambazaji wa teknolojia zinazobuniwa na taasisi hizo; na*
 - iv) Kuhamasisha sekta binafsi kutumia teknolojia husika.*
- (g) Kushirikiana na Msajili wa Hazina na wizara za kisekta kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa visivyofanya kazi vinafanya kazi*
- i) Kukamilisha tathmini ya viwanda vyote vilivyobinafsishwa;*
 - ii) Kupitia mikataba ya ubinafsishaji ya viwanda visivyofanya kazi; na*
 - iii) Kuhamasisha uwekezaji mpya katika viwanda hivyo.*

5.1.2 Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

264. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo;

- (a) Kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo na biashara ndogo*
- i) Kutoa mwongozo kwa Serikali ngazi ya Mkoa na Wilaya namna ya kujenga viwanda vidogo ;*
 - ii) Kuhamasisha Serikali ngazi ya Wilaya na Mkoa kutenga maeneo ya ujenzi wa viwanda na biashara kwa kulenga mahitaji ya sasa na baadae;*
 - iii) Kubaini tabaka la kati na kulihamasisha kujenga viwanda*

- vidogo; na
- iv) Kukamilisha mwongozo wa taarifa muhimu kwa wajasiriamali wadogo wanapoanzisha biashara.
- (b) *Kuwezesha uanzishwaji wa kongano za samani*
- i) Kwa kushirikiana na wadau kuainisha na kutenga maeneo ya kujenga kongano la samani;
 - ii) Kuhamasisha wajasiriamali katika fani ya samani kufanya kazi sehemu moja na kwa pamoja; na
 - iii) Kutafuta rasilimali za kuendeleza kongano la samani.
- (c) *Kuendelea na kazi ya kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003*
- i) Kuendelea na tathmini ya utekelezaji wa sera ya sasa; na
 - ii) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kufanya mapitio ya tathmini na kutoa mtazamo wa sera inayoandaliwa.
- (d) *Kuendelea kusimamia Mfuko wa Kuwaendeleza Wajasiriamali Wadogo (NEDF)*
- i) Kuongeza mtaji wa Mfuko;
 - ii) Kuratibu kwa karibu wajasiriamali wote wanaofaidika na mfuko huo; na
 - iii) Kuhakikisha kwa kutumia mfuko huo, mtando wa viwanda unaenea nchi nzima.
- (e) *Kutumia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kama nyezo ya kujenga viwanda*
- i) Kulifanyia mageuzi Shirika la SIDO ili lishiriki kikamilifu katika ujenzi wa viwanda;
 - ii) Kuhamasisha wananchi kupitia maonesho juu ya ushiriki katika ujenzi wa viwanda;
 - iii) Kupitia maonesho kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kutumia bidhaa za ndani; na
 - iv) Kuhamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia kupitia viatamizi.

5.1.3 Sekta ya Biashara

265. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

(a) *Kuendeleza majadiliano ya kibiashara kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral) kwa ajili ya kupanua fursa za masoko na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji;*

- ***Biashara baina ya Nchi na Nchi***

- i) Kuratibu na kushiriki majadiliano ya kibiashara baina ya nchi na nchi kupitia Tume za Pamoja za Biashara (Joint Trade Commissions); na kushiriki katika majadiliano ya kibiashara na diplomasia baina ya nchi na nchi kupitia Tume za Pamoja za Kudumu (Joint Permanent Commissions). Lengo la majadiliano hayo ni kuimarisha mahusiano ya kibiashara na diplomasia ya kiuchumi, kuibua maeneo mapya ya ushirikiano na kutatua changamoto za kibiashara baina ya Tanzania na nchi hizo;
- ii) Kukamilisha mpango kazi wa utekelezaji kwa ajili ya kuongeza mauzo kwenye Soko la Marekani kupitia Mpango wa AGOA. Hiyo ikiwa ni pamoja na kubuni miradi ya uongezaji thamani katika maeneo ya bidhaa zilizoainishwa kwenye mkakati wa kitaifa wa AGOA;
- iii) Kuratibu na kushiriki katika jumbe/ziara za biashara nchi rafiki, ndani na nje ya nchi, zikiwemo China, India, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mauritius, Misri, Sudani ya Kusini, Urusi, Uturuki na Vietnam kwa lengo la kuimarisha biashara kati Tanzania na nchi hizo. Ziara hizo zinalenga kushirikisha sekta binafsi na kuunganisha sekta hiyo na wenzao kutoka nje katika kubaini fursa nafuu za biashara; na
- iv) Kuratibu na kushiriki katika makongamano ya biashara ndani na nje ya nchi.

- ***Biashara za Kikanda***

- i) Kuendelea na utekelezaji wa Itifaki za Soko la Pamoja na Ushuru wa Pamoja za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC Common Market and Customs Union Protocols) kwa lengo la kurahisisha na kuimarisha biashara katika Tanzania na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya hiyo. Maeneo yatakayowekewa mkazo ni pamoja na Uimarishaji wa Biashara ya Huduma, na Ushuru wa Forodha wa Pamoja (Common External Tariff-CET); na Uondoaji wa Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru (Non-Tariff Barriers-NTBs);
- ii) Kuendelea na utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Hiyo ikiwa ni pamoja kushiriki majadiliano ya biashara ya huduma; kusimamia ustawi wa uzalishaji na biashara ya sukari na karatasi za vifungashio kutoka Tanzania; na kushiriki katika utekelezaji wa Mkakati wa Viwanda wa SADC uliozinduliwa hivi karibuni kwa lengo la kuongeza uzalishaji na biashara ya bidhaa za viwandani ndani na nje ya SADC. Tunatarajia kuwa juhudi hizo zitasaidia kuongeza biashara ya Tanzania katika SADC;
- iii) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara la Utatu (Tripartite Free Trade Area-TFTA) linalojumuisha Kanda za COMESA,EAC na SADC; na
- iv) Kuratibu na kushiriki katika majadiliano yanayoendelea ya kuanzisha Eneo Huru la Biashara kwa Nchi za Afrika (*Continental Free Trade Area-CFTA*). Majadiliano hayo yatakapokamilika yatapanua zaidi soko na wigo wa wafanyabiashara nchini kufanya biashara katika Bara la Afrika. Aidha, tutatumia fursa hiyo kuvutia uwekezaji zaidi nchini na kuuzwa kwa unafuu katika masoko mapana ya kikanda na Afrika kwa ujumla.

- ***Biashara za Kimataifa***

- i) Kushiriki katika majadiliano ya kutunga sheria za kibashara kimataifa kupitia Mkutano wa 11 wa WTO wa Majadiliano Ngazi ya Mawaziri (WTO Ministerial Conference) unaotarajiwa kufanyika nchini Argentina mwaka 2017;
 - ii) Kushiriki katika majadiliano katika Kamati za Biashara za Kudumu za WTO (TBT, SPS na Trade Facilitation);
 - iii) Kuimarisha kamati za kitaifa za kusimamia urahisishaji wa biashara nchini ambazo ni;
 - Kamati ya Kusimamia Uondoaji wa Vikwazo vya Kibashara Visivyo kuwa vya Kiushuru (NTBs);
 - Kamati ya Urahisishaji Biashara (National Trade Facilitation Committee);
 - Kamati ya Usimamizi wa Masuala ya Afya za Binadamu, Wanyama na Mimea (National SPS Committee); na
 - Kamati ya Vikwazo vya Biashara vya Kiufundi (National TBT Committee).
- (b) *Kukamilisha mapendekezo ya uandikaji upya wa Sheria ya Anti-Dumping and Countervailing Measures.* Sheria hiyo ikikamilika, itasaidia kuvilinda viwanda na wafanyabiashara nchini dhidi ya athari ya bidhaa shindani zinazouzwa nchini kwa bei ya chini kwa udanganyifu, tofauti na bei halisi ya soko;
- (c) *Kuratibu zoezi la kuridhiwa kwa Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani (WTO) wa Urahisishaji wa Biashara (Trade Facilitation Agreement-TF).* Wizara itawasilisha rasimu ya pili ya Waraka wa kuridhiwa Mkataba huo ambao utaongeza chachu ya maboresho yanayoendelea nchini ya kurahisisha ufanyakaji biashara. Kupitia Mkataba huo, Tanzania itapata fursa za ziada za kifedha na kiufundi kuzidisha kasi ya maboresho ya ufanyakaji biashara nchini;

- (d) *Kuendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Kitaifa ya Urahisishaji Biashara* (National Committee for Trade Facilitation), na
- (e) *Kuratibu na kushiriki kwenye majadiliano ya biashara ya kimataifa katika mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa na mengineyo ikiwemo UNCTAD, CFC na ITC.*

5.1.4 Sekta ya Masoko

266. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018;
Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- (a) *Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji*
 - i) Kuondoa tozo, kero, ada zinazojirudia na kurazinisha majukumu ya taasisi za udhibiti;
 - ii) Kuondoa mwingiliano wa majukumu ya taasisi za umma ili kupunguza gharama za uanzishaji na uendeshaji wa biashara;
 - iii) Kuhakikisha huduma za usajili wa biashara unafanyika kuititia mitandao ya kompyuta (online registration) na usajili wa makampuni ufanyike kwa muda mfupi kadiri iwezekanavyo; na
 - iv) Kuhamisha jukumu la utoaji wa leseni za biashara toka Wizarani (Daraja A) kwenda BRELA na kutolewa katika kanda za Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza.
- (b) *Kuwaunganisha wazalishaji na masoko*
 - i) Kuwahamasisha wakulima kuzalisha na kuwaunganisha na viwanda vya usindikaji;
 - ii) Kushirikiana na viwanda kutafuta masoko ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa nchini;
- (c) *Kuendelea kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala*
 - i) Kuhamasisha sekta binafsi kujenga maghala;

- ii) Kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa maeneo yote yanayozalisha zao la korosho;
 - iii) Kuanzisha matumizi ya Mfumo kwa mazao ya ufuta, mbaazi, mahindi na nafaka; na
 - iv) Kuunganisha Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Mazao na Bidhaa (commodity exchange)
- (d) *Kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo maalum vya kuuzia mazao*
 - i) Kusimamia matumizi ya vituo hivyo ili vitumike kwa uuzaaji na ununuzi wa mazao;
 - ii) Kuhamasisha ushindani wakati wa kununua na kuuza ili mkulima apate bei nzuri; na
 - iii) Kusimamia na kuhimiza matumizi ya vipimo rasmi kwa nia ya kumlinda mlaji.
- (e) *Kuimarisha biashara na masoko ya mipakani*
 - i) Kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kujenga Vituo vya Pamoja vya Ulaguzi Mipakani;
 - ii) Kutoa elimu kwa jamii ya wafanyabiashara kuhusu fursa na taratibu za kufanya biashara ya mipakani (cross border trade); na
 - iii) Kubainisha vikwazo vya kufanya biashara mipakani na kushirikiana na mamlaka nyingine katika kuviondoa.
- (f) *Kuhamasisha na kuwezesha wananchi kutangaza bidhaa na huduma za Tanzania*
 - i) Kuwapatia mabanda wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na makundi maalum kutangaza bidhaa kupitia maonesho;
 - ii) Kuratibu ushiriki wa wajasiriamali na wafanyabiashara wa Tanzania katika maonesho ya ndani na nje ya nchi; na
 - iii) Kuratibu ushiriki wa sekta binafsi na wataalam wa Serikali katika safari maalum za kutafuta fursa za masoko nje ya nchi.

- (g) *Kuimarisha na kuboresha Mfumo wa Ukusanyaji wa Taarifa za Masoko*
- i) Kupanua wigo wa vyanzo na aina ya taarifa za masoko; na
 - ii) Kutoa vitendea kazi vya kisasa kwa vyanzo vya taarifa na kukuza matumizi ya TEHAMA kukusanya na kusambaza taarifa muhimu za masoko.
- (h) *Kuandaa na kupitia Sera, Sheria na Kanuni za mbalimbali*
- i) Kuandaa Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji (National Consumer Protection Policy);
 - ii) Kuandaa Sera ya Taifa ya Viwango (National Quality Policy);
 - iii) Kukamilisha Sera na Mkakati wa Miliki Bunifu;
 - iv) Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 na Kanuni zake;
 - v) Kukamilisha Marekebisho ya Sheria ya Haki Miliki na Haki Shiriki ya Mwaka 1999;
 - vi) Kuandaa Kanuni za utekelezaji wa marekebisho ya Sheria ya Vipimo ya 2016;
 - vii) Kushirikiana na OR-TAMISEMI kuandaa sheria ndogo ya kusimamia matumizi ya vipimo rasmi katika biashara ngazi ya vitongoji, vijihi na wilaya ; na
 - viii) Kuandaa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje.

5.1.5 Sekta ya Uwekezaji

267. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

- (a) *Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996;*
- i) Kuratibu uwepo wa mazingira bora ya uwekezaji;
 - ii) Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza nchini; na

- iii) Kuhamasisha wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa za uwekezaji za kikanda na kimataifa.
- (b) *Kukamilisha mapitio ya Sera, Mkakati na Sheria ya Uwekezaji*
 - i) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996;
 - ii) Kukamilisha mapitio ya Sheria ya Uwekezaji ya 1997; na
 - iii) Kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji.
- (c) *Kufuatilia miradi ya uwekezaji nchini*
 - i) Kuratibu uanzishwaji wa kamati ya kitaifa ya kufuatilia uwekezaji nchini; na
 - ii) Kufanya tathmini ya miradi yote iliyowekezwa nchini.
- (d) *Kuratibu kwa karibu uwekezaji katika sekta maalum*
 - i) Kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya sukari;
 - ii) Kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu (deep sea) na viwanda vya samaki; na
 - iii) Kuanzisha na kuboresha vivutio vya uwekezaji katika viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi “*Light Manufacturing*”.

5.2 TAASISI CHINI YA WIZARA

5.2.1 Shirika la Maendeleo la Taifa

268. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018; Wizara kuititia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) itatekeleza malengo yafuatayo:

- (a) Kukamilisha mapitio ya vivutio na Mkataba wa Utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma na kuanza utekekelezaji;
- (b) Kuendelea kutafuta mwekezaji wa kutekeleza Mradi wa Kuzalisha Magadi wa Engaruka;
- (c) Kuendelea kutafuta mwekezaji atakayeingia ubia na Serikali

- kwa ajili ya kufufua Kiwanda cha Matairi cha Arusha;
- (d) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kufufua Kiwanda cha KMTC;
 - (e) Kuhamasisha utekelezaji wa Mradi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta katika eneo la TAMCO;
 - (f) Kuendeleza utekelezaji wa mradi wa viwanda vyatia kusindika nyama Dodoma, Kibaha na Pwani;
 - (g) Kuendelea kutafuta mwekezaji kwa ajili ya kuendeleza mradi wa kuzalisha mafuta kutokana na michikichi;
 - (h) Kuendelea kutafuta mwekezaji kwa ajili ya wa Mradi wa Kilimo cha Ufuta katika Kijiji cha Mandawa;
 - (i) Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Miundombinu katika Eneo la Viwanda la TAMCO Kibaha;
 - (j) Kuanzisha upembuzi yakinifu wa kuanza ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea Asili (biofertilizer) katika eneo la Kiwanda cha Biolarvicides (viuadudu);
 - (k) Kugawa eneo la viwanda (*Cadastral survey*) eneo la KMTC; na
 - (l) Kwa kushirikiana na RAHCO kutafuta mwekezaji kwa ajili ya kuanzisha mgodi wa mawe wa kuzalisha kokoto za zege, reli, ujenzi na kiwanda cha kutengeneza nguzo za umeme, taa za barabarani na simu (*concrete electric poles*), Muheza Tanga.

5.2.2 Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania

269. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenyelengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;
- (b) Kuanzisha na kuhakiki maabara ya makaa ya mawe, mafuta na gesi itakayokuwa na viwango vyatia kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
- (c) Kuendelea na mchakato wa kufanya utafiti na kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ngozi jinsi ya kupunguza

- uharibifu wa mazingira kwa kuhifadhi na kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama ‘Leather boards’;
- (d) Kuendelea na kukamilisha mchakato wa kuhakiki (Accreditation) na kuboresha maabara ya mazingira, kemia na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;
 - (e) Kuanzisha na kuhakiki (Accreditation) maabara ya vipimo vya chuma kigumu (Iron and Steel metallurgy laboratory);
 - (f) Kufanya matengenezo ya vifaa vya maabara ya mazingira, chakula na kemia;
 - (g) Kutafiti vigezo vya uzalishaji wa chuma cha pua (steel bar production parameter) katika viwanda/mashine za kawaida za chuma (conventional rolling mill); na
 - (h) Kuendelea kukamilisha mapitio ya Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 iliyozindua TIRDO kwa kuwasilisha ripoti ya mapitio ya sheria kwa Wizara mama (Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji) na hatimaye kupelekwa Bungeni.

5.2.3 Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo

270. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kujenga uwezo wa taasisi katika kubuni, kuendeleza na kusambaza teknolojia kwa kuboresha (upgrade) na kukarabati vitendea kazi (mashine na vifaa mbalimbali) vya karakana ya kuunda na kuendeleza chasili, kuboresha vitendea kazi katika ofisi za usanifu zikiwemo programu zitumikazo katika shughuli za ubunifu na usanifu na kuongeza ujuzi wa wafanyakazi wa taasisi katika teknolojia ya utengenezaji wa hali ya juu;
- (b) Kuboresha, kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji na utumiaji kibiashara wa mitambo ya kusindika mafuta ya kula yatokanayo na mbegu za mafuta. Mitambo hiyo inahusisha

- mashine za kusafisha mbegu, kukamua, kuchuja na kusafisha mafuta (refining);
- (c) Kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji kibiashara wa teknolojia za kuzalisha bidhaa za marumaru kama vile vigae vya marumaru (ceramic tiles) kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini;
 - (d) Kuboresha teknolojia za kuteketeza taka ngumu na hatarishi zitokanazo na utoaji wa huduma za afya na huduma za udhibiti kwa lengo la kulinda afya na mazingira;
 - (e) Kubuni na kuendeleza teknolojia jadidifu hususan mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji na nishati ya upepo na mtambo wa kutengeneza kuni na mkaa utokanao na mabaki ya mimea au vumbi la makaa ya mawe, na
 - (f) Kufanya utafiti kuhusu aina ya vifaa vya pikipiki na vifaa vya pikipiki za miguu mitatu vinavyoweza kutengenezwa nchini na kufanya majaribio na kutengeneza utaratibu wa kuunda (manufacturing process) vipuri vya pikipiki hapa nchini kwa kuwezesha wajasiriamali watengenezaji.

5.2.4 Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini

271. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kujenga uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kununua zana za kilimo zilizofanyiwa majaribio nchini;
- (b) Kujenga maabara kwa ajili ya majaribio ya zana za kilimo;
- (c) Kutafiti mahitaji, kuendeleza na kutengeneza teknolojia mbalimbali za kilimo na ufundi vijijini hasa kwenye uendelezaji wa teknolojia ya trekta la CAMARTEC (CFT), teknolojia za vipandio za kukokotwa na ng'ombe na kuvutwa na trekta (planters), na mashine za kuvuna na kuchakata mazao ya mifugo, alizeti, mbaazi, mahindi na mpunga (agro-processing) kwa kushirikiana na wadau wetu wa ndani (wabunifu, wajisiliamali, vyuo vikuu na mashirika ya sio ya

- kiserikali); na
- (d) Kutafiti na kuendeleza usambazaji wa teknolojia za matumizi bora ya nishati ya kuni, mkaa na biogesi kwa kushirikiana na wajasiriamali, makampuni binafsi, mafundi, Wizara ya Nishati na Madini, Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) na wadau wetu wa maendeleo ambao ni *Africa Biogas Partnership Programme* (ABPP).

5.2.5 Kampuni ya Mbolea Tanzania

272. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kukamilisha majadiliano ya kuanzisha mtambo wa kutengeneza mbolea aina ya NPKs nchini;
- (b) Kuanza utekelezaji wa Makubaliano ya Awali (MoU) na Kampuni ya OCP ya Morocco wa kununua mbolea kutoka Kampuni hiyo na kuisambaza nchini; na
- (c) Kuendelea kununua na kusambaza mbolea za aina mbalimbali nchini.

5.2.6 Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje

273. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Mamlaka ya Kuendeleza Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo Nje (EPZA) itatekeleza yafuatayo:

a) *Bagamoyo SEZ*

- i) Kuratibu usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani ya mradi kwa awamu ya kwanza;
- ii) Kuratibu uboreshaji wa makazi holela (*Regularization and upgrading*) ya maeneo ya makazi ya Kiromo, Mlingotini na Zinga; na

- iii) Kuratibu ujenzi na usambazaji wa miundombinu ya nje, umeme na maji kufikia eneo la mradi, (*offsite infrastructure*).*

b) *Kurasini Trade and Logistic Centre*

- i) Kuhakikisha upatikanaji wa hati miliki ya eneo lote la mradi; na*
ii) Kuingia ubia na sekta binafsi katika kuendeleza na kuendesha mradi.

c) *SEZ za Bunda, Kigoma, Manyoni, Mtwara, Ruvuma na Tanga*

- i) Kumalizia malipo ya fidia katika maeneo ya mradi yaliyofanyiwa uthamini ya Kigoma, Manyoni, Ruvuma na Tanga SEZ;*
ii) Kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya ndani katika maeneo ya mradi wa Kigoma;
iii) Kupima viwanja (survey) na gharama za usajili wa hati miliki katika maeneo ya miradi ya Bunda, Kigoma, Manyoni na Tanga; na
iv) Kuendelea kutangaza miradi kitaifa na kimataifa na kuendeleza shughuli zote za maaendeleo ya miradi ya Ruvuma na Tanga.

5.2.7 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo

274. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) itatekeleza malengo yafuatayo:

- a) *Kujenga maeneo ya viwanda katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, na Simiyu;***
- i) Kujenga miundombinu ya viwanda (barabara, mifumo ya maji, Umeme na mitaro ya maji machafu) katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, na Simiyu;*

- ii) Kujenga mabanda ya viwanda kumi na moja katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, na Simiyu;
 - iii) Kujenga ofisi za SIDO za kutolea huduma katika mikoa mipyä ya Geita na Simiyu ; na
 - iv) Kusajili viwanda vyote vidogo nchini.
- b) *Kuimarisha uwezo wa uhawilishaji wa teknolojia;*
 - i) Kuimarisha Kituo cha Maendeleo ya Teknolojia cha Shinyanga; na
 - ii) Kuwezesha utengenezaji na usambazaji wa teknolojia rahisi za vijiji.
- c) *Kutekeleza Mkakati wa Wilaya Moja Bidhaa Moja (ODOP);*
 - i) Kupitia upya maelezo na takwimu za kila Wilaya na kutengeneza maandiko yatayotumiwa na watu kuanzishia miradi ; na
 - ii) Kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo.
- d) *Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali - Kwa kuuongezea mtaji Mfuko wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wananchi (NEDF).*

5.2.8 Chama cha Hakimiliki Tanzania

275. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuongeza makusanyo ya mirabaha kutoka kwa watumiaji wa kazi za sanaa / muziki na kugawa kwa wasanii;
- (b) Kuendeleza mazungumzo na mashirika ya utangazaji ili waanze kulipia mirabaha;
- (c) Kutoa elimu kwa wananchi na wadau wa sanaa kuhusiana na mambo ya Hakimiliki na Hakishiriki;
- (d) Kufanya ukaguzi wa kazi zinazolindwa na Sheria ya Hakimiliki

- na Hakishiriki (anti piracy raids);
- (e) Kushughulikia migogoro na kesi za Hakimiliki na Hakishiriki ;
- (f) Kushughulikia marekebisho ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7/1999 na Kanuni za Leseni na kanuni zingine zinazohusiana na Hakimiliki; na
- (g) Kuendelea kusajili wanachama wasanii na kazi zao.

5.2.9 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

276. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuandaa Sera ya Uwekezaji, uendeshaji wa Akaunti ya Kinga ya utendaji kwa waendeshaji wa ghala na Sera ya Mafunzo ili kuongeza ufanisi;
- (b) Kufuatilia vibali vya ajira kujaza nafasi zilizo wazi katika ikama ya Bodi;
- (c) Kuandaa mukutano wa wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala;
- (d) Kuainisha na kufanya ukaguzi wa ghala zilizosajiliwa chini ya mfumo na zinazotarajiwu kusajiliwa;
- (e) Kutafuta na kuboresha vyanzo vya ndani vya mapato kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi;
- (f) Kuandaa warsha za kisekta kwa wadau kama chombo cha kupata mrejesho wa uendeshaji wa Mfumo kutoka kwa wadau wa zao husika;
- (g) Kupata mtaalamu/mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuandaa, Sera ya Uwekezaji, Sera ya kuendesha Akaunti ya Kinga ya Utendaji pamoja na taratibu za ndani juu ya utoaji wa leseni za kuendesha ghala;

- (h) Kupitia upya Mpango Mkakati wa Bodi ili kuainisha na kuyaondoa majukumu yaliyokwisha kutekelezwa na kuongeza majukumu mengine ya kipaumbele katika taasisi;
- (i) Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo husika;
- (j) Kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi kwa wadau wote ili waelewe na kutekeleza kwa ufanisi;
- (k) Kushiriki katika Maonesho ya Sabasaba na Nanenane ili kutoa elimu ya mfumo kwa wadau hususan wadau wa kilimo; na
- (l) Kufanya maandalizi ya kuhamia Dodoma.

5.2.10 Baraza la Ushindani

277. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Baraza la Ushindani (FCT) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kusikiliza na kutoa maamuzi ya kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa udhibiti na ushindani wa kibashara nchini;
- (b) Kuongeza uwezo wa Baraza katika kushughulikia kesi zinazohusu masuala ya ushindani wa kibashara kwa kuwaongezea ujuzi Wajumbe wa Baraza, Watumishi wa Baraza sambamba na maboresho katika mifumo ya utendaji kazi wa Baraza;
- (c) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza, umuhimu katika uchumi pamoja na namna ya kuwasilisha rufaa katika Baraza; na
- (d) Kuendelea kushughulikia masuala mtambuka ikiwa ni pamoja na utawala bora na mapambano dhidi ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI.

5.2.11 Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni

278. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018; Wizara kupitia Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuendelea kuboresha mifumo na taratibu za utoaji huduma kwa kutumia njia za kiteknolojia ili kutoa huduma bora na kwa wakati;
- (b) Kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kufungua vituo vya kutoa huduma mikoani na wilayani;
- (c) Kuboresha mifumo ya uwajibikaji, weledi na uadilifu kwa watumishi wa BRELA;
- (d) Kujenga mifumo thabiti ya mawasiliano ndani na nje ya ofisi;
- (e) Kupitia upya muundo wa wakala ili uweze kwenda na wakati;
- (f) Kupitia sheria zote zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati;
- (g) Kuendelea kutoa Elimu na Uhamasishaji wa Usajili na Urasimishaji wa Biashara kwa wananchi katika ngazi za mikoa na wilaya; na
- (h) Kuanzisha utoaji wa leseni za biashara daraja la kwanza kwa ngazi za kanda.

5.2.12 Wakala wa Vipimo

279. *Mheshimiwa Spika*, Katika Mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kukagua na kusimamia matumizi sahihi ya vipimo 745,702;
- (b) Kutoa elimu kwa umma kupitia maonesho saba (Sabasaba, Nanenane, MOWE), kuandaa na kufanya vipindi kumi vya televisheni na radio na matangazo matano kuhusu matumizi sahihi ya vipimo;
- (c) Kuiboresha kanzidata ya vipimo itakayotumiwa wakati wa kupanga mipango ya Wakala;

- (d) Kununua vitendea kazi yakiwemo magari kumi na vihakiki mita za maji, umeme na gesi;
- (e) Kuanzisha na kutekeleza Mfumo wa Ufuartiliaji na Tathmini (M&E) ili kuimarisha utunzaji wa takwimu mbalimbali;
- (f) Kuongeza idadi ya watumishi 96 na kuwaongezea uwezo wa kitaalam waliopo ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia;
- (g) Kufanya maboresho ya ofisi nne za Wakala wa Vipimo katika mikoa Tanzania Bara na kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Upimaji Matenki ya Mafuta Misugusugu Kibaha;
- (h) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika kutekeleza majukumu ya Wakala; na
- (i) Kuongeza juhudu katika ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwenye maeneo mbalimbali ya mipakani, bandarini na viwandani kwa lengo la kuhakiki uzito, ujazo, vipimo vya urefu au namba kwa lengo la kumlinda mlaji.

5.2.13 Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji

280. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji (NCAC) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Tume ya Ushindani ili iweze kuruhusu ajira ya Afisa Mtekelezaji Mkuu wa Baraza la Taifa la Mtetezi wa Mlaji;
- (b) Kuanda hadidu za rejea za Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji; na
- (c) Kumwanda Mtaalamu Mwelekezi kuanda Rasimu ya Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji.

5.2.14 Shirika la Viwango la Taifa

281. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Shirika la Viwango la Taifa (TBS) itatekeleza

yafuatayo:-

- (a) Kusimamia kwa nguvu zote ubora wa bidhaa hasa zinazotoka nje ili kulinda viwanda vya ndani;
- (b) Kutayarishaviwango 350 vyakitaifakatikasektandogondogo, ambavyo kati ya hivyo 120 ni vya uhandisi (Engineering) na 230 ni vya usindikaji (Process Technology);
- (c) Kutoa leseni ya ubora kwa bidhaa 240 kutoka katika sekta mbalimbali zikiwemo bidhaa za wajasiriamali wadogo (SMEs);
- (d) Kukagua ubora wa bidhaa 34,000 zitokazo nchi za nje kabla ya kuingia nchini (Pre-Shipment Verification of Conformity to Standards- PVoC (CoCs));
- (e) Kufanya ukaguzi wa ubora na kutoa leseni za ukaguzi 42,000 za magari yaliyotumika (used motor vehicles) yanayoingizwa nchini;
- (f) Kutoa hati 45 chini ya Mpango wa Msaada wa Kiufundi kwa Wauzaji wa Bidhaa za Nje (Technical Assistance to Exporters - TAE);
- (g) Kutoa mafunzo na semina 30 kuhusu viwango na udhibiti wa ubora (Quality Assurance Training) kwa wadau mbalimbali;
- (h) Kupima sampuli 10,000 za bidhaa mbalimbali;
- (i) Kufanya ugezi kwa vifaa/mashine mbalimbali vipatavyo 8,000;
- (j) Kufungua ofisi mpya tano za mipakani;
- (k) Kujenga maabara mpya ya kisasa (New TBS Test House);
- (l) Kuanzisha na kufungua ofisi mpya tano za kanda, (Kanda ya Kaskazini-Arusha, Kanda ya Nyanda za Juu-Mbeya, Kanda ya Ziwa- Mwanza, Kanda ya Kati-Dodoma na Kanda ya Kusini-Mtwara); na
- (m) Kuajiri wafanyakazi 136 kwa kibali cha mwaka 2015/2016 na wafanyakazi 114 kwa mwaka 2017/2018.

5.2.15 Tume ya Ushindani

282. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Tume ya Ushindani (FCC) itatekeleza yafuatayo:

(a) Kudhibiti na Kupambana na Uingizaji na Uzalishaji wa Bidhaa Bandia;

- i) Tume ya Ushindani itafanya kaguzi za kushtukiza katika mikoa mbalimbali. Kaguzi hizo zitahusisha bidhaa mbalimbali kama vile zitakavyowekwa kwenye mpango kazi wa mwaka husika na zile zitakazoripotiwa na Wamiliki wa Hataza (brand owners);
- ii) Tume ya Ushindani itaendelea na ukaguzi bandarini na katika bandari kavu (ICDs) kama itakavyotakiwa katika mpango kazi wa mwaka 2017/18;
- iii) Tume ya Ushindani inaendelea kujipanga katika mpango kazi wake wa mwaka 2017/18 ili kuweza kuwa na ofisi katika mikoa mbalimbali kama ambavyo imekuwa ikiombwa/ikishauriwa kwa nyakati tofauti tofauti, na kuanzia mikoa inayotarajiwa ni Tanga, Arusha na Mwanza; na
- iv) Kuendelea na juhudi za kupambana na kuthibiti bidhaa bandia ambazo zinachangia katika kudidimiza soko la Tanzania.

(b) Uchunguzi na Usikilizaji wa Kesi za Ushindani;

- i) Kuendelea kuchunguza na kuchukua hatua za kisheria juu ya mashauri mbalimbali yahusuyo makubaliano yanayofifisha ushindani “Anti-competitive agreement”;
- ii) Kuchunguza mashauri yahusuyo miungano ya makampuni ambayo haikutolewa taarifa kwenye Tume “Un-notified mergers”; na

- iii) Kuchunguza na kuchukua hatua za utekelezaji wa sheria juu ya mashauri yahusuyo matumizi mabaya ya nguvu katika soko “Abuse of market power”.*
- (c) Utafiti wa Masoko ili Kubaini Matatizo ya Ushindani Usio wa Haki na Masoko husika na Hatua za Kurekebisha;*
- i) Kufanya utafiti katika Sekta ya Afya zitakazohusisha upitiaji wa maandiko, uandaaji wa andiko dhana na ukusanyaji wa takwimu na taarifa muhimu kutoka maeneo mbalimbali; na*
 - ii) Kufanya utafiti katika sekta nyingine kama itakavyoagizwa.*
- (d) Kumlinda na Kumuelimisha Mlaji;*
- i) Kuendelea kushughulikia malalamiko ya walaji wa bidhaa na huduma;*
 - ii) Kufanya mapitio na usajili wa mikataba ya walaji;*
 - iii) Kushiriki katika kutengeneza Sera ya Taifa ya Kumlinda Mlaji;*
 - iv) Kuendelea kusikiliza na kushughulikia malalamiko kuhusu bidhaa zisizo salama; na*
 - v) Kuandaa miongozo kuhusu sheria ya kumlinda mlaji na mikataba inayomkandamiza mlaji.*

5.2.16 Kituo cha Uwekezaji Tanzania

283. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kufanya uhamasishaji kwa kuwalenga wawekezaji wa nje (Targeted Investment Promotion) na pia kufanya uhamasishaji wa wawekezaji wa ndani ili kuvutia wawekezaji kwenye sekta muhimu zitakazokuza urchumi wa nchi kwa haraka hususan Sekta ya Viwanda;*

- (b) Kuimarisha Kitengo cha Kuperemba Miradi ya Uwekezaji (Monitoring and Evaluation) kwa lengo la kuhakiki miradi ilioandikishwa TIC;
- (c) Kutembelea miradi iliyosajiliwa na TIC kwa lengo la kutatua matatizo yanayowakabili wakati wa kutekeleza miradi yao;
- (d) Kuwasaidia wawekezaji kupata vibali na hati mbalimbali za kisheria ili waweze kuwekeza hapa nchini;
- (e) Kufanya tafiti mbalimbali zitakazotumika kuishauri Serikali kuhusu Sera ya Uwekezaji;
- (f) Kuhudumia wawekezaji kwa kuboresha huduma mahali pamoja (One Stop Shop) na kuwezesha usajili kwa njia ya mtandao;
- (g) Kuchapisha na kusambaza taarifa sahihi kwa wawekezaji kuhusu fursa za uwekezaji pamoja na upatikanaji wa mitaji ya wabia;
- (h) Kushirikiana na Serikali kutafuta maeneo yenyeye ardhi inayofaa kuwekeza kwa ajili ya wawekezaji;
- (i) Kuwasaidia wajasiliamali wadogo na wa kati kuibua fursa za uwekezaji na pia kuwaunganisha na wafanyabiashara wakubwa (Business Linkages) kwa lengo la kukuza biashara zao na kuongeza kipato;
- (j) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kituo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; na
- (k) Kutekeleza mkakati wa kukitangaza kituo na kazi zake kwa wawekezaji na wanaotaka kuwekeza (Information and Communication Campaign) ili wafahamu vivutio vyatua uwekezaji vilivyopo nchini.

5.2.17 Chuo cha Elimu ya Biashara

284. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kukamilisha ujenzi wa ghorofa tatu katika Jengo la 'Cafeteria' (Vertical Extension of Cafeteria Building) Kampasi ya Dar

- es Salaam kwa ajili ya maktaba mpya, madarasa pamoja na kumbi za mihadhara;
- (b) Kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa ghorofa tisa katika Kampasi ya Dar es Salaam;
 - (c) Ujenzi na ukarabati wa majengo katika Kampasi ya Mwanza;
 - (d) Awamu ya pili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya katika eneo la Iganzo;
 - (e) Ujenzi wa Kampasi ya Zanzibar;
 - (f) Kuboresha mifumo ya TEHAMA; na,
 - (g) Kuimarisha uwezo wa watumishi (Capacity building) katika mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya shahada za uzamili na uzamivu.

5.2.18 Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania

285. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) itatekeleza yafuatayo:-

- (a) *Kuboresha Upatikanaji wa Soko la Bidhaa na Huduma zinazozalishwa Nchini;*
Katika kutimiza jukumu hilo, TanTrade kwa kushirikiana na Mamlaka zingine za Serikali na sekta binafsi, imedhamiria kuboresha uratibu wa maonesho ya biashara yanayofanyika hapa nchini yakiwemo Maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, Maonesho ya Nanenane na Maonesho ya SIDO. Pia itaratibu na kuongoza misafara na mikutano ya kibiashara, kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Maonesho ya Kibiashara ya Kigali-Rwanda, Nairobi-Kenya, Maputo-Msumbiji na Bujumbula – Burundi. Vilevile, itaratibu Tamasha la Biashara Mjini Zanzibar na pia kukusanya na kusambaza kwa wadau mbalimbali hususan wazalishaji na wafanyabiashara wa Tanzania taarifa za biashara na masoko ya bidhaa mbalimbali zinazozalishwa hapa nchini.

- (b) *Kuratibu na Kudhibiti Uendeshaji wa Maonesho ya Kimataifa Nchini kwa Mujibu wa Sheria;*

Mamlaka itaendelea kutoa vibali kwa waandaji wote wa

maonesho ya kimataifa yatakayoandalika nchini na nje ya nchi na kuhakikisha kuwa waandaaji hao wanafuata taratibu za uandaaji wa maonesho kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya ubora kiwemo usalama wa watembeleaji, usafi, upatikanaji wa huduma muhimu zikiwemo choo na matibabu ya dharula, mpangilio wa majengo na usafiri wa uhakika.

(c) Kuimarisha na Kuijengea Uwezo Sekta Ndogo na ya Kati ya Biashara (SMEs) ili iweze Kujiendesha Kiushindani;

TanTrade itaendelea na jukumu lake la msingi la kuwajengea wazalishaji na wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs) uwezo kwa njia ya mafunzo, kuwapa taarifa za biashara na masoko, kutatta changamoto na vikwazo vya kiutendaji na kuweka mazingira rafiki ya kibiashara ili waweze kufikia vigezo vya ushindani na kuongeza tija na ufanisi kimataifa katika uzalishaji na biashara zao.

(d) Kuongeza Ushindani katika Sekta ya Biashara;

TanTrade kwa kushirikiana na sekta binafsi, taasisi na wizara za serikali itahimiza uchakataji wa bidhaa asili za Tanzania ikiwemo mazao ya kilimo, misitu, uvuvi na madini kabla hazijauzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Hatua hiyo imelenga kuongeza thamani ya bidhaa husika, ajira kwa rasilimali za Tanzania ikiwemo rasilimali watu (wafanyakazi), ardhi na madini. TanTrade kwa kushirikiana na vituo vya uwekezaji TIC, ZIPA na EPZA itahimiza utengenezaji wa bidhaa za mwisho (Final Consumer Goods) kwa maliasili zinazozalishwa hapa nchini zikiwemo nguo, bidhaa za ngozi, unga wa kakao, mafuta ya kupikia, kwa kutaja machache.

5.3 MAENDELEO YA RASILIMALI WATU NA UTOAJI WA HUDUMA

5.3.1 Maendeleo ya Rasilimali Watu

286. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuhamishia watumishi 81 Makao Makuu ya Nchi Dodoma katika Awamu ya Tatu;
- (b) Kuajiri watumishi wapya 23 wa kada mbalimbali ili kuziwezesha Idara na Vitengo kupata rasilimali watu ya kutosha ili kutoa huduma bora inayotarajiwa;
- (c) Kupandisha vyeo watumishi 143 wa kada mbalimbali;
- (d) Kujenga uwezo kwa rasilimali watu kwa kuwapeleka watumishi kumi na tano katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi hamsini katika mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbalimbali ambayo yatawasaidia kuboresha utendaji wao wa kazi na kukidhi mahitaji ya kimuundo katika kada mbalimbali;
- (e) Katika Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (MWAMTUKA au OPRAS), Wizara itatekeleza yafuatayo;
 - i) Kutoa mafunzo kwa watumishi wapya watakaoajiriwa kuhusu namna ya ujazaji wa fomu za OPRAS;
 - ii) Kuhakikisha kuwa watumishi wote wanasaini mikataba yao ya kazi kwa wakati;
 - iii) Kufanya mapitio ya nusu mwaka; na
 - iv) Kufanya tathmini ya utendaji kazi wa watumishi wa mwaka mzima kwa wakati.
- (f) Kuwa na program mbalimbali za michezo kwa lengo la kujenga afya za watumishi, kushirikiana na kufahamiana;
- (g) Kuendelea na uratibu wa masuala ya uendeshaji wa shughuli za Wizara;

- (h) Kuratibu shughuli za utoaji huduma stahiki kwa viongozi na watumishi wa Wizara kwa kuzingatia Taratibu, Miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma; na
- (i) Kuhakikisha watumishi watakaohitimisha ajira zao wanalipwa mafao kwa wakati.

5.3.2 Usimamizi wa Ununuzi

287. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza yafuatayo:

- (a) Kuandaa Mpango wa Ununuzi wa Wizara kwa mwaka 2017/2018;
- (b) Kuratibu vikao vya Bodi ya Zabuni;
- (c) Kufanya ununuzi na kugawa bidhaa na huduma mbali mbali kwa mujibu wa Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2017/2018 ambapo taarifa za ununuzi za kila mwezi na kila robo ya mwaka zitaandaliwa na kuwasilishwa kwenye Taasisi ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA); na
- (d) Kuhakiki mali za Wizara (Physical Verification and stock taking) kwa mwaka 2017/2018 na kufanikisha uhuishaji wa Daftari la Mali za Wizara (Updating Asset Register) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 na Kanuni zake, na GN.132 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004.

5.3.3 Masuala Mtambuka

(a) *Kudhibiti Rushwa*

288. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kuweka mikakati mbalimbali na kutoa mafunzo ya sheria mbalimbali za kazi, kanuni na taratibu zinazotoa miongozo

ya utoaji wa huduma bora na uwajibikaji katika utumishi wa umma na kuhakikisha kuwa zinafuatwa. Aidha, Wizara itahakikisha kuwa inawachukulia hatua za kinidhamu watumishi ambao watabainika kujihusisha na vitendo vya rushwa. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya elimu ya Huduma kwa Mteja kwa watumishi ili kuwapatia mbinu za utoaji huduma bora kwa wateja wake wa ndani na nje ya Wizara.

(b) *Mazingira*

289. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Wizara itahakikisha inaongeza uelewa kwa wenye viwanda juu ya matumizi ya mitambo ya kisasa katika uzalishaji ili kupunguza utiririshaji wa majitaka hususan yale yaliyo na kemikali ambayo huchafua vyanzo vya maji na pia kwa viwanda kupunguza uzalishaji wa taka ngumu.

(c) *Kupambana na UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza*

290. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) mahala pa kazi kwa kutoa huduma bora kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI waliojiweka wazi kwa mujibu wa Mwongozo wa Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha watumishi juu ya masuala ya UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza pamoja na upimaji wa afya zao kwa hiari mara kwa mara.

(d) *Masuala ya Jinsia*

291. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2017/2018, Wizara kuititia Dawati la Jinsia itatekeleza yafuatayo:

- i) Kuhuisha masuala ya jinsia katika mipango ya uzalishaji wa mazao na mnyororo wa thamani katika bidhaa zinazozalishwa;
- ii) Kushiriki katika mikutano ya kitaifa na kimataifa katika masuala ya kijinsia; na

- iii) Kuandaa semina ya kuwajengea uwezo waratibu wa masuala ya jinsia Wizarani na katika Taasisi zilizo chini ya Wizara juu ya uratibu wa masuala ya jinsia, ufuatiliaji na tathmini.

5.3.4 Usimamizi wa Mapato na Matumizi

292. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuhakikisha kwamba, kila anayefanya biashara hapa nchini anakuwa na leseni halali inayolingana na biashara anayoifanya. Aidha, Maafisa Biashara wa Wizara na Kitengo cha Ufuatiliaji na Uperembaji (M & E Section) wakishirikiana na Maafisa Biashara walio katika Halmashauri na Manispaa zote nchini watafanya ukaguzi na kuchukua hatua za kisheria kwa mfanyakia biashara yejote atakayepatikana akifanya biashara bila leseni au leseni stahiki.

293. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itahakikisha inafanya matumizi kulingana na kanuni, taratibu na sheria za fedha za Serikali. Matumizi yote yatafanyika kulingana na mpangilio wa Bajeti ya Wizara (objective, targets and activities). Wizara katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, itaendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kiweze kuhakikisha taratibu zote za fedha zinafuatwa na malipo yanafanyika kulingana na vipaumbele vilivyowekwa kwenye Bajeti ya Wizara. Aidha, Wahasibu wataendelea kupewa mafunzo ili kupanua taaluma zao na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Pia yatafanyika mafunzo ya muda mfupi kazini juu ya sheria, taratibu na kanuni za fedha na manunuzi ya umma kwa Wahasibu, Maafisa Ugavi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakurugenzi na Wahasibu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Lengo ni kuwapa mwangaza wa kuzijua sheria, taratibu na kanuni za msingi juu ya usimamizi wa fedha za Serikali. Mtumishi atakayefanya kinyume, sheria itachukua mkondo wake.

294. *Mheshimiwa Spika*, baada ya maelezo hayo naomba sasa niwasilishe maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018.

6.1 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

6.2 MAPATO YA SERIKALI

295. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi **20,000,000,000** kutokana na ada za leseni, uuzaji wa nyaraka za zabuni na faini kwa kukiuka sheria ya leseni za biashara.

6.3 MAOMBI YA JUMLA YA FEDHA

296. *Mheshimiwa Spika*, maombi ya fedha kwa ajili ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka 2017/2018 yapo katika Mafungu Mawili ambayo ni Fungu 44 (Viwanda) na Fungu 60 (Biashara na Uwekezaji). Kwa mwaka 2017/2018, Wizara imetengewa kwa Fungu 44 na Fungu 60 jumla ya Shilingi **122,215,109,750** kwa Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha, hizo Matumizi ya Kawaida ni Shilingi **42,024,732,750** na Matumizi ya Maendeleo ni Shilingi **80,190,377,000**.

6.4 MAOMBI YA FEDHA FUNGU 44

297. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Fungu 44 (Viwanda) imetengewa jumla ya Shilingi **98,012,870,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi **24,172,493,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **73,840,377,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa zinajumuisha Shilingi **4,569,373,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na Shilingi **19,603,120,000** kwa ajili ya Mishahara (PE). Kati ya fedha za Mishahara zilizotengwa, zinajumuisha **Shilingi 3,289,552,000** za Mishahara ya Wizara na Mishahara ya Mashirika chini ya Wizara (**Fungu 44**) **Shilingi 16,313,568,000**. Aidha, fedha za Matumizi Mengineyo yaani **Shilingi 4,569,373,000** ni kwa ajili

ya Wizara (**Fungu 44**). Mashirika chini ya Wizara (**Fungu 44**) kwa mwaka huu wa fedha hayakutengewa Matumizi Mengineyo (OC).

298. *Mheshimiwa Spika*, fedha za Matumizi ya Maendeleo **Shilingi 73,840,377,000** zilizotengwa, zinajumuisha **Shilingi 73,575,068,000** fedha za ndani na Shilingi **265,309,000** fedha za nje. Aidha, katika fedha za ndani, **Shilingi 10,960,000,000** sawa na **asilimia 15** ya fedha za Matumizi ya Maendeleo ni kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 62,615,068,000** sawa na **asilimia 85** ya fedha za Matumizi ya Maendeleo ni kwa ajili ya Mashirika chini ya Wizara. Fedha za nje zote ni kwa ajili ya taasisi chini ya Wizara hususan katika kuboresha viwango katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

6.5 MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO ZA NDANI

299. *Mheshimiwa Spika*, fedha za ndani za Maendeleo, zimeelekezwa katika miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Miradi Mikubwa ya Kielelezo; Miradi ya Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO Kibaha; Kuendeleza Kongano za Viwanda; Kuendeleza Tafiti za Maendeleo ya Viwanda; Kuendeleza Viwanda Vidogo, Biashara Ndogo, Ujasiriamali na Kuongeza mtaji kwenye Mfuko wa NEDF.

300. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 200,000,000** sawa na **asilimia 0.3** ya Bajeti ya Maendeleo (**Fungu 44**), zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza Miradi Mikubwa ya Kielelezo katika kuratibu na ufuutiliaji wa kazi za miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga katika Mkoa wa Njombe. Aidha, jumla ya **Shilingi 2,070,000,000** sawa na **asilimia 2.8** ya Bajeti ya Maendeleo (**Fungu 44**) zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda ambayo ni pamoja na Mradi wa Magadi Soda katika Bonde la Engaruka na Mradi wa Kufufua Kiwanda cha Matairi (General Tyre) Arusha.

301. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 26,559,200,000** sawa na **asilimia 36.2** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi ili kuchochaea ukuaji wa uchumi. Kanda hizo ni:- Kanda ya Bagamoyo (Technological Park), Tanga, Kigoma, Ruvuma na Manyoni ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Kituo cha Biashara cha Kurasini; hususan katika kukamilisha malipo ya fidia kwa wakazi watatu ambao nyumba zao hazikuthaminiwa hapo awali baada na Mthamini Mkuu wa Serikali wakati wa zoezi la uthamini.

302. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 12,939,068,000**. sawa na **asilimia 17.6** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO, Kibaha ikiwa ni pamoja na kuendeleza viwanda vya nguo na Kiwanda cha Matrekta cha (URSUS). Vilevile, jumla ya **Shilingi 10,500,000,000** sawa na **asilimia 14.3** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya Kuendeleza Kongano za Viwanda hususan Kongano la Ngozi na Bidhaa za Ngozi Dodoma. Kimsingi, Kongano husaidia kuondoa changamoto za miundombinu duni, ukosefu wa mitaji, masoko na teknolojia duni na kuleta ufanisi kwenye viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

303. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 6,500,000,000** sawa na **asilimia 8.9** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44), zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza tafiti za maendeleo ya viwanda katika taasisi za TIRDO, TEMDO na CAMARTEC.

304. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi 14,146,800,000** sawa na **asilimia 19.3** ya Bajeti ya Maendeleo, zimetengwa kwa ajili ya Kuendeleza Viwanda Vidogo, Biashara Ndogo na Ujasiriamali ikiwa ni pamoja na kujenga maeneo ya viwanda katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara, Njombe, na Simiyu; Kutekeleza Mkakati wa Wilaya Moja Biadhaa (ODOP), na kuuongezea mtaji Mfuko wa NEDF. Vilevile, jumla ya **Shilingi 460,000,000** sawa na **asilimia 0.6** ya Bajeti ya Maendeleo (Fungu 44) , zimetengwa kwa ajili ya **Counter part funds** katika miradi ya *Gender, Trade Mainstreaming, KAIZEN Program,*

na *UNIDO Programme*. Mchanganuo wa matumizi ya fedha za maendeleo unapatikana katika Kitabu cha nne cha Makadirio ya Fedha za Serikali kwa mwaka 2017/2018 katika Fungu 44.

6.6 MAOMBI YA FEDHA FUNGU 60

305. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Fungu la 60:Biashara na Uwekezaji imetengewa jumla ya Shilingi **24,202,239,750** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, Shilingi **15,964,331,000** ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **6,350,000,000** ni ya Bajeti Matumizi ya Maendeleo.

306. *Mheshimiwa Spika*, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 1,887,908,750** za Matumizi Mengineyo na **Shilingi 14,076,422,250** kwa ajili ya Mishahara.KatiyafedhazilizotengwakwaajiliyaMatumiziMengineyo zinajumuisha **Shilingi 1,805,185,000** za Matumizi Mengineyo ya Wizara na **Shilingi 82,723,750** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo kwa taasisi chini ya Wizara. Aidha, kati ya fedha ilizotengwa kwa ajili ya Mishahara zinajumuisha **Shilingi 1,116,186,000** Mishahara ya Wizara na **Shilingi 14,848,145,000** Mishahara ya taasisi chini ya Wizara (Fungu 60).

6.7 MATUMIZI YA FEDHA ZA MAENDELEO

307. *Mheshimiwa Spika*, kati ya **Shilingi 6,350,000,000** Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo zilizotengwa kwa mwaka 2017/2018 (Fungu 60), **Shilingi 2,000,000,000** ambazo ni **asilimia 31.5** ya fedha za Fungu 60 zimetengwa kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 4,350,000,000** ambazo ni **asilimia 65.5** zimetengwa kwa ajili ya taasisi chini ya Wizara. Fedha hizo zimeelekezwa katika Mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) na Mradi wa Kuimarisha taasisi chini ya Wizara (*Institution Support*) mtawalia.

308. *Mheshimiwa Spika*, katika fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya kuimarisha taasisi chini ya Wizara zinajumuisha **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya

kuboresha miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) hususan kuchangia katika kujenga jengo la maabara ya kisasa litakalokuwa na ghorofa sita; **Shilingi 1,650,000,000** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uhakiki na upimaji (*Secondary and working standards*) kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa Wakala wa Vipimo; **Shilingi 500,000,000** kwa ajili ya kuendeleza biashara hususan kuandaa Mpango Kabambe wa Kuboresha Miundombinu ya Uwanja wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa wa Mwalimu Julius K. Nyerere Barabara ya Kilwa Dar- es Salaam, na **Shilingi 200,000,000** kwa ajili ya kuboresha Mfumo wa Usajili wa Kazi za Wanachama wa COSOTA wanaojishughulisha na kazi za ubunifu kwa njia ya mtandao.

309. *Mheshimiwa Spika*, katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP), **Shilingi 2,000,000,000** zimetegwa kwa ajili ya kukuza masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha mnyororo wa thamani na kuwezesha wakulima kuunganishwa na masoko; Kufanya tafiti za mwenendo wa masoko ya mazao makuu ya chakula na mifugo; kufuatilia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Zao la Korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara na Pwani; na Kupanua wigo wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa mazao ya alizeti, mahindi, mchele, na ufuta.

310. *Mheshimiwa Spika* mchanganuo wa fedha za Matumizi ya Maendeleo unapatikana katika Kitabu cha Nne cha Makadirio ya Fedha za Serikali kwa mwaka 2017/2018 katika Fungu: 60.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, wajenzi wa nchi ni wananchi.

Hivyo, napenda kuwashukuru kwa dhati Watanzania wote kwa uzalendo wenu wa kuitendea haki na kuipigania kwa kauli na vitendo ajenda ya kitaifa ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ndiyo, tumepega hatua kwenda mbele, lakini inatubidi kuongeza nguvu, mbinu na maarifa zaidi ili vita hiyo iwe na medani zinazokidhi aina na namna ya mapambano ya kiushindani yaliyopo na yajayo. Siri ya wazi ya ushindi ni uwajibikaji wa kila mmoja wetu na kuwepo ushirikiano usio na shaka na endelevu wa wadau wetu. Serikali kwa upande wake itaendeleza na kuboresha ulinzi kwa sekta, kuweka mazingira ya uwekezaji, uendelezaji, ujenzi na uboreshaji wa viwanda, biashara na masoko ili wadau wote waweze kutumia ipasavyo fursa zilizopo na zijazo. Naomba Watanzania wote na wote wenye mapenzi mema kwa nchi yetu muendelee kutuamini na kutupa ushirikiano unaohitajika. Tunaamini tuko katika njia na mwelekeo sahihi. Sasa tusonge mbele kwa pamoja kwa nia na ari moja

311. *Mheshimiwa Spika*, Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara www.mit.go.tz.

312. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

